

**ULUMBILUGHNA NA ATHARI ZAKE KATIKA UANDISHI WA INSHA ZA  
SHULE ZA MSINGI YA CGHU NA MOI AVENUE; KIFANI CHA SHENG NA  
KIINGEREZA KWA KISWAHILI**

**NA  
HYLINE MONCHARI NYARUNDA  
C50/85215/2016**

**WASIMAMIZI**

- 1. DKT. JEFWA MWERI**
- 2. MS. JUDY ONYANCHA**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA  
SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI, IDARA YA  
KISWAHILI**

**UNGAMO**

Tasniifu hii ni kazi yangu binafsi na haijawasilishwa kwa mahitaji ya Shahada katika Chuo kingine chochote kile.

Sahihi.....*lififi*..... Tarehe 22-2-2022

**HYLINE MONCHARI NYARUNDA**

**C50/85215/2016**

(Mtahiniwa)

Tasniifu hii imewasilishwa kwa madhumuni ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi kupitia Idara ya Kiswahili.

Sahihi.....*J. M. O. M.*..... Tarehe 01/03/2022

**DKT. JEFWA MWERI**

(Msimamizi)

Sahihi.....*J. M. O. M.*..... Tarehe 03/03/2022

**MS. JUDY ONYANCHA**

(Msimamizi)

## **TABARUKU**

Tasnifu hii naitabarukia mwanangu Jecinta Faith na wazazi wangu Bw.Wilfred na Bi.Pacificah ambao wamekuwa nguzo muhimu katika masomo yangu kuanzia shule ya msingi hadi uzamili. Kwa muhibu Ben, asante kwa juhudini zako.

## **SHUKRANI**

Safari ya kukamilisha tasnifu ilikuwa na changamoto si haba, ila nashukuru kwa mawaidha, uelekezi na mawazo ya watu mbalimbali. Mchango wao mkubwa ulirahisisha changamoto ambazo zilihusiana na utafiti huu. Natoa shukrani zangu kwa Mungu kwa kunipa afya njema katika kipindi hiki cha shahada ya uzamili na kuniwezesha kuikamilisha. Kwa neema ya Mungu tuliweza kuikamilisha tasnifu hii.

Ningependa kuwashukuru wasimamizi wangu, Dkt. Jefwa Mweri na Judy Onyancha kwa kujitolea kwao kusoma na kunipa marekebisho yaliyonifaa kwa wakati ufaao katika kukamilisha kazi hii. Walijitolea mhanga kunielekeza kila nilipowatumia kazi yangu. Walinihudumia kila nilipowahitaji ingawa walikuwa na majukumu si haba chuoni na katika familia zao. Nawashukuru kwa mawaidha na maelekezo yao ya kitaaluma ambayo yalinifaa si haba. Mungu awabariki na awaongezee hekima, mwendelee kuwahudumia wanafunzi wengine.

Namshukuru mtoto wangu, Jecinta Faith kwa kunivumilia kipindi cha utafiti wangu. Nililazimika kushughulikia utafiti wangu na kumnyima nafasi ya kutangamana naye hata wakati wa usiku.

Nawashukuru dada na ndugu zangu kwa kusimama nami katika kipindi cha utafiti huu. Vile vile, siwezi kuwasahau marafiki wangu Ruth na Lidya kwa kunipa moyo hata wakati nilikuwa nimekosa tumaini la kukamilisha tasnifu hii. Mungu awabariki.

Siwezi kuwasahau wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Nairobi hasa wale wa Idara ya Kiswahili kwa kunipa mwongozo uliofaa na kunifanya kuendelea na masomo yangu. Nawashukuru, Prof. Hezron Mugambi, Dkt. Jefwa Mweri, Prof. Iribemwangi, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Jerono, Dkt. Swaleh, Prof. Rayya Timammy na Ms. Judy Onyancha. Mungu awabariki kwa kujitolea kwenu kuhudumia wanafunzi.

Safari hii tulianza na wanafunzi wenzangu na ambao tulitiana moyo sana. Marehemu Grace Mutahi, lala salama, Dadangu Jackline Nyarunda, David Okeno, Kemunto, Lucy

Gatere, Wafula, Mwanarusi, Robert, Irene, Tunu Chombo, Gladys, Risasi, Fatma Ali, David Rachel, Mwaipaja, Poulet, Bridgit, Poline Kaaria, Opiyo, Brenda, Imani Hudaa, Ndegwa na wengineo asante kwa kukubali kushirikiana nami kipindi cha usomaji wetu.

Pia kwa njia ya kipekee ningependa kuwashukuru walimu wakuu wa shule za msingi ya Moi Avenue na ile ya CGHU kwa kuniruhusu kukusanya data ya utafiti shulenii mwao. Ninawashukuru walimu wezangu kwa kunitia moyo hadi tamati mwa tasnifu hii nao ni; Bi. Celina Thuku, Bi. Warui, Bw. Millar Kennedy na Dan Rawo wa Imara ECDE College

**MAELEZO YA ISTILAHI NA VIFUSHO VYA MANENO**

CGHU      Cutch Gujarati Hindu Union

SSD      Sri Saraswati Deepak

## **IKISIRI**

Utafiti huu ulinuia kuchunguza athari za ulumbilugha kwa Kiswahili. Tasnifu hii imegawanywa kwa sura tano. Katika sura ya kwanza tulishughulikia utangulizi wa kazi hii kwa ujumla kwa kuangazia tatizo la utafiti, maswali na malengo ya utafiti huu, sababu za kuchagua mada, yaliyoandikwa kuhusiana na mada yetu na vile vile mbinu za utafiti. Katika sura ya pili, tulishughulikia dhana za ulumbilugha na kuchanganya ndimi na hatimaye tuliangazia mielekeo ya wanafunzi kuhusu Kiingereza, Kiswahili na Sheng'. Tulijikita kwa athari hasi na chanya za Sheng' na Kiingereza kwa Kiswahili kwa kuangazia insha za wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue. Kutokana na data ya utafiti huu, tuligundua kuwa athari hasi ni nyingi zaidi ya athari chanya na hili ni jambo linalowafanya wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue kupata alama za chini katika uandishi wa insha za Kiswahili. Tulishughulikia athari hasi na chanya za sheng' na Kiingereza kimofolojia katika sura ya tatu na vile vile kisintaksia katika sura ya nne. Athari hasi za Sheng' na kimofolojia ambazo tulishughulikia ni: ukataji wa silabi za Kiswahili kwa namna isiyofaa, kuandika ukubwa na udogo wa nomino za Kiswahili visivyo na pia kunyambua vitenzi vya Kiswahili visivyo. Athari hasi za Kiingereza tulizobaini katika mofolojia ni uswahilishaji maneno ambayo yana msamati uliozoleka katika Kiswahili, matumizi ya konsonanti za Kiingereza katika uandishi wa insha, kutumia maneno ya Kiingereza na uambishaji wa maneno ya Kiswahili visivyo. Athari chanya ya ulumbilugha kimofolojia iliyobainika katika data ya utafiti huu ni ufahamu wa maana za maneno. Katika sintaksia, tulishughulikia athari hasi na chanya za ulumbilugha katika uandishi wa insha za Kiswahili. Tuliangazia sentensi katika insha za watafitiwa wetu na tuligundua kuwa athari hasi za Sheng' kisintaksia ni: matumizi ya mbinu ya uhuishaji pasipofaa, uongezeaji wa viambishi visivyo, kuendeleza misamati ya Kiswahili visivyo na matumizi ya maneno ya Sheng'. Tulibaini kuwa pia umilisi wa Kiingereza uliwaathiri kwa njia hasi kwa kuwa wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue wanaendeleza viambishi vya nafsi visivyo, matumizi mabaya ya vivumishi vya aina mbalimbali kama vile vivumishi vya a-unganifu, vionyeshi, vimilikishi, virejeshi na vile vya idadi. Athari hizi hasi zinaifanya sentensi kutokuwa sahihi na hivyo basi wanafunzi wanaadhibiwa kwa kufanya makosa ya kisarufi. Hatimaye, tulishughulikia athari chanya za ulumbilugha kisintaksia na tulibaini kuwa uliwawezesha wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue wanatunga sentensi ambazo zimekamilika kimaana, sahihi na kimantiki. Hatimaye tulishughulikia mahitimisho ya utafiti huu na mapendekezo kwa watafiti wa baadaye.

## YALIYOMO

UNGAMO.....	Error! Bookmark not defined.
TABARUKU .....	ii
SHUKRANI.....	iv
MAELEZO YA ISTILAHINI NA VIFUSHO VYA MANENO .....	vi
IKISIRI .....	vii
YALIYOMO.....	viii
SURA YA KWANZA .....	12
1.0 Utangulizi .....	12
1.1 Usuli wa Mada ya Utafiti .....	12
1.2 Tatizo la Utafiti .....	15
1.3 Maswali ya Utafiti .....	16
1.4 Malengo na Madhumuni ya Utafiti .....	16
1.5 Sababu za Kuchagua Mada .....	16
1.6 Upeo na Mipaka .....	18
1.7 Msingi wa Kinadharia .....	19
1.7.1 Nadharia ya kumudu .....	19
1.8 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada.....	23
1.9 Mbinu za Utafiti .....	28
1.9.1 Walengwa.....	29
1.9.2 Sampuli Kielelezo .....	29
1.9.3 Ala za Ukusanyaji Data.....	30
1.9.4 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data.....	30
SURA YA PILI.....	30

ULUMBILUGHA NA MIELEKEO KUHUSU SHENG', KIINGEREZA NA KISWAHILI .....	30
2.0 Utangulizi .....	30
2.1 Ulumbilugha.....	31
2.2 Athari za Ulumbilugha.....	33
2.2.1 Kuchanganya Ndimi.....	34
2.2.2 Uchopekaji wa Maneno ya Lugha Zingine Katikati ya Sentensi ya Kiswahili....	36
2.2.3 Uchopekaji wa Maneno ya Lugha Zingine Mwishoni mwa Sentensi ya Kiswahili.....	37
2.2.4 Uambatishaji Kiungo.....	38
2.3 Mielekeo Kuhusu Sheng', Kiingereza na Kiswahili .....	39
2.3.1 Mielekeo ya Wanafunzi Kuhusu Sheng' .....	39
2.3.2 Mielekeo ya Wanafunzi Kuhusu Kiingereza .....	41
2.3.3 Mielekeo ya Wanafunzi Kuhusu Kiswahili .....	45
2.4 Hitimisho.....	48
SURA YA TATU .....	49
ATHARI ZA KIINGEREZA NA SHENG' KWA MOFOLOJIA YA KISWAHILI KATIKA UANDISHI WA INSHA .....	49
3.0 Utangulizi .....	49
3.1. Athari za Sheng' Kimofolojia katika Uandishi wa Insha za Kiswahili .....	50
3.1.1 Ukataji Silabi za Kiswahili kwa Namna Isiyofaa.....	50
3.1.2.0 Kuandika Ukubwa na Udogo wa Nomino kwa Namna Isiyofaa .....	53
3.1.2.1 Kuandika Ukubwa wa Nomino kwa Namna Isiyofaa.....	54
3.1.2.2 Kuandika Udogo wa Maneno kwa Namna Isiyofaa.....	57
3.1.3 Mnyambuliko wa Vitenzi kwa Namna Isiyofaa.....	61
3.2 Athari za Kiingereza Kimofolojia katika Uandishi wa Insha za Kiswahili .....	63

3.2.1 Kuswahilisha Neno Kutokana na Msamati wa Kiingereza.....	64
3.2.2 Matumizi ya Konsonanti za Kiingereza Katika Uandishi wa Insha za Kiswahili	65
3.2.3 Kuchanganya Ndimi katika Uandishi wa Insha .....	68
3.3 Uambishaji .....	71
3.4 Athari Chanya za Ulumbilugha Kimofolojia Katika Uandishi wa Insha za Kiswahili .....	72
3.4.1 Ufahamu wa Maana za Maneno.....	72
3.5 Hitimisho.....	74
SURA YA NNE.....	75
ATHARI ZA KIINGEREZA NA SHENG' KISINTAKSIA KATIKA UANDIKAJI INSHA ZA KISWAHILI.....	75
4.0 Utangulizi .....	75
4.1 Athari za Kiingereza Kisintaksia katika Uandishi wa Insha za Kiswahili .....	76
4.1.1 Athari za Ulumbilugha Katika Kuandika Viambishi vya Nafsi.....	76
4.1.2 Matumizi Mabaya ya Vivumishi.....	79
4.1.2.1 Matumizi Mabaya ya Vivumishi vya –a-unganifu.....	80
4.1.2.2 Matumizi Mabaya ya Vivumishi Vionyeshi .....	82
4.1.2.3 Matumizi Mabaya ya Vivumishi Vimilikishi .....	84
4.1.2.4 Matumizi Mabaya ya Vivumishi Virejeshi .....	86
4.1.2.5 Matumizi Mabaya ya Vivumishi vya Idadi.....	90
4.2 Athari za Sheng' Kisintaksia Katika Uandishi wa Insha za Kiswahili .....	93
4.2.1 Matumizi ya Mbinu ya Uhuishaji Pasipofaa .....	93
4.2.2 Kuchopeka Silabi au Virejeshi Pasipofaa .....	95
4.2.3 Matumizi ya Maneno ya Kiswahili Visivyo .....	96
4.2.4 Matumizi ya Maneno ya Sheng' Katika Insha za Kiswahili.....	99
4.3 Athari Chanya za Ulumbilugha Katika Sintaksia .....	101

4.4 Hitimisho.....	103
SURA YA TANO .....	105
MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI .....	105
5.0 Utangulizi .....	105
5.1 Muhtasari.....	105
5.2 Mahitimisho Ya Utafiti .....	106
5.2.1 Athari Hasi za Sheng' na Kiingereza kwa Kiswahili katika Uandishi wa Insha za Wanafunzi wa Shule za Msingi za CGHU na Moi Avenue.....	106
5.2.2 Athari Chanya za Sheng' na Kiingereza kwa Kiswahili katika Uandishi wa Insha za Wanafunzi wa Shule za Msingi za CGHU na Moi Avenue .....	107
5.2.3 Sababu za Wanafunzi wa Shule za Msingi Kupendelea Sheng' au Kiingereza Zaidi Kuliko Kiswahili na Jinzi Mitazamo Yao ya Sheng' na Kiingereza Huathiri Maandishi Yao ya Insha za Kiswahili.....	107
5.3 Changamoto za Utafiti .....	107
5.4 Mapendekezo .....	108
MAREJELEO .....	109
VIAMBATISHO.....	114

## SURA YA KWANZA

### 1.0 Utangulizi

Utafiti huu ulilenga kuchunguza athari za ulumbilugha katika insha za wanafunzi wa shule za msingi. Tulijikita kwa athari hasi na chanya za Sheng' na Kiingereza kwa Kiswahili katika insha za wanafunzi wa shule teule za msingi. Sehemu hii inajumuisha vipengele vifwatavyo: Mwanzo ni usuli wa mada, pili ni tatizo la utafiti, tatu ni maswali ya utafiti, nne tuliangazia malengo, tano tulielezea sababu za kuchagua mada, sita ni upeo na mipaka, saba ni msingi wa kinadharia,nane ni yaliyoandikwa kuhusu mada na mwisho tuliangazia mbinu za utafiti.

### 1.1 Usuli wa Mada ya Utafiti

Lugha hutumiwa kufanikisha mawasiliano mionganoni mwa watumizi wake. Mawasiliano huchukuliwa kuwa yamefanikiwa iwapo kuna uelewano kati ya washiriki wake. Lugha mbalimbali huweza kutumiwa katika mawasiliano husika kwa nia ya kukidhi mahitaji kama vile kufidia msamati au kufafanua dhana fulani. Utumizi wa lugha mbalimbali hutegemea mazingira na hali ya watumizi wa hizo lugha. Hali hii hutokea kwa watu ambao ni walumbilugha. Kuna uwezekano wa mtu kutumia lugha tatu katika mawasiliano yake jambo ambalo linaweza kumwathiri kwa njia mbalimbali kwa mfano anapoandika kazi fulani kutumia lugha hizo. Jambo hili limechochea utafiti huu kwani wanawingilugha hupitia hali hii. Lengo la huu utafiti ni kuchunguza athari za ulumbilugha katika uandishi wa inshakwa kuangazia namna Sheng' na Kiingereza huathiri Kiswahili.

TUKI (1990) na Massamba (2004) wanaafikiana kuwa ulumbilugha ni sawia na wingilugha. Katika utafiti huu tulitumia dhana hizi kama visawe. Massamba anahoji kuwa ulumbilugha ni ule uwezo wa mzungumzaji kutumia lugha mbili na zaidi katika mazungumzo. Buliba na wenzake (2006) nao wanasema kuwa ulumbilugha ni ule uhodari wa kutumia lugha mbalimbali katika mazungumzo ili kufaulisha mawasiliano. Kwa hivyo basi, ulumbilugha ni hali ya mzungumzaji kuwa na uwezo wa kutumia lugha mbili au zaidi katika mawasiliano. Mwanaulumbilugha hutumia lugha azijuazo katika mazingira tofauti akiongozwa na nia ya mazungumzo yake na mazingira anamojipata. Wanaulumbilugha pia huweza kutumia lugha wazijuazo katika mazungumzo ili kuweza kujieleza ipasavyo na kutimiza jukumu lao la kimsingi la

kimawasiliano. Wanapofanya hivi, hata hivyo kuna athari ambazo zinaweza kujitokeza za mwingiliano wa lugha hizi wanazozifahamu.

Musau (2000) anayaona matumizi ya wingi lugha kama yanayochochewa na mahitaji mapya ya kimawasiliano yanayoendelea kuchipuka na kupanuka nje ya mawanda ya kawaida ya lugha ya binadamu. Maoni ya Musau yanaonyesha kuwa wanaulumbilugha hutumia lugha wazijuazo mara nyingi wakizichanganya katika mazungumzo yao ili kukidhi haja ya mawasiliano yao. Kwa hali hii, wanaulumbilugha hawawezi kuepuka kutumia lugha wazijuazo kwa kubadilisha au kuzichanganya katika mawasiliano yao.

Hivyo basi, mahitaji ya kutimiza malengo ya mawasiliano ya watu ndio huchochea matumizi ya wingilugha katika mawasiliano. Wanaulumbilugha hutumia lugha ambazo wanazifahamu kwa kuzibadilisha au kuzichanganya ili kujieleza ipasavyo na kwa hali hii kutimiza malengo ya mawasiliano yao. Bloomfield (1993) anauona wingi lugha kama umilisi kamilifu wa lugha mbalimbali kama ule wa mzawa wa lugha moja. Kwa mujibu wa Bloomfield, mtu huchukuliwa kuwa mwanawingi lugha wakati ana tajriba ya kutumia lugha mbalimbali kwa njia sawa. Hivi kwamba anao umilisi kamili wa lugha hizo zote. Maoni haya ya Bloomfield yanaonyesha kuwa sharti mwanawingi lugha awe na umilisi sawa wa lugha mbili au zaidi. Kwa upande mwingine, Mackey (1998) naye anachukulia wingilugha kama matumizi ya zamu au ya kubadilishana kwa lugha mbili au zaidi katika mazungumzo. Mackey anazungumzia suala la mwanawingilugha kuwa na uwezo wa kutumia lugha mbalimbali kwa kubadilishana. Kulingana naye, umilisi sio jambo la lazima kwa mwanawingilugha. Mackey anadai pia kuwa uwezo wa kutumia lugha azijuazo mtu katika mawasiliano ndio humfanya kurejelewa kama mwanawingilugha.

Utafiti huu ulizingatia maoni ya Massamba (2004) na Nsiga (2018) ambao wanauchukulia ulumbilugha kama uwezo wa mtu wa kutumia lugha mbili au zaidi katika mawasiliano. Kwao, suala la umilisi sawa wa lugha hizo sio la muhimu, mradi mtu anaweza kuwasiliana kwa lugha ambazo anazijua. Nsiga anazungumzia aina tatu za ulumbi ambazo hujitokeza kwa watu. Aina ya kwanza ni ulumbi taifa ambao unahu su kugawa lugha mbalimbali katika majukumu tofauti tofauti kama vile lugha ya kisheria, ibada na shule. Pili ni ulumbi wa taasisi ambao unahu su taifa kuzipa lugha mbili au zaidi hadhi sawa. Kwa mfano, nchini Kenya, Kiswahili na Kiingereza ni lugha rasmi kwa mujibu wa katiba ya mwaka wa 2010. Tatu ni ulumbi binafsi ambao unahu shisha hali ambapo mtu hutumia lugha mbalimbali katika mazingira tofauti.

Utafiti wetu unajikita katika aina hizi tatu za ulumbi kwa kuwa tulishughulikia lugha za Kiingereza na Kiswahili ambazo zimepewa nafasi ya kuwa lugha rasmi nchini Huku lugha ya taifa ikiwa ni Kiswahili. Kwa hali hii basi, utafiti huu ulijikita kwa hadhi ya lugha ya Kiswahili, Kiingereza na Sheng' katika uandishi wa insha za wanafunzi wa shule teule za msingi za CGHU na Moi Avenue. Uteuzi wa mada hii unasababishwa na hali kwamba Kiingereza na Kiswahili hutumiwa katika elimu nchini Kenya. Wanafunzi wanapaswa kutumia lugha hizi mbili katika uandishi wao ambapo Kiswahili hutumiwa katika somo lake huku Kiingereza kikitumika katika utahini wa masomo mengine isipokuwa Kiswahili. Hii inaonyesha kuwa Sheng' haina hadhi yoyote katika elimu. Kwa hivyo basi, matumizi yake wakati wa kuandika insha hayakubaliki. Ijapokuwa Kiingereza kina hadhi ya lugha rasmi, matumizi yake katika insha pia hayakubaliki. Kwa hivyo, utafiti huu uliangazia namna ujuzi wa lugha ya Kiingereza na ile ya Sheng' huathiri Kiswahili katika uandishi wa insha hasa ya shule za msingi nchini Kenya hasa katika viwango vya isimu vyaa mofolojia na sintaksia.

Matumizi ya lugha mbalimbali ambazo mtu anazijua huchukuliwa kama jambo la kimsingi katika mawasliano ya kawaida. Katika mawasliano rasmi, wazungumzaji hawana budi kutumia lugha inayokubalika na kueleweka na washiriki wake na ni nadra kwa wazungumzaji katika hali rasmi kutumia lugha zaidi ya moja katika mazungumzo yao. Lugha itakayotumiwa katika mazungumzo fulani rasmi huchochewa na hadhira na mada inayozungumziwa. Hali hii ni tofauti katika mazungumzo ya kawaida ambapo wazungumzaji hutumia lugha wazijuazo katika mazungumzo yao. Ingawa hivyo, hali inakuwa tofauti kwa wasomi wa shule za msingi wanapoandika insha hasa wale wanaoishi katika mazingira ya wingilugha. Hii ni kwa sababu wanafunzi hutahiniwa kwa kutumia aidha lugha ya Kiingereza au ya Kiswahili nchini Kenya. Suala la kutumia lugha zaidi ya moja katika mtihani huchukuliwa kuwa kosa na adhabu hutolewa. Kwa mfano katika uandishi wa insha mwanafunzi anayetumia maneno ya Sheng' au Kiingereza huadhibiwa kwa kutolewa nusu alama kwa kila kosa la kisarufi. Hali hii huwaathiri wasomi wa shule za msingi kwa njia hasi. Hivyo basi, utafiti huu uliangazia athari za ulumbilugha kwenye uandishi wa insha kwa kujikita kwenye athari za Sheng' na Kiingereza kwa Kiswahili ili kuweza kutoa suluhu kwa swali hili.

Utafiti huu unanuia kuonyesha namna wanafunzi wa shule ya msingi hutumia lugha wazijuazo na namna matumizi ya lugha hizi huathiri maandishi yao ya insha. Katika utafiti huu tulijikita

katika taaluma ya isimujamii tukifuata maoni ya Spolsky (1998) na Trudgill (2000) ambao wanaafikiana kuwa isimujamii hushughulikia namna jamii hutumia lugha huku wakichochewa na hali na muktadha wa mazungumzo. Kujikita kwetu katika isimujamii kulituwezesha kuelezea athari zitokanazo na ulumbilugha katika muktadha wa maandishi insha za wanafunzi. Tulijikita katika athari ya Sheng' na Kiingereza katika uandishi wa insha jambo ambalo huwafanya kuadhibiwa kwa kutolewa alama nusu kwa makosa ya hijai na yale ya kisarufi.

## 1.2 Tatizo la Utafiti

Lugha huwa kiungo dhabiti katika kufanikisha mawasiliano. Nyenzo za mawasiliano zaweza kuwa kupitia kwa mdomo, lugha ishara au kwa maandishi. Wanafunzi wa shule za msingi wanapoandika insha za kiswahili hukumbwa na changamoto kama vile matumizi ya lugha zingine katika insha hizo jambo lisiloruhusiwa katika utahini. Wanafunzi wa shule za msingi kama vile za CGHU na ile ya Moi Avenue jijini Nairobi hutumia lugha ya Kiswahili, Sheng' na Kiingereza katika mawasiliano yao shulen. Wanafunzi hawa hutumia lugha hizi kwa kubadilishana wanapozungumza. Kwa hali hii wanafunzi huchanganya lugha hizi tatu katika mawasiliano yao wanapozungumza na hili ni jambo ambalo linaweza kuathiri uandishi wao wa insha pia. Inaelekea kuwa lugha hizi tatu basi zitaathiriana kwa njia mbalimbali.

Mtafiti alitathmini athari za Sheng' na Kiingereza katika Kiswahili kwa kujikita kwa makosa ya mofolojia na sintaksia yanayobainika katika insha za wanafunzi. Tunajikita kwa matapo haya ya kiisimu kwa kuwa athari za lugha fulani kwa lugha nyingine huonekana katika neno. Kwa mfano, iwapo neno litaendelezwa visivyo basi huathirika kama wasemavyo Apel(2014) na Anglin (1993). Kwa hivyo makosa mengi hujitokeza katika mofolojia na katika sintaksia na kuzua athari hasi kwa wanafunzi hasa wanapoandika insha katika lugha ya Kiswahili na ambayo pia ni lugha ya taifa. Hivyo basi utafiti huu ulichunguza athari za Sheng' na Kiingereza ambazo hutumiwa sambamba na lugha ya Kiswahili katika uandishi wa insha za wanafunzi wa shule za msingi tukizingatia kwamba uchanganyaji lugha shuleni huwa na athari hasi na chanya katika elimu ya wanafunzi hasa wa shule za msingi. Kwa mfano, athari hizi huweza kujitokeza katika uandishi wa insha za wanafunzi na kwa njia hii kufanya matokeo yao kuwa duni. Utafiti huu hivyo basi uliangalia sababu ambazo huwafanya wanafunzi wa shule za msingi kupendelea kutumia elementi za sarufi ya Sheng' au Kiingereza katika insha badala ya kutumia Kiswahili sanifu. Tulitizama pia jinsi mitizamo ya wanafunzi hawa kuhusu lugha ya Sheng na Kiingereza

inavyoathiri matumizi ya Kiswahili katika maandishi. Hali hii ndio inatufanya kuamini kuwa zipo athari chanya za Sheng' na Kiingereza kwa Kiswahili katika elimu ya wanafunzi wa shule za msingi.

### **1.3 Maswali ya Utafiti**

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo

- i. Je, Sheng' na Kiingereza zina athari zipi hasi katika uandishi wa insha za wanafunzi wa shule za msingi na athari hizi hujitokeza kivipi?
- ii. Athari chanya za Sheng na Kiingereza kwa lugha ya Kiswahili katika elimu ya wanafunzi wa shule za msingi hujitokeza kivipi?
- iii. Je, ni kwa jinsi gani mitizamo ya wanafunzi hawa kuhusu lugha hizi za Kiswahili, Sheng' na Kiingereza huathiri maandishi yao ya insha?

### **1.4 Malengo na Madhumuni ya Utafiti**

Utafiti huu unalenga kuchunguza na kutathmini athari za Sheng' na Kiingereza katika Kiswahili kwa kujikita kwa makosa katika viwango vya kimofolojia na kisintaksia.

Utafiti huu uliongozwa na madhumuni yafuatayo:

- i. Kuchanganua athari hasi za Sheng' na Kiingereza kwa Kiswahili katika uandishi wa insha za wanafunzi wa shule za msingi.
- ii. Kuchunguza athari chanya za Sheng' na Kiingereza kwa Kiswahili katika uandishi wa insha za wanafunzi wa shule za msingi.
- iii. Kuchanganua sababu ambazo huwafanya wanafunzi wa shule za msingi kupendelea Sheng' au Kiingereza zaidi kuliko Kiswahili na jinsi mitizamo yao ya Sheng na Kiingereza huathiri maandishi yao ya insha za Kiswahili.

### **1.5 Sababu za Kuchagua Mada**

Shule ya msingi ya CGHU na ile ya Moi Avenue zinapatikana katikati mwa jiji kuu la Nairobi. Hizi ni shule za msingi za umma ambazo wanafunzi wake hutoka mitaa inayozunguka jiji kama vile Majengo, Kariwa, Kariokor, Landmawe, Gikomba na Muthurwa. Idadi kubwa ya wanafunzi hawa huingiliana na wachuuzi wajapo shuleni na warudipo nyumbani. Wanafunzi hawa pia

huhusika katika uchuuzi wa matunda, njugu na peremende watokapo shulen na wakati wa wikendi. Hali hii huwafanya wanafunzi kuwasiliana kwa kuchanganya lugha mbalimbali katika mazingira wanamojikuta. Wanapokuwa shulen hutakikana kutumia kiingereza na Kiswahili sanifu. Hivyo basi katika mawasiliano yasiyo rasmi wanafunzi huchanganya ndimi kutokana na mazoea. Uchanganyaji ndimi huu wa Sheng', Kiswahili na Kiingereza huathiri uandishi wa insha za wanafunzi hawa kwa sababu, kulingana na mtaala wa shule, lugha ya Kiingereza hutumika katika utahini wa masomo mengine isipokuwaa Kiswahili.

Shule mbalimbali nchini Kenya huwa na sera zao za lugha kama asemavyo Amollo (2012). Anaendelea kusema kuwa zipo changamoto za kiusimamizi wa shule ambazo huwafanya wanafunzi kutumia lugha ya Kiingereza zaidi wanapokuwa shulen. Shule ya msingi ya CGHU hajjaweka sera zozote za lugha ambazo zinapaswa kufuatwa na wanafunzi ilhali shule ya Moi Avenue ina sera kama vile kutumia Kiingereza kuanzia Jumatatu hadi Alhamisi huku Kiswahili kikutumika Ijumaa pekee. Sera hizi huwekwa na usimamizi wa shule na walimu wa lugha ili kuwafanya wanafunzi kutumia lugha ya Kiingereza na Kiswahili ambazo hutumiwa katika mitihani. Kama asemavyo Amollo changamoto za kiusimamizi wakati mwingine huwafanya wanafunzi kutumia lugha fulani na kupuuza nyingine. Ukosefu wa sera ya lugha katika shule ya msingi ya CGHU uliwapa wanafunzi fursa ya kutumia lugha yoyote ile ikiwemo Sheng' shulen. Hali hii ya uhuru wa matumizi ya lugha yoyote ile shulen huwa na athari zake katika uandishi wainsha za wanafunzi. Athari hizi zaweza kuwa chanya au hasi. Ndiposa tulifanya utafiti huu ili kuchanganua athari hizi katika maandishi ya insha za wanfunzi wa shule hizi za msingi na kutoa mapendekozo yatakayopelekea kuboresha elimu ya wanafunzi wa wingilugha.

Kiswahili ni lugha ya taifa na vile vile rasmi nchini Kenya na hivyo basi, kinapaswa kutumiwa kwa ustadi katika mawasiliano. Kwa hali hii basi, tunatarajia kuwa wanafunzi wa shule teule za msingi watatumia Kiswahili bila kuchanganya na lugha zingine. Hata hivyo sivyo mambo yalivyo kwa sababu ya athari zinazotokana na ulumbilugha. Lugha ya Kiingereza ina hadhi ya kuwa rasmi nchini Kenya. Kwa hali hii basi, wanafunzi wanapaswa kutumia lugha rasmi katika maandishi bila kuchanganya na lugha zingine. Hii ina maana kuwa wanafunzi wanapaswa kuzingatia kanuni za kisarufi za lugha ya Kiswahili katika uandishi wa insha. Kwa upande mwingine, Sheng' inaenea na inaathiri matumizi ya Kiswahili katika mawasiliano. Matumizi ya maneno ya Sheng' au Kiswahili huwafanya kuelewa dhana husika zaidi na kuzihuzisha katika

mazingira yao. Hali hii yaweza kuwa na athari aina mbili. Kwanza wanafunzi hawa wanaweza kupuuza dhana za kisayansi na badala yake kutumia maneno ya Sheng' au Kiswahili. Hii ni athari hasi na inaweza kujitokeza kwa somo la Kiswahili kwa kuathiriwa na Sheng' na Kiingereza. Kwa upande mwingine, wanafunzi wanaweza kuelewa dhana za kisayansi zaidi kwa kuwa wanatumia maneno ambayo wanayaelewa zaidi. Athari chanya inajitokeza katika hali hii. Athari za ulumbilugha basi zitajitokeza katika somo la Kiswahili katika elimu ya wanafunzi wa shule ya CGHU na ile ya Moi Avenue. Utafiti huu ulishughulikia athari hizi hasi na chanya katika viwango vya isimu vya kimofolojia na kisintaksia katika uandishi wao wa insha.

## **1.6 Upeo na Mipaka**

Uchunguzi huu wa kitaalamu ulishughulikia ulumbilugha na athari zake katika uandishi wa insha za wasomi wa shule ya CGHU na ile ya Moi Avenue. Utafiti huu tuliangazia athari za lugha ya Sheng' na ile ya Kiingereza katika insha za Kiswahili. Tuliangazia maandishi ya wasomi wa shule teule za msingi zipatikanazo katikati mwa jiji la Nairobi. Mtafiti alichunguza mazungumzo yao na kuangazia namna mazungumzo hayo huathiri uandishi wa wanafunzi wa shule ya msingi ya CGHU na ile ya Moi Avenue jijini Nairobi. Hii ni kutokana na ukweli kuwa ulumbilugha huchochea suala la uchanganyaji lugha katika mawasiliano. Wanafunzi ambao huchanganya ndimi katika mazungumzo yao huweza kujipata wakitumia lugha kwa namna hiyo hiyo katika uandishi.

Hii ndio maana tuliangazia pia mazungumzo yao na kuangazia namna yaliathiri uandishi wao wa insha. Katika maandishi tulijikita zaidi kwa insha za Kiswahili za wanafunzi wa darasa la nne hadi nane. Hii ni kwa sababu, wanafunzi huanza kuandika insha katika darasa la nne na hivyo basi tulikuwa na data kutoka darasa hili. Tuliangazia pia insha za darasa la nane, ambalo ni la mwisho katika elimu ya msingi. Wanafunzi wa darasa la nane walikuwa na uzoefu wa kuandika insha. Hii ndio sababu tuliangazia insha zao na kutaka kujua iwapo wanazingatia sheria za uandishi wa insha. Tulichunguza namna Sheng' na Kiingereza huathiri Kiswahili kutokana na ulumbilugha katika uandishi wa insha hizo. Utafiti ulishughulikia athari hizo katika viwango vya kimofolojia na kisintaksia kwa kubainisha makosa ambayo hutokana na athari za ulumbilugha kwa wanafunzi wa shule za msingi katika uandishi wao wa insha ya Kiswahili. Tulibainisha ni wanafunzi wa kiwango kipi ambao huathirika zaidi na ulumbilugha katika uandishi wa insha na kuelezea sababu zake.

Utafiti huu ulikitwa katika shule za msingi mbili: ile ya CGHU na ile ya Moi Avenue. Shule hizi zinapatikana katikati mwa jiji la Nairobi na kwa sababu hii, wengi wa wanafunzi wake hutoka maeneo yanayolizunguka jiji kama vile Muthurwa, Kariwa, Kariokor, Kirinyaga, Majengo na Gikomba. Hizi ni shule za serikali zilizo na wanafunzi takribani 700 na ambao wengine wao huhusika katika uchuuzi wa bidhaa kama vile njugu jijini Nairobi hivyo basi huwa kwa kiasi kikubwa kunatokea uchanganyaji ndimi katika mawasiliano yao. Utafiti uliangazia mazungumzo yao hasa wanapokuwa nje wakati wa mapumziko ili kubaini matumizi yao ya lugha ya Kiingereza, Sheng' na ile ya Kiswahili. Mazungumzo haya yalitupa mwanga wa namna wanavyotumia lugha hizi na jinsi inavyoathiri uandishi wao wa insha.

Utafiti uliangazia athari chanya na hasi zitokanazo na ulumbilugha katika uandishi wa insha za wanafunzi wa shule ya msingi ya CGHU na Moi Avenue. Tulitaka kubaini sababu ambazo huwafanya wanafunzi wa shule ya CGHU na Moi Avenue kutumia lugha hizi tatu katika mazungumzo yao ilhali wanajua vizuri masharti ya utahini wa mitihani kama walivyoolezwa na walimu wao kwa nia ya kuwafanya kufaulu mtihani hasa ule wa insha za Kiswahili. Inawezekana ulumbilugha huwawezesha wanafunzi kujieleza ipasavyo katika uandishi wa insha na hii ni athari chanya.

## **1.7 Msingi wa Kinadharia**

Nadharia zilizoongoza utafiti huu ni pamoja na nadharia ya kumudu ambayo imeasisiwa na Gibson (1986) na ile ya uchanganuzi makosa yake Corder (1960). Nadharia hizi zilituwezesha kuchambua athari hasi na chanya zitokanazo na lugha za Sheng' na Kiingereza katika uandishi wa insha za Kiswahili kuititia kwa makosa ya wanafunzi. Nadharia ya kumudu ni mwafaka katika utafiti huu kwa kuwa inashughulikia masuala ya ulumbilugha huku ile ya uchanganuzi makosa ikiangazia makosa yanayojitokeza katika mawasiliano. Tuliongozwa na mihimili ya nadharia hizi kama ilivyojitekeza katika vijishehemu vifuatavyo.

### **1.7.1 Nadharia ya kumudu**

Nadharia hii iliasisiwa na Gibson(1977; 1986). Nadharia hii imeweza kutazamwa kwa njia ya kiisumu na kiisimujamii. Nadharia hii imekuzwa pia na wasomi kama vile Aronin na Singleton (2007, 2010 na 2012), na Dewaele (2010).

Wasomi, Aronin na Singleton ndio walifuata mkabala wa isimujamii katika kueleza mihimili ya nadharia hii ya kumudu ndiposa tulikita utafiti wetu kwa maoni yao. Gibson (1977) alishughulikia nadharia ya kumudu kwa kutumia wanyama. Alitaka kujua uhusiano uliopo baina ya wanyama na mazingira yao. Aligundua kuwa mazingira huathiri tabia za wanyama. Katika mwaka wa 1986, Gibson alishughulikia namna watu hutumia lugha kwa misingi ya mazingira yao. Aligundua kuwa huwezi kutenganisha lugha inayotumiwa na mazingira. Anasema kuwa watu hutumia lugha mbalimbali katika mazingira mbalimbali. Hii inaonyesha kuwa wana ulumbilugha huamua lugha ipi itumike wapi na vipi. Uamuzi wa lugha ipi itumike wapi na vipi huathiriwa na hali, nia na muktadha wanamojipata wazungumzaji. Aronin na Singleton (2007) waliangazia madai haya ya Gibson kuhusu nadharia ya kumudu kwa mkabala wa isimujamii. Wanasema kuwa watumizi lugha hujua uwezekano na umuhimu wa kutumia lugha mbalimbali katika muktadha mmoja. Wazungumzaji hawa hutumia lugha ambazo wanazijua na huzitumia iwapo zitaafiki muktadha wa mazungumzo. Walijikita katika elimu na wanasema kwamba wanafunzi hupata ujuzi wa lugha fulani wakati fulani na mahali fulani kutegemea na ujuzi wao katika lugha zingine na namna lugha hizo zitawasaidia katika kutimiza malengo yao ya kiakademia.

Aronin na Singleton (2010) wanakubaliana na maoni ya Gibson(1986) kuwa kumudu lugha huambatana na tabia za wanafunzi na wanaozungumza nao na vilevile lugha wanayofunziwa shulen. Hali hizi huwafanya wanafunzi kuwa na upekee wa kumudu lugha fulani na kuzitumia lugha hizi mbalimbali kama mtu binafsi. Hivi kwamba, hali ya kumudu lugha fulani hutofautiana kutoka kwa mwanafunzi mmoja hadi mwingine. Aronin na mwenzake wanatoa mfano wa kumudu lugha mbalimbali na kusema kuwa wanafunzi ambao walikulia mazingira ambamo watu wanatumia lugha ya kwanza huweza kuchukua muda kuelewa lugha inayofunzwa shulen au lugha ya taifa ingawa wamo katika mazingira sawa kama vile nchi moja yenye lugha ya taifa.

Katika mwaka wa 2012, Aronin na Singleton walirejelea tena nadharia ya kumudu. Waliongezea suala la aina za kumudu lugha. Wanaelezea kategoria mbili za kumudu lugha: kwanza, umudu lugha wa jamii na pili, umudu lugha wa kibinafsi. Wanasema kuwa umudu lugha wa kijamii huathiri umudu lugha wa kibinafsi. Wanaelezea kuwa umudu lugha wa kijamii unahusisha lugha ambazo huzungumzwa katika jamii. Wanasema kuwa umudu lugha wa kijamii huchochewa na hali mbalimbali za jamii husika kama vile, kazi wazifanyazo, kiwango cha elimu na

mwonoulimwengu wao. Wanatoa mfano wa wazazi ambao huchanganya lugha wanapokuwa nyumbani na wanapokuwa nje hali ambayo huathiri namna watoto wao huzungumza pia. Kwa hali hii, viamuzi kama vile mada inayozungumziwa, hali ya wazungumzaji mtu binafsi na mahali huathiri matumizi ya lugha ya wanaulumbilugha.

Kwa upande mwengine, umudu lugha wa kibinafsi unahusu namna mtu binafsi hutumia lugha katika mazungumzo na maandishi. Jamii anamokulia mtu huathiri namna ye ye huzungumza akitumia lugha azijuazo huku akizibadilisha. Hii inaonyesha kuwa umudu lugha wa jamii huathiri umudu lugha wa kibinafsi. Hii ina maana kwamba jamii huathiri namna mtu huzungumza jambo ambalo hutokea kwa wanafunzihasa wa shule za msingi na ambalo huwaathiri kwa njia hasi au chanya.

Lugha ya Kiswahili na kingereza nchini hutumika katika utahini. Lugha kama vile Kifaransa, Kijerumani na Kichina hutumiwa katika utahini ila sio masomo ya lazima shulen na pia hayapatikani katika shule zote za msingi humu nchini. Kwa hivyo, Kiingereza na Kiswahili hutumika katika utahini katika shule za msingi nchini Kenya. Wanafunzi hujifunza lugha yao ya kwanza kisha baadaye hujifunza lugha zingine kama vile Kiingereza. Wanafunzi wengi huwa wanajua lugha ya Kiswahili maana ni lugha ya taifa nchini na ni lugha sambazi jijini Nairobi. Wanafunzi hawa hujifunza Kiingereza shulen ila wapo wengine ambao hujifunza Kiswahili shulen hasa wale wa mashinani ambapo jamii yao hutumia lugha zao za kwanza wanapokuwa nyumbani. Kulingana na nadharia ya kumudu, wanafunzi hujua kuzungumza lugha zinazofunzwa shulen kutegemea walimu wao. Hivi kwamba wanafunzi huweza kuiga walimu wao kwa kutumia lugha rasmi. Nadharia hii ya kumudu pia inadai kuwa mwanafunzi anaweza kosa kuona thamani ya kujua lugha fulani. Kwa mfano, mwanafunzi anaweza kiona Kiswahili kama lugha ya watu ambao hawajasoma na kwa hali hii hataona thamani ya kuimudu lugha hii.

Nadharia ya kumudu ilitufaa katika utafiti huu ambapo tulichanganua athari za ulumbilugha katika insha za wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue. Nadharia hii ilituongoza katika kueleza namna wanafunzi huathirika kwa kutumia lugha ya Sheng' na Kiingereza kwa Kiswahili wanapokuwa shulen. Kama tulivyosema awali, utahini wa shule ya msingi huwa wa Kiingereza na Kiswahili, hata hivyo wanafunzi hawa hutumia Sheng' kwenye mazungumzo yao ingawa sio lugha ya utahini. Matumizi haya ya Sheng' kulingana na nadharia ya kumudu hutokana na mazingira wanamokulia wanafunzi. Kwa hali hii, iwapo wanafunzi

huwa katika mazingira ambayo yana watu wanaotumia lugha mbili au zaidi, basi wao pia hawataepuka kuchanganya lugha wazijuazo katika mazungumzo yao jambo ambalo huathiri uandishi wao pia wa insha za Kiswahili. Nadharia hii ilitufaa katika kuchambua athari hasi na chanya za matumizi ya Sheng' na Kiingereza kwa Kiswahili katika insha za wanagenzi wa shule za msingi za CGHU na wale wa Moi Avenue. Tuliongozwa na mihimili ya nadharia ya kumudu ifuatayo:

- i. Mazingira huathiri tabia za watu. Hivi kwamba watu huzungumza au kuandika kutegemea na hali za mazingira wanamokulia.
- ii. Wanaulumbilugha huamua lugha ipi itumike wapi na itumike vipi. Hii ni kwa sababu wao huwa na umilisi wa lugha mbalimbali na hivyo basi huwa huru kuteua na kutumia lugha fulani kutegemea mazingira. Uhuru wa kuteua na kutumia lugha tumizi haufai kwa wanafunzi kwa kuwa Kiswahili na Kiingereza ndizo lugha za utahini.
- iii. Wanaulumbilugha hutumia lugha fulani kutegemea umuhimu wake na uwezekano wa kutumia lugha hiyo katika muktadha husika. Hii ina maana kwamba, wanafunzi hutumia lugha kwa kuzichanganya kwa kuwa pengine hamna sera ya lugha katika shule husika.
- iv. Umudu lugha wa kijamii huathiri umudu lugha wa kibinagsi. Hii ndio sababu wanafunzi hutumia lugha ambazo wamezizoea wanapokuwa manyumbani. Vile vile, inawezekana kuwa wao hutumia lugha kwa kuiga walimu wao.

### **1.7.2 Nadharia Ya Uchanganuzi Makosa**

Utafiti huu ulinuia kuelezea athari ambazo hujitokeza katika insha za wanagenzi wa shule teule za msingi. Tulisema awali kuwa utafiti huu ulikitwa katika taaluma ya isimujamii, ingawa hivyo, nadharia ya kiisimu ilitufaa kwa kuwa tunazingatia athari za ulumbilugha katika uandishi wa insha kwa kuzingatia vipengele vya mofolojia na sintaksia. Athari hizi hutokana na makosa yanayojitokeza katika insha za wanagenzi wa shule teule za msingi. Nadharia hii iliasisiwa na Corder (1960). Nadharia hii ilizuka ili kutosheleza upungufu wa nadharia ya uchanganuzi linganuzi ambayo hutumiwa ili kubainisha lugha ya kwanza na ya pili kwa wanafunzi ili kukadiria makosa yanayojitokeza katika mawasiliano.

Nadharia ya uchanganuzi makosa huangazia aina mbalimbali za makosa ambayo hujitokeza katika mawasiliano na vile vile huelezea visababishi vyta makosa hayo (Corder, 1981). Kwa mujibu wa Corder mtafiti anapaswa kufuata hatua mahsusini anapochanganua makosa katika mawasiliano. Hatua hizo ni: kukusanya sampuli ya kazi ya wanaojifunza lugha ya pili, kutambua makosa katika mawasiliano, kuelezea makosa hasa ya kisarufi, kuelezea chanzo cha makosa husika na hatimaye kutathmini makosa kwa nia ya kutafuta suluhu lake. Hii ina maana kuwa, kulingana na utafiti wetu, ni muhimu kutambua na kubainisha makosa yanayojitokeza katika insha za wanafunzi wa shule teule za msingi ambayo hutokana na athari za ulumbilugha katika jamii. Hili lilituwezesha kutoa suluhisho ambalo litaweza kusaidia katika kupambana na makosa katika uandishi wa insha za wanafunzi wa shule za msingi.

Nadharia ya uchanganuzi makosa pia iliendelezwa na Larsen (1992) ambaye anasema kuwa mtafiti anapaswa kuchunguza jumla ya makosa ya wanagenzi wanapojifunza lugha ya pili. Anaendelea kusema kuwa dosari hizi ni za kijumla na huwa katika vitengo kama vile: ujumlishaji wa kiholela, kutumia sheria ambazo hazitoshelezi mahitaji ya kimawasiliano, kutozingatia kaida za lugha husika na kubuni mambo yasiyo ya kweli. Kwa hali hii basi, nadharia hii ni muhimu kwa maana tuliangazia athari za ulumbilugha kama zinavyojitokeza katika uandishi wa insha wa shule teule za msingi. Tulijikita kwa maoni ya Corder (1981) na yale ya Larsen (1992) katika kuchanganua athari za ulumbilugha katika uandishi wa insha za wanagenzi wa shule ya CGHU na ile ya Moi Avenue. Tulijikita katika hatua za uchanganuzi makosa kama zilivyoelezwa na wasomi hawa ili kubainisha makosa yanayojitokeza katika uandishi wa insha na hatimaye kutoa suluhisho lake.

## **1.8 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada**

Kipengele hiki kiliangazia mada zinazohusiana na ulumbilugha kama zilivyoshughulikiwa na waandishi mbalimbali. Maoni ya waandishi hawa mbalimbali yalituwekea msingi kwa utafiti wa sasa. Tulishughulikia waandishi kutegemea mwaka wao wa uandishi kuanzia ule wa kale hadi wa hivi punde.

Ogechi na Jwan (2004) waliangazia matumizi ya lugha rasmi katika shughuli za masomo ya watoto wa mitaani walio katika Mashirika ya Kurekebisha Tabia. Watafiti hawa waligundua kuwa watoto hawa wa mitaani huzungumza kwa kutumia Sheng' na Kiswahili na vile vile

hutumia Kiingereza hapa na pale. Katika shule hizi za kurekebisha tabia, waligundua kuwa walimu hufunza kwa kuchanganya Kiswahili na Kiingereza. Hali hii ya kuchanganya lugha hizi mbili katika ufundishaji wa wanafunzi hawa ilidhihirisha kuwa ilikuwa mwafaka katika ufunzaji wao kwani wanafunzi walielewa kilichofunzwa zaidi. Utafiti wao ulijikita kwa elimu ya watoto wa kurandaranda mitaani ilhali sisi tulijikita kwa watoto wa shule ya msingi wanaotoka manyumbani mwao. Ingawa hivyo utafiti huu ulituwekea msingi katika kuelezea athari hasi na chanya za ulumbilugha kwa kujikita kwa Sheng' na Kiingereza katika somo la Kiswahili kwa wanagenzi wa shule ya CGHU na Moi Avenue.

Wanjugu (2010) alitafiti kuhusu sababu na athari za ubadilishaji-msimbo shulenii katika shule ya upili ya Akiba. Alijikita katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Aliongozwa na nadharia ya ukubalifu wa mawasiliano ya Howard Giles. Aligundua kuwa sababu za kiutambuzi za ubadilishaji-msimbo zinahusiana na zile za kijamii na kibinagsi. Pia alithibitisha kuwa zipo athari zitokanazo na ubadilishaji-msimbo. Wanjugu aliangazia athari hasi tu za ubadilishaji msimbo katika utafiti wake ila utafiti wa sasa uliangazia athari hasi na chanya za ulumbilugha. Pia, mtafiti huyu alijikita kwenye shule ya upili ilhali sisi utafiti wetu ulikuwa wa shule ya msingi. Ingawa hivyo, utafiti wa Wanjugu ilitufaa sio haba kwa kuwa tunaangazia athari za ulumbilugha kwa Kiswahili. Utafiti wake wa athari za ubadilishaji msimbo ni muhimu kwetu kwa kuwa hali hii husababishwa na wingilugha. Pia wingilugha ndio huwafanya wanafunzi kuchanganya ndimi ingawa wanajua kuwa ni kinyume na kanuni za shule.

Gonzalez (2010) alitafiti juu ya uwililugha katika elimu ya wanafunzi kwenye nchi ya Ufilipino. Alitaka kubaini athari za lugha zitumiwazo darasani na kufafanua mikakati inayopaswa kutiliwa maanani ili kupunguza athari za uwili lugha katika elimu ya mwanafunzi. Aligundua kuwa lugha ya Kiingereza ilipendeleta katika shule ambazo zilihudhuriwa na wanafunzi wa tabaka la juu huku wakikiona Kifilipino kama lugha isiyokuwa na manufaa mengi katika maisha yao ya baadaye. Kwa upande mwingine, Kifilipino kilipendeleta na wanafunzi wengine huku wakichanganya Kiingereza katika mazungumzo yao. Aliona hali hii ya kuweka sera ya lugha iliyotaka lugha zote mbili kutumiwa katika elimu kama iliyokwamizwa na ukosefu wa kutokuwepo kwa mikakati tosha ya utekelezaji wa sera ya lugha nchini humo. Alipendekeza kuwa lugha ya Kifilipino na Kiingereza zichukuliwe kama lugha sawa na wala sio kuiona lugha moja kuwa duni na nyingine kuwa na hadhi. Kwa njia hii, basi, athari hasi za uwililugha katika

elimu zingepungua. Utafiti wake ulionyesha kuwa lugha ya kwanza ni muhimu katika ufundishaji wa wanafunzi na wala hazingatii athari za lugha hiyo katika elimu. Utafiti wa Gonzalez ni muhimu kwa utafiti wa sasa kwa kuwa sisi pia tulishughulikia athari za ulumbilugha katika uandishi wa insha za kiswahili. Ingawa hivyo, utafiti wake si sawa na wetu kwani alijikita kwa lugha ya Kiingereza na Kifilipino ilhali sisi tulijikita kwa athari za lugha ya Sheng'na kiingereza kwa Kiswahili.

Cortez na wengine (2010) walishughulikia ufaafu wa uwililugha katika mchakato wa ufundishaji na usomaji. Waligundua kuwa wanafunzi ambao hufunzwa kwa lugha mbili-Kifilipino na Kiingereza walifanya vyema katika mitihani yao ikilinganishwa na wenzao waliofunzwa kwa lugha ya Kiingereza tu. Wanasema kuwa sababu kuu ya wanafunzi wanaofunzwa kwa kutumia lugha mbili kupita mtihani ni kuwa waliweza kufunzwa na lugha yao ya kwanza. Ufunzaji wa wanafunzi kwa lugha yao ya kwanza ni muhimu kwa kuwa wanafunzi huelewa dhana husika zaidi. Utafiti wake ni muhimu kwa utafiti huu kwani uliuwekea msingi katika kuangazia athari za ulumbilugha katika uandishi wa inshaya wanafunzi wa shule ya CGHU na ile ya Moi Avenue. Ingawa hivyo, utafiti wetu ultofautiana na huu wa wasomi hawa kwa kuwa wao walijikita katika ufaafu wa uwili lugha katika ufundishaji na usomaji ilhali sisi tulishughulikia athari za ulumbilugha katika uandishi wa insha za wanafunzi. Pia wao walizingatia Kifilipino ambacho ni lugha yao ya kwanza na Kiingereza ilhali sisi tulijikita kwa lugha ya Kiingereza, ambayo ni lugha rasmi nchini Kenya, Sheng' ambayo ni lugha vipindi na namna lugha hizi zinavyoathiri ile ya Kiswahili ambayo ni lugha ya taifa na rasmi nchini Kenya kwa mujibu wa katiba ya 2010. Utafiti huu hukuangazia lugha ya kwanza ya wanafunzi.

Igbaria (2010) alichunguza namna watu katika mji wa Israel humudu lugha ya Kiingereza. Aligundua kuwa umri na kiwango cha elimu huathiri kiasi cha kumudu Kiingereza. Alipata kuwa watu walio na kiwango cha juu cha elimu nchini humo hutumia Kiingereza katika mazungumzo yao. Alipata kuwa watu hawa walitumia lugha zao za kwanza kwa nadra sana. Utafiti huu ultufaa sana katika utafiti wetu kwa kuwa alitumia nadharia ya kumudu tulioitumia kama ilivyoelezwa na Gibson (1977). Ingawa hivyo, tafiti hizi zinatofautiana Kwa vile, Igbaria alitumia mbinu ya mahojiano ilhali sisi tulitumia mbinu kadhaa kama vile kurekodi. Pili, aliwahoji watafitiwa wake katika duka la kuuza simu ilhali watafitiwa wetu ni wanagenzi wa shule ya msingi ya CGHU na ile ya Moi Avenue. Tatu, aliwahoji watafitiwa wake kwa kutumia

lugha yao ya kwanza ilhali sisi tulijikita kwa mazungumzo kwa lugha ya Sheng' na Kiingereza na namna zinavyowaathiri wanagenzi wa shule za msingi katika uandishi wao wa somo la Kiswahili.

Kachipela (2014) aliangazia makosa ambayo hufanywa na wanagenzi wa shule za msingi katika somo la Kiswahili. Utafiti wake ulionyesha kuwa Sheng' huathiri matokeo ya Kiswahili. Utafiti wake ulituwekea msingi bora kwa utafiti wa sasa kwa kuwa utafiti wake na wetu unahu athari itokanayo na matumizi ya lugha mbili katika elimu. Ingawa hivyo, utafiti wake ulitofautiana na wetu kwa kuwa sisi tuliangazia athari hasi na chanya za uchanganyaji lugha za Kiingereza na Sheng' kwa Kiswahili katika elimu. Pia, Kachipela aliangazia makosa katika somo la Kiswahili tu ilhali utafiti wa sasa uliangazia namna Sheng' na Kiingereza huathiri insha za Kiswahili katika shule za msingi za CGHU na Moi Avenue ambazo zinapatikana katikati mwa jiji la Nairobi. Hata hivyo, utafiti wake ulitufaa sio haba.

Mkumba (2015) alichunguza athari za kiisimu za lugha ya Kiswahili katika lugha ya Kiyao. Kutokana na kuathiriana kwa lugha zinapokutana, Kiswahili pia kimekiathiri Kiyao. Mkumba alipata kuwa athari hizi hujitokeza katika mazungumzo na katika maandishi. Kuathiriana huku kwa lugha kulichochewa na matumizi ya pamoja ya lugha ya Kiswahili na Kiyao kwa muda mrefu. Utafiti wa Mkumba unatofautiana na wetu kwa vile sisi tuliangazia athari za ulumbilugha katika uandishi wa insha za wanafunzi wa shule ya msingi. Mkumba alijikita kwa kuathiriana kwa lugha mbili kutokana na mazingira ya matumizi ya lugha hizo. Hali hii ni tofauti na utafiti wa sasa ambapo tuliangazia athari za wingilugha katika maandishi ya wanagenzi wa shule za msingi. Pia alijikita kwa lugha ya Kiyao na Kiswahili huku sisi tukiangazia athari za Kiingereza na Sheng' katika Kiswahili. Ingawa hivyo, utafiti wake utatufaa kwa kuwa suala la kuathiriana kwa lugha hupatikana katika ulumbilugha pia.

Kamau (2015) aliangazia athari za lugha ya Kiswahili na lugha nyingine katika lugha ya Kikuyu. Aligundua kuwa ingawa lugha ya Kikuyu ni thabiti kiisimujamii kutokana na kuwa na wazungumzaji wengi, lugha hii huathiriwa na lugha zingine hasa katika mji wa Nairobi na maeneo ya karibu. Alipata kuwa lugha ya kikuyu iliathiri zaidi vijana wa jamii ya wakikuyu. Athari hizi zilijitokeza katika kusoma, kuongea na kuandika kwao. Kamau aligundua kuwa vijana hawa walikichukulia Kikuyu kwa njia hasi na kupendelea kutumia Kiswahili, Kiingereza na Sheng' katika mazungumzo yao. Utafiti wa Kamau unaonyesha kuwa Kikuyu kimetengwa na

kupewa nafasi ya pemberi kutokana na kuwepo kwa lugha zaidi ya moja katika mazingira wanamokulia vijana hawa. Utafiti huu wa Kamau ni muhimu kwetu kwa kuwa alishughulikia athari za ulumbilugha kama tulivyotafiti. Pia, Kamau aliangazia lugha ya Kiingereza, Sheng' na Kiswahili kama tulivyofanya. Utafiti wa sasa ni tofauti na huu wa Kamau kwa sababu aliangazia athari za lugha nyingine katika lugha ya Kikuyu ambayo ni lugha ya kwanza ya watafitiwa wake ilhali sisi tuliangazia athari ya ulumbilugha katika maandishi ya somo la Kiswahili. Aliangazia vijana ilhali sisi tulishughulikia wanafunzi wa shule ya msingi. Vile vile, Kamau alitumia mbinu za hojaji, mijadala ya makundi na pia kufanya mazoezi ya kuzungumza ilhali utafiti wetu ulitumia mbinu ya kurekodi na kuchunguza insha za wanagenzi wa shule ya CGHU na ile ya Moi Avenue. Hata hivyo, utafiti wake ulituwekea msingi kwa kuwa suala la kuwa na mtazamo hasi kuhusu lugha fulani huweza kujitokeza pia shulen. Mtazamo huu hasi huwapelekea wanafunzi kuichukulia lugha fulani kuwa duni na hivyo kuepuka kuitumia katika mawasiliano yao. Hali hii huathiri elimu yao kwa njia hasi jambo ambalo tulishughulikia katika utafiti huu.

Okoto (2015) alishughulikia athari ya Sheng' katika lugha ya Kiswahili. Aligundua kuwa watumizi wa Sheng' huacha kutumia maneno rasmi ya Kiswahili. Alitoa mfano wa *demu* ambalo lina maana ya kitambaa kitumiwacho na akina mama kufungia maziwa wanapolima. Kutokana na mfano huu, ni wazi kuwa yapo maneno ya Kiswahili ambayo huepukwa na watu kwa kuamini kuwa ni maneno ya Sheng'. Utafiti wa Okoto haufanani na wetu kwa kuwa alitafiti athari za Sheng' katika Kiswahili bila kujikita katika elimu. Utafiti wetu pia uliangazia athari hasi na chanya za ulumbilugha katika uandishi wa insha za wanafunzi wa shule ya msingi. Ingawa hivyo utafiti wa Okoto ni muhimu kwa utafiti wa sasa kwani sote tulishughulikia athari za lugha moja kwa lugha nyingine.

Mekonge (2016) alishughulikia athari za Sheng' katika shughuli za mafunzo ya Kiswahili katika shule za upili za eneo la Kisii. Alilenga kuchanganua makosa ya kimofolojia pamoja na kisemantiki yanayojitokeza kwenye insha za Kiswahili zilizoandikwa na wanagenzi wa shule za upili. Alibaini kwamba Sheng' ilikuwa imeathiri uandishi wa insha shulen. Alichunguza wanafunzi wa vidato vyote vinne na kugundua kuwa wanafunzi wa kidato cha nne walikuwa wameathirika zaidi na Sheng' na ndio sababu hawakufanya vyema katika somo la Kiswahili. Athari za uwili lugha zilijitokeza wazi katika insha za wanafunzi hawa. Utafiti wa Mekonge ulituwekea msingi katika utafiti wa sasa kwa kuwa alishughulikia Sheng' na Kiswahili kama sisi.

Pia, Mekonge alishughulikia wanafunzi kama tulivyofanya sisi. Ingawa hivyo, utafiti wake ulitofautiana na huu wa sasa kwa kuwa alishughulikia wanafunzi wa shule ya upili ilhali sisi tulishughulikia wanafunzi wa shule ya msingi. Pili, alijikita kwa lugha mbili ilhali sisi tulijikita kwa lugha tatu. Tatu, miji ya utafiti inatofautiana kwani utafiti wake ni wa mji wa Kisii ilhali sisi tuliangazia wanafunzi wa jiji la Nairobi ambapo inaaminika kuwa Sheng' imekita mizizi ikilinganishwa na miji mingine humu nchini Kenya.

Odawa na Chacha (2018) walichunguza dhima ya ujozi lugha katika kufanikisha mawasiliano kwa kujikita katika sajili ya mchezo wa kandanda. Walipata kuwa matumizi ya lugha hudhibitiwa na kaida, maadili na mazoea ya jamii husika. Ingawa hivyo, walipata kuwa lugha moja huweza kukosa kukidhi mahitaji yote ya kimawasiliano katika nyanja mbalimbali. Hii ndio sababu ujozi lugha ni muhimu kwa kuwa huziba ufa huu wa kimawasiliano bali sio umilisi finyu wa vipashio vya lugha husika. Walipata kuwa dhima ya ujozi lugha katika sajili ya mchezo wa kandanda ni: kurejelea dhana ngeni, kufafanua dhana, kupendeza na kujitambulisha kwa wasikilizaji, kuonyesha hisia zinazoibuliwa katika ujumbe na kusisitiza ujumbe. Utafiti huu wa Odawa na Chacha uliangazia dhima ya ujozi lugha katika kufanikisha mawasiliano. Walionyesha kuwa lugha moja husika yaweza kupungukiwa kwa njia moja au nyingine na ndio maana watu huchanganya ndimi ili kukidhi mahitaji yao ya kimawasiliano. Utafiti huu ni tofauti na wetu kwa namna zifuatazo: kwanza, utafiti wetu ulihusu athari za ulumbilugha katika elimu ya wanafunzi wa shule ya msingi, pili, tuliongozwa na mihimili ya nadharia kinyume na wao maana utafiti wao haukujikita kwa nadharia yoyote ile, tatu, utafiti wetu unarejelea masuala ya kiakademia huku wao wakijikita kwa sajili ya mchezo kwa kutegemea utangazaji wake katika vyombo mbalimbali vya utangazaji. Mbinu za utafiti pia zilitofautiana na zetu kwani wao waliskiliza tu matangazo ya mchezo wa kandanda ilhali sisi tulishughulikia insha za wanafunzi na mazungumzo yao. Ingawa hivyo, Utafiti huu ulitufaa kwa kuwa walijikita kwa imani kuwa matumizi ya lugha mbalimbali katika mawasiliano huwa na manufaa. Manufaa haya ndio ambayo tunayachukulia kuwa athari chanya katika elimu ya wanafunzi wa shule za msingi.

## **1.9 Mbinu za Utafiti**

Utafiti huu ulikuwa wa nyanjani. Mtafiti alizuru shule ya msingi ya CGHU na ile ya Moi Avenue zilizo katikati mwa jiji kuu la Nairobi. Tulijikita katika shule hizi mbili za msingi na za umma. Shule ya msingi ya Moi Avenue inapatikana katika barabara ya Moi huku shule ya Cutch

Gujarati Hindu Union (CGHU) ikiwa katika barabara ya Ronald Ngara. Shule ya msingi ya Moi Avenue imepakana na Jeevajee Gardens. Shule hii ni ya mseto ikiwa na wanafunzi takribani mia tano na walimu kumi na watano. Wanafunzi wa shule hii hutoka mitaa kama vile Kalifonia, Kariwa, Kirinyaga na Ngara. Shule ya msingi ya CGHU imepakana na eneo la Bus Station. Shule hii vile vile ni ya mseto ikiwa na wanafunzi mia mbili na walimu kumi. Wanafunzi wa shule hii hutoka maeneo ya Muthurwa, Landmawe, Kariokor, Gikomba na Majengo. CGHU pia ni shule ya msingi ya serikali ya Kenya.

Shule za serikali kwa kawaida huwa na idadi kubwa ya wanafunzi kwa kuwa serikali hugharamia elimu ya wanafunzi. Kwa hali hii wazazi huwa wamepunguziwa mzigo wa kulipa karo. Hii ndio sababu shule za serikali huwa na idadi kubwa ya wanafunzi kama ile ya Moi Avenue. Ingawa hivyo, shule ya CGHU ina wanafunzi wachache kwa sababu inapatikana katikati mwa jiji ambapo kuna shule zingine za msingi za umma kama vile Sri Saraswati Deepak (SSD), St Peter Clavers na Islamia. Hivyo basi, wazazi wa maeneo yaliyo karibu na shule ya CGHU huwa na shule kadhaa za kuchagua wanapotaka kuwapeleka watoto wao shule. Kwa sababu hii, shule ya msingi ya CGHU na ile ya Moi Avenue zilikuwa mwafaka katika utafiti wetu.

### **1.9.1 Walengwa**

Wanafunzi wa shule ya msingi ya CGHU na wale wa Moi Avenue walikuwa walengwa katika utafiti huu. Shule ya msingi ya CGHU ina wanafunzi 200 huku wale wa Moi Avenue ni 500 na hawa walikuwa walengwa katika utafiti huu. Shule hizi zina wanafunzi takribani 700. Tulizingatia wanafunzi wa darasa la nne hadi la nane kwa kuwa wao ndio huandika insha katika mitihani. Kwa hali hii basi, shule ya CGHU walengwa ni wanafunzi 80 huku wale wa Moi Avenue ni wanafunzi 200. Tulitumia idadi ya kimaksudi iliyotuwezesha kutimiza malengo ya utafiti wetu kwa kuwa utafiti huu ni wa uchambuzi ubora.

### **1.9.2 Sampuli Kielelezo**

Utafiti wetu ni wa uchambuzi ubora. Hii ndio sababu tulijikita kwa maoni ya Mugenda na Mugenda (2003) wanaosema kuwa iwapo idadi ya wanaotafitiwa ni kubwa, basi mtafiti atumie idadi itakayomwezesha kutimiza malengo ya utafiti wake. Tulijikita kwa wanafunzi wa madarasa ya juu ambaو huandika insha na ambaو ndio inakisiwa kuwa waliathiriwa zaidi na ulumbilugha kwa kuwa wanapenda kutumia lugha ya Kiingereza, Kiswahili na Sheng' katika mazungumzo yao na hivyo kuathirika katika uandishi wao wa insha.

### **1.9.3 Ala za Ukusanyaji Data**

Utafiti huu ni wa nyanjani. Data ya kimsingi tuliyoitumia ni ya insha ambazo ziliandikwa na wanafunzi wa shule teule za msingi jijini Nairobi. Vile vile tulipata data ya pili kutoka kwa maktaba ambapo tulidurusu makala ya wasomi mbali mbali ili kubaini yaliyohusiana na mada yetu utafiti pamoja na maelezo kuhusu nadharia tulizozitumia

### **1.9.4 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data**

Data yetu ni ya kiustahilifu na hivyo basi hatulizingatia idadi ya watafitiwa. Baada ya kukusanya data kwa kuangazia insha za wanafunzi, tuliichanganua data hiyo kwa njia ya kinadhari tukiongozwa na mihimili ya nadharia ya kumudu iliyoasisiwa na Gibson (1977) na ile ya uchanganuzi makosa iliyoasisiwa na Corder (1960) kwa njia iliyotimiza malengo ya utafiti wetu. Data tuliyoipata,tuliichanganua na kuiwasilishwa kwa sura nne kutegemea malengo yetu ya utafiti. Kila lengo lilishughulikiwa katika sura yake binafsi kwa kujikita kwenye nadharia ya utafiti.

## **SURA YA PILI**

### **ULUMBILUGHA NA MIELEKEO KUHUSU SHENG', KIINGEREZA NA KISWAHILI**

#### **2.0 Utangulizi**

Katika sura ya kwanza tulionyesha kuwa nia kuu ya utafiti huu ni kuchunguza athari za lugha ya Sheng' na Kiingereza kwa Kiswahili kama inavyojitokeza katika uandishi wa insha za wanafunzi wa shule za msingi. Utafiti huu ulichunguza athari za ulumbilugha kwa wanafunzi wa shule za msingi ya CGHU na Moi Avenue. Shule hizi zinapatikana katika jiji la Nairobi ambapo wakaazi ni watu kutoka jamiiilugha mbalimbali na hili ni jambo ambalo huwalazimu watu kuwasiliana kwa kutumia lugha inayoleweka na wazungumzaji wote. Ni kwa misingi hii ambapo Githiora (2002) anasema kuwa Kiswahili ndio lugha ambayo hutumiwa zaidi jijini Nairobi. Msomi huyu anaendelea kusema kuwa Nairobi ni mji ulio na watu wa matabaka mbalimbali ya kiuchumi. Anasema kuwa pengo baina ya matajiri na maskini ni kubwa mno na watu hawa huishi katika mitaa mbalimbali jijini humo. Utabaka huu unadhihirika pia katika matumizi ya lugha ambapo watu wa tabaka la juu hupendelea kutumia Kiingereza katika mawasiliano na vile vile hutumiwa katika utahini wa mitihani katika shule na vyuo nchini Kenya (Githiora, 2002). Kiswahili ni

somo la lazima katika shule za msingi na za upili. Watafitiwa wetu ambao ni wanafunzi wa shule za msingi pia wanatakiwa kuwa na ujuzi wa lugha hii ya taifa. Kwa jumla wanafunzi nchini Kenya huwa na ujuzi wa lugha takribani tatu: Kiswahili, Kiingereza na lugha ya mama. Ulumbilugha huwa na athari hasi na chanya kwa wanafunzi wa shule ya msingi. Hii ndio maana tulijadili ulumbilugha kwa ujumla na mielekeo ya wanafunzi kuhusu Kiingereza, Sheng' na vile vile Kiswahili katika vijisehemu vifuatavyo.

## **2.1 Ulumbilugha**

Katika kisehemu hiki, tuliangazia ulumbilugha kama unavyojitokeza katika jamii. Ulumbilugha katika jamii husababishwa na mambo mengi kukiwemo elimu na ndoa mseto n.k. nchini Kenya, wanafunzi hutahiniwa kwa kutumia Kiswahili na lugha za kigeni kama vile Kiingereza ambacho pia ni lugha rasmi, Kifaransa na Kijerumani. Hii ina maana kuwa wanafunzi wanalazimika kujua lugha mbili au zaidi na hili ni jambo ambalo huzua ulumbilugha. Ni muhimu kutaja hapa pia kuwa wanafunzi huwa wanatoka jamiilugha mbalimbali. Hivyo basi, wanafunzi hawa tayari huwa na lugha yao ya kwanza na ambayo wao huitumia nyumbani na mitaani. Hali hii hukoleza zaidi ulumbilugha kwa kuwa wanafunzi hutumia lugha mahsus iwanapokuwa nyumbani na mitaani na kisha kutakiwa kutumia Kiingereza na Kiswahili wanapokuwa shulen. Hali hii ya kutumia lugha mbalimbali kutegemea mazingira huwa na athari hasi na chanya katika kuandika insha za Kiswahili kwa wanafunzi kama tulivyoonyesha katika utafiti huu.

Katika utafiti huu, tulitumia dhana uwililugha na ulumbilugha/wingilugha kama visawe. Ulumbilugha ni umilisi wa lugha zaidi ya moja katika mawasiliano, pia hujulikana kama wingi lugha. Iribemwangi na Mukhwana (2011) wanauona ulumbilugha kama uwezo wa mtu au jamii kutumia lugha mbili katika mawasiliano. Kutokana na maoni haya, tunaweza kusema kuwa watu ambao wanauwezo wa kutumia lugha zaidi ya mbili katika mawasiliano huchukuliwa kuwa wanaulumbilugha. Kwa upande mwingine Mackey (1998) anauona ulumbilugha kama matumizi ya lugha mbili au zaidi kwa kuzibadilisha katika mawasiliano. Hii ina maana kuwa mwanaulumbilugha huchanganya ndimi katika mawasiliano kwa kutumia lugha mbili au zaidi. Ni kwa misingi hii ambapo tunasema kuwa wanaulumbilugha ambao huchanganya ndimi katika mawasiliano hujipata pia wakitumia lugha zaidi ya moja katika uandishi. Hili ndilo jambo linalowaathiri wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue katika uandishi wa insha. Hii ndio sababu tuliangazia athari za ulumbilugha kwa wanafunzi wa shule hizi za msingi.

Bloomfield (1993) anasema kuwa ulumbilugha hauwezi kuepukika katika taifa ambapo wenyiji ni watu wa makabila tofauti tofauti. Hali hii hutokea kwa kuwa watu wa makabila mbalimbali hulazimika kutumia lugha inayolewaka na wote katika mawasiliano. Hapa ndipo suala la lugha sambazi hujitokeza kwa nia ya kukidhi mahitaji ya kimawasiliano katika jamii na ambayo huwaunganisha watu wa makabila mbalimbali. Hali hii huwalazimu watu kujua lugha ya pili ambayo itawawezesha kuwasiliana na wenzao wa makabila mengine. Bloomfield anaelezea sababu saba zinazochangia kuwepo kwa ulumbilugha katika jamii na ambazo ni: ndoa mseto, elimu, uchumi na biashara, udiplomasia, kuwepo kwa sera za lugha za wakoloni, kuwepo kwa dini mbalimbali na mwingiliano wa watu katika jamii. Sababu hizi zilidhihirika katika elimu ya wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue zilizoko jijini Nairobi.

Katika utafiti huu, lililojitokeza ni kuwa elimu, ndoa mseto, dini tofautitofauti, uchumi na biashara na mwingiliano wa watu katika jamii husababisha ulumbilugha kwa wanafunzi wa shule za msingi. Ikumbukwe kuwa Wakenya kwa jumla ni wanaulumbi-lugha, ambapo wao hutumia lugha ya mama na aidha Kiswahili au Kiingereza wakiwanyumbani na hatimaye hujifunza Kiingereza na lugha zingine za kigeni shuleni. Jambo la kimsingi ni kuwa Wakenya ni wanaulumbilugha. Athari za ulumbilugha zilidhihirika wazi kwa wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na ile ya Moi Avenue katika uandishi wao wa insha za Kiswahili. Tunaweza kusema kuwa wanafunzi wa shule hizi za msingi wanatumia lugha kutegemea mazingira watokako. Katika utafiti wetu, tulibaini kuwa wanafunzi wa Shule za msingi za CGHU na Moi Avenue hutoka mitaa duni ya Majengo, Kariokor, Landmawe na Gikomba. Wakaaji wa maeneo haya wanajihuisha na biashara mbalimbali na uchuuzi ili kupata riziki. Inawezekana pia kuwa watoto wa wachuuzi hawa huhusika katika uchuuzi watokapo shuleni, wikendi na siku za likizo. Ni kwa misingi hii ambapo tunasema kuwa watoto hawa hutumia lugha kutegemea mazingira. Wanafunzi hupaswa kutumia Kiingereza na Kiswahili wanapokuwa shuleni kwa kuwa ndizo lugha za utahini. Sera ya lugha ya shule ya Moi Avenue hairuhusu uchanganyaji ndimi katika mawasiliano. Kwa hivyo basi wanafunzi hawa wanapaswa kutumia Kiswahili au Kiingereza katika mazingira ya shule na wanapojibu maswali ya mitihani yao. Wanafunzi hawa wanapokwenda nyumbani huwa huru kutumia lugha wazijuazo katika mawasiliano. Maoni yetu ni kuwa wanafunzi hawa wanashindwa kuzingatia sera za lugha za shule kutokana na kujipata katika mazingira mbalimbali na ambayo huwahitaji kutumia lugha tofauti tofauti na kwa namna tofauti. Hii ni hali ambayo tuliishuhudia katika uandishi wa insha ambapo wanafunzi huchopeka

maneno ya lugha ya Kiingereza na Sheng' hapa na pale. Hii ni licha ya kuwa wanajua kuwa ni kinyume na matarajio ya utahini ambapo wanapaswa kutumia Kiswahili pekee katika uandishi wa insha za Kiswahili.

Wasomi kama vile Habwe na wenzake (2010), Wamitila (2003) na Buliba na wenzake (2006) wanaonyesha kuwa wanaulumbilugha huchanganya ndimi katika mawasiliano yao. Hii inaonyesha kuwa uchanganyaji ndimi hauwezi kuepukika kwa wanaulumbilugha. Tulibaini kuwa matumizi ya uchanganyaji ndimi katika mawasiliano yalijitokeza katika uandishi wa insha za Kiswahili za wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue. Ni kwa misngi hii ambapo tunasema kuwa ulumbilugha huwaathiri wanafunzi wa shule za msingi katika uandishi wao wa insha.

## **2.2 Athari za Ulumbilugha**

Ulumbilugha hujidhihirisha kuitia uchanganyaji ndimi katika uandishi wa insha za wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue. Hii ina maana kuwa ulumbilugha ni umilisi unaowawezesha watu kukamilisha mawasiliano yao kwa kutumia lugha tofauti katika mazungumzo au maandishi yale yale. Watu huchanganya ndimi kwa sababu mbalimbali kama inavyojitokeza katika Makala ya Ho (2007). Sababu hizi ni kama vile, kufidia msamiati, kwa nia ya kujieleza ipasavyo, kujinasibisha na kundi fulani la watu na vile vile kutokana na mazoea. Kwa upande wa wanafunzi wa shule za msingi, tunaweza kusema wao huchanganya ndimi kwa sababu ya mazoea na kufidia msamiati. Tunasema hivi kwa sababu, kama tulivyoonyesha awali, wanafunzi wa shule ya msingi ya CGHU na ile ya Moi Avenue hutoka mitaa duni ambapo Sheng' imekithiri (Iribemwangi, 2020). Kutokana na mazoea ya kutumia Sheng' katika mawasiliano wanapokuwa mitaani, inakuwa vigumu kuepuka kuchanganya ndimi wanapoandika insha. Vile vile, tunaweza kusema kuwa wanafunzi wa shule hizi za msingi huwa walibobeza zaidi katika Sheng' na hivyo basi huwa hawajui dhana zinazotumiwa kurejelea mambo fulani na ndio sababu wao huchopeka maneno ya Sheng' wanapoandika insha. Vile vile wanafunzi wa shule za msingi huchopeka maneno ya Kiingereza wanapoandika insha kwa kuwa wao hufunzwa masomo mengi kwa lugha hii ikilinganishwa na Kiswahili. Kwa mfano, "**Ikifika Sunday, tunaenda kuchunga mbuzi zetu.**" Katika sentensi hii mtafitiwa alitumia Kiswahili ila akachopeka neno *Sunday* ambalo ni la Kiingereza. Maoni yetu ni kuwa mwanafunzi huyu wa shule ya msingi ya CGHU ameathiriwa kutokana na mazoea ya kutumia Kiingereza zaidi

ikilinganishwa na Kiswahili wanapofunzwa shulen. Uchanganyaji ndimi katika uandishi wa insha huwafanya wanafunzi kuadhibiwa kwa kutolewa alama. Hii inakuwa athari hasi kwa kuwa wao hupata alama finyu katika mitihani ikilinganishwa na wenzao ambao hutumia Kiswahili pekee yake katika uandishi wa insha.

Katika utafiti huu, tunatumia dhana ya ubadilishaji msimbo kwa maana ya matumizi ya lugha zaidi ya moja katika uandishi wa insha, kama vile, "**sherehe ilikuwa ifanyike December**." Katika mfano huu, neno *December* ni la Kiingereza na limetumika pamoja na maneno ya Kiswahili katika sentensi hii. Tulitumia dhana, uchanganyi ndimi kwa maana ya kutumia mizizi ya Kiingereza na kuongezea viambishi vya Kiswahili. Kwa mfano, "**dada aliwed mpenzi wake**." Neno *aliwed*, ndilo tunalorejelea kama uchanganyaji ndimi. Neno hili lina mzizi wa Kiingereza, *wed* na viambishi awali vya Kiswahili **ali-**. Kutokana na mifano hii, tunaweza kusema kuwa uchanganyaji ndimi ni mtindo wa kutumia mzizi wa neno la lugha fulani kisha kuongezea viambishi vya lugha nyingine.

Ulumbilugha ndio chanzo cha uchanganyaji ndimi katika mawasiliano ya wanafunzi wa shule ya msingi. Kama tulivyosema awali, hali hii hudhihirika katika mazungumzo na maandishi yao. Deuchar na Quay (2000) wanadai kuwa uchanganyaji ndimi mionganoni mwa watoto husababishwa na mazingira wanamokulia. Mazingira ambapo wakaazi hutumia lugha zaidi ya moja katika mawasiliano huwafanya watoto kuwa na umilisi wa lugha hizo. Wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue hutoka mitaa duni ambapo wakaazi ni watu wa lugha mbalimbali na ambapo Sheng' hutumika zaidi (Githiora, 2002). Hili ni jambo ambalo huwafanya wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na wenzao wa Moi Avenue kuchanganya ndimi au kubadilisha msimbo wanapoandika insha. Kwa hivyo, utafiti huu ni muhimu kwa kuwa uliangazia uchanganyaji ndimi na aina zake kama inavyobainika katika vijisahemu vifuatavyo:

## 2.2.1 Kuchanganya Ndimi

Kuchanganya ndimi ni mbinu ya mawasiliano ambapo wazungumzaji hutumia lugha zaidi ya moja katika muktadha mmoja. Nkonko (1997) anasema kuwa kuchanganya ndimi ni mtindo wa kutumia lugha mbili au zaidi katika muktadha mmoja. Anaendelea kusema kuwa mtindo huu wa uchanganyaji ndimi hutokea kwa wanawingi lugha. Msomi huyu pia anasema kuwa, katika taaluma ya isimujamii, uchanganyaji ndimi huhusisha matumizi ya lugha zaidi ya mbili ambapo

anaashiria kuwa lugha huwa na hadhi mbalimbali kwa wazungumzaji. Anasema kuwa, watumizi lugha huwa na lugha msingi na nyingine ambayo hutumiwa hapa na pale. Hii inaonyesha kuwa wazungumzaji hutumia zaidi lugha msingi wanapowasiliana na kisha kuchopeka maneno ya lugha nyinginezo katika mazungumzo husika. Tulikubaliana na maoni ya msomi huyu kwa kuwa tuliyashuhudia katika mazungumzo ya wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na ile ya Moi Avenue. Tulibaini kuwa watafitiwa wetu ni wanaulumbilugha ambapo wanajua lugha zaidi ya moja. Lugha hizi ni kama vile Kikuyu, Kikisii, Kijaluo n.k ambazo ni lugha za wazazi wao, Kiswahili, Kiingereza na Sheng'. Ni muhimu kutaja hapa pia kuwa wanafunzi hawa walilelewa katika mitaa duni ambapo watu walizoea kuchanganya ndimi katika mawasiliano yao na ndiposa wao pia huchopeka maneno ya lugha zingine wanapoandika insha. Ikumbukwe kuwa mojawapo wa maagizo katika karatasi za maswali ya insha ni kuandika kwa kutumia Kiswahili pekee. Wanafunzi ambao huchanganya ndimi katika uandishi wa insha huadhibiwa kwa kupewa alama chache ikilinganishwa na wenzao ambao wanazingatia maagizo ya utahini.

Kutokana na data ya utafiti huu, uandishi wa insha za Kiswahili katika shule za msingi za CGHU na Moi Avenue ulidhihirisha matumizi ya uchanganyaji ndimi. Hii ni kutokana na mahali walipolelewa. Data yetu inaonyesha kuwa wanafunzi huchanganya Kiswahili, Kiingereza na Sheng' katika insha zao. Kwa mfano, katika insha yenye mada, 'Shule Yetu' mtarufiwa ameandika kuwa "**shule yetu ina madem wakubwa sana hata kuliko wa secondary**." Mtarufiwa ametumia lugha tatu katika sentensi hii moja. Neno *madem* ni la Sheng' kwa maana ya wasichana. Mtarufiwa pia ametumia neno la Kiingereza, *secondary* kwa maana ya shule ya upili. Ipara na Maina (2008) wanasema kuwa uchanganyaji ndimi ni hali ambapo watu hutumia lugha moja na kisha kuchopeka maneno ya lugha nyingine ya pili au ya tatu kwa muda mfupi na hatimaye hurejelea lugha msingi katika mawasiliano husika. Hii inaashiria kuwa mzungumzaji huanza kwa lugha msingi kisha kuchopeka maneno ya lugha nyingine tofauti katika sentensi husika na hili ni jambo ambalo huashiria uchanganyaji ndimi katika sentensi moja. Hali hii ndio huzua aina mbalimbali za uchanganyaji ndimi.

Uchanganyaji ndimi huwa wa aina mbalimbali kama inavyojitokeza katika maandishi mbalimbali. Muysken (2000) anasema kuwa uchanganyaji ndimi hutokea pale ambapo kipengele kimoja cha kileksika na kisarufi kutoka kwa lugha mbalimbali hutokea kwa sentensi ile ile moja. Kwa upande mwengine, awali, Richards na wenzake (1985) walielezea kuwa uchanganyaji ndimi

ni ule uchopekaji wa maneno ya lugha moja katika sentensi iliyo katika lugha nyingine. Maoni ya wasomi hawa yana mwingiliano mkubwa. Tunasema hivi kwa sababu wote wanaonyesha kuwa uchanganyaji ndimi ni matumizi ya lugha zaidi ya moja katika usemi mmoja. Wasomi hawa wanazungumzia aina moja tu ya uchanganyaji ndimi ambayo ni uchopekaji wa maneno ya lugha nyingine katika mawasiliano. Hata hivyo, mtaalamu Romaine (1989) anazungumzia aina tatu za uchanganyaji ndimi na ambazo zitatuongoza katika utafiti huu. Aina hizo tatu za uchanganyaji ndimi ni: Uchopekaji wa maneno ya lugha zingine katikati ya sentensi, uchopekaji wa maneno ya lugha zingine mwishoni mwa sentensi na uambatishaji kiungo. Tulijadili aina hizi za uchanganyaji ndimi katika vijisehemu vifuatavyo:

### **2.2.2 Uchopekaji wa Maneno ya Lugha Zingine Katikati ya Sentensi ya Kiswahili**

Uchopekaji wa maneno ya lugha zingine katikati ya sentensi hutokea pale ambapo mzungumzaji au mwandishi anaanza sentensi kwa lugha moja, kisha kuchopeka neno la lugha nyingine na hatimaye kuikamilisha kwa lugha aliyoanza nayo. Romaine (1989) anaelezea kuwa uchopekaji wa maneno ya lugha nyingine katikati ya sentensi ni uingizaji wa vipashio vya lugha nyingine katikati ya sentensi zilizo na lugha msingi. Hili linathihirisha kuwa maneno ya lugha zingine yanayochopekwa katika sentensi zenye lugha msingi huzingatia kanuni za kifonolojia za lugha msingi katika uundaji wa vishazi au kazi andishi husika. Kwa mfano, katika mawasiliano ambapo Kiswahili ni lugha msingi, wazungumzaji au waandishi wanaweza kuchopeka neno la Kiingereza katikati ya mazungumzo au matini husika. Neno hilo la Kiingereza lililochopekwa katikati ya sentensi huchukua muundo wa lugha ya Kiswahili na vile vile huzingatia upatanisho wa kisarufi kama ilivyo katika matini au mazungumzo ya Kiswahili. Kwa mfano, “**mama alikuja nyumbani April na alituletea nguo mpya**”. Katika mfano huu, Kiswahili ndio lugha msingi kisha neno *April* la Kiingereza likachopekwa katikati ya sentensi. *April* ni neno huru na wala halijaambishwa na viambishi vya Kiswahili.

Maneno ya lugha nyingine yaliyochopekwa katika matini au mazungumzo husika huweza kuchukua muundo wa maneno huru au yaliyo na viambishi vya lugha nyingine na kisha mzizi kuwa wa lugha hiyo geni. Mfano wa maneno yaliyoongezewa viambishi ni kama vile kubuy, kusit na kusettle. Maneno haya huweza kutumiwa katikati ya sentensi ifuatavyo:

- 1. a) Nilienda kwa duka kubuy (kununua)mkate.**

**b) Nilitakiwa kusit (kufanya) hiyo exam (mtihani) mwaka uliopita.**

**c) Tutaenda kusettle (kuishi) Nakuru.**

Tulionyesha kuwa wanaulumbilugha huweza kuchopeka maneno ya lugha zingine katikati ya sentensi ya Kiswahili. Hali hii hutokea kwa sababu ya kuwa na umilisi wa lugha zaidi ya moja na hivyo basi kujipata akizitumia lugha azijuazo katika mawasiliano. Kutokana na athari za wingilugha, wanaulumbilugha pia huchopeka maneno ya lugha zingine mwishoni mwa sentensi za Kiswahili kama tulivyoonyesha katika kisehemu kifuatacho.

### **2.2.3 Uchopekaji wa Maneno ya Lugha Zingine Mwishoni mwa Sentensi ya Kiswahili**

Uchanganyaji ndimi hutokea kwa njia nyingi. Tulionyesha kuwa maneno ya lugha geni huweza kuongezwa katikati ya sentensi ya Kiswahili katika kisehemu kilichopo hapo juu. Katika kisehemu hiki, tulijadili uchopekaji wa maneno mwishoni mwa sentensi ya Kiswahili. Uchopekaji wa aina hii hutokea pale ambapo msemaji au mwandishi huanza kwa lugha msingi kama vile Kiswahili na kisha kutia maneno ya lugha nyingine geni mwishoni mwa sentensi husika. Poplack (1980) anasema kuwa watu huchopeka neno moja kutoka lugha geni kutokana na hali ya kusahau neno mwafaka kwa lugha msingi. Vile vile, inawezekana kuwa msemaji au mwandishi hajui neno husika kwa lugha msingi. Hali hii huweza kuchochea uchanganyaji ndimi katika sentensi moja. Buliba na wengine (2006) wanasema kuwa wanaulumbilugha huchanganya ndimi kwa sababu ya mtindo. Kulingana nao, uchanganyaji ndimi ni mtindo wa kusisitiza kile kinachosemwa. Vile vile, wanasema kuwa watu huchanganya ndimi kwa sababu ya kutaka kupambanua dhana geni na pia kubainisha hisia fulani. Hii inadhihirisha kuwa wanaulumbilugha huchanganya ndimi kutokana na vichocheo mbalimbali. Vichocheo hivi hutofautiana kutegemea kinachozungumziwa.

Wanafunzi wa shule ya msingi pia huchanganya ndimi katika uandishi wao wa insha kwa sababu mbalimbali. Mazingira ambamo watoto wamelelewa huwafanya kutumia lugha kwa namna mahsus. Watoto ambao hutoka mitaa ambamo watu huchanganya ndimi katika mawasiliano yao huathirika kwa njia hasi au chanya. Tunasema hivi kwa sababu watoto hawa hujipata wakichanganya ndimi hata katika uandishi wa insha ilhali wanajua kuwa ni kosa. Wanafunzi wa shule za msingi huchanganya ndimi kwakuongezea maneno ya lugha geni katika lugha msingi. Hii ni kwa sababu ya mazoea na pia kutumia maneno kutoka kwalugha ambayo hutambulika

kwa urahisi kulingana nao. Kwa mujibu wa Aloo (2002) uchanganyaji ndimi hutokea wakati ambapo watu hawataki kutafsiri. Kwa hivyo basi, wanafunzi huchopeka maneno ya lugha nyingine geni bila hata juhudini ya kuliswahilisha neno husika. Hali hii pia hutokea katika uandishi wa insha ya wanafunzi wa shule ya msingi ya CGHU na Moi Avenue. Kwa mfano,

- 2. a) Ilikuwa siku ya kwenda secondary (shule ya upili).**
- b) ..... ana madoadoa black na white (nyeusi na nyeupe).**
- c) Tulienda na mama yangu wedding (arusi).**
- d) Huyo mtoto alinipea bukla (kitabu).**

Watafitiwa walichopeka maneno ya Kiingereza na Sheng' mwishoni mwa sentensi. Mifano 2a), b), c) na d), inaonyesha athari za Kiingereza na Sheng' kwa Kiswahili. Wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue wanatumia maneno ya Kiingereza na Sheng' mwishoni mwa sentensi katika uandishi wa insha za Kiswahili. Maneno, *secondary*, *black*, *white* na *wedding* ni ya Kiingereza. Neno *bukla* hutumiwa katika Sheng' kwa maana ya kitabu. Haya ni maneno ambayo yana misamiati yake kwa Kiswahili na ambayo imezoleka. Haiwezekani kuwa watafitiwa wetu hawajui neno ‘kitabu’ kiasi cha kuwafanya kutumia Sheng’. Hii ndio sababu tunasema kuwa wanafunzi wanajua maneno mwafaka ya Kiswahili ila wanachanganya ndimi kwa sababu ya kuathiriwa na ulumbilugha. Athari hii ni hasi kwa sababu inawafanya wanafunzi kutumia maneno ya Sheng’ na Kiingereza katika insha za Kiswahili.

Katika uandishi wa insha wanafunzi wa shule za msingi huchopeka maneno katika sehemu mbalimbali kukiwemo katikati na mwishoni mwa sentensi kama tulivoonyesha katika mifano iliyopo hapo juu. Uchanganyaji ndimi hutokea kwa sababu mbalimbali kama vile, mazoea ya watu kuchanganya ndimi wanapozungumza na hivyo basi kujipata katika hali husika wakati wa kuandika. Mazoea ya kuchanganya ndimi wakati wa mzungumzo huwaathiri wanafunzi pia katika uandishi wao. Hii ni athari hasi kwa kuwa wanafunzi hutakiwa kutumia Kiswahili peke yake katika uandishi wa insha na wala hawaruhusiwi kuchanganya ndimi. Ni kwa misingi hii ambapo tunasema kuwa wanafunzi huchanganya ndimi kutohana na athari za ulumbilugha.

#### **2.2.4 Uambatishaji Kiungo**

Uambatishaji kiungo ni mtindo wa uchopeka ji wa maneno au virai vya lugha nyingine na ambao hutokea mwanzoni mwa sentensi. Hali hii hutokea pale ambapo mwandishi au msemaji anakosa

msamiati mwafaka wa lugha msingi ambayo inatawala mawasiliano husika. Kwa hivyo basi, tunaweza kusema kuwa wanaulumbilugha wakati mwingine hukosa msamiati mwafaka wa neno fulani la lugha msingi na ndiposa huanza sentensi kwa kutumia neno la lugha nyingine tofauti. Kwa mfano:

**3. a) Sanitizer (kieuzi) inapaswa kuwekwa mkobani mwako.**

**b) Magistrate (hakimu) ameondoka sasa hivi.**

**c) Laptop (kipakatalishi) yangu imeharibika.**

### **2.3 Mielekeo Kuhusu Sheng', Kiingereza na Kiswahili**

Tulionyesha kuwa wanafunzi ambao ni wanaulumbilugha huchanganya ndimi wanapozungumza na hata kuandika. Hata hivyo, wanaulumbilugha huchukulia lugha wazijuazo kwa namna tofauti tofauti. Ikumbukwe kuwa wanafunzi wa shule za msingi hujifunza lugha nyumbani na vile vile shulenii. Wanafunzi hawa huwa na mielekeo mbalimbali kuhusu Sheng' ambayo huzungumzwa mitaani huku wakitakiwa kutumia Kiingereza na Kiswahili peke yake shulenii. Kwa hali hii basi, wanafunzi huwa na mielekeo tofauti tofauti kuhusu Sheng', Kiingereza na Kiswahili kama tulivyoonyesha katika sehemu zifuatazo:

#### **2.3.1 Mielekeo ya Wanafunzi Kuhusu Sheng'**

Sheng' ni lugha ambayo misamiati yake imeundwa kutoka kwa lugha zingine. Karanja (1993) anasema kuwa Sheng' huundwa kutokana na maneno ya Kiswahili na Kiingereza. Kwa upande mwingine, Githiora (2002) anadai kuwa Sheng' huundwa kwa kutumia maneno ya Kiswahili na lugha za asili za Wakenya. Kutokana na maoni ya wasomi hawa, tunaweza kusema kuwa watumizi wa Sheng' huunda misamiati kutoka kwa lugha zingine zinazowazunguka. Hii pia ni athari nyingine ya ulumbilugha. Tunasema hivi kwa sababu watumizi wa Sheng' hubuni misamiati mipyka kutoka kwa lugha zingine ambazo wanazijua wao. Kwa hivyo basi, wanaulumbilugha ambao hupendelea kutumia Sheng' katika mawasiliano yao huunda misamiati mipyka kutoka kwa lugha zingine na ambazo wanazijua. Githiora (2002) na Githinji (2008) wanasema kuwa chimbuko la Sheng' ni mitaa ya Mashariki jijini Nairobi. Wakazi wa mitaa hii ni watu wa mapato wastani na vile vile wapo makabwela. Githiora anataja mitaa kama vile

Bahati na Jericho na ambayo inaaminika kuwa Sheng' ilianzia maeneo haya. Hii inaonyesha kuwa Sheng' inahusishwa na wakazi wa mitaa duni mjini Nairobi.

Wasomi mbalimbali walielezea chimbuko la Sheng' nchini Kenya. Karanja (1993) na Mazrui (1995) wanasema kuwa Sheng' iliibuka mwanzoni mwa miaka ya 1930. Karanja anasema kuwa yeye na wenzake walitumia Sheng' kuwasiliana kwa nia ya kuficha siri zao. Hii ina maana kuwa Sheng' ni lugha inayotumiwa na wanakundi-ndani kuficha siri zao. huu ni mwelekeo hasi kuhusu Sheng' hasa ikizingatiwa kuwa inahusishwa zaidi na vijana nchini Kenya. Hata hivyo, wasomi wengine, mathalan, Osinde (1986), Githiora (2002), Abdulaziz na Osinde (1997), wanadai kuwa Sheng' iliibuka baina ya 1960-1980. Sheng' ni lugha ya utambulisho wa vijana mjini Nairobi (Githiora, 2002). Hii inadhihirisha kuwa Sheng' ni lugha inayotumiwa na vijana zaidi ikilinganishwa na makundi mengine ya watu. Maoni ya Githiora yanaonyesha kuwa vijana ndio huhusishwa zaidi na matumizi ya Sheng'. Inadaiwa kuwa Sheng' hutumiwa na vijana ambao hutaka kuficha siri zao dhidi ya makundi mengine ya kijamii. Hali hii inaashiria kuwa Sheng' inahusishwa na watu ambao wanaendeleza shughuli zao bila kutaka kujulikana na watu wa makundi mengine ya kijamii kwa nia ya kuficha siri zao.

Kwa upande mwingine, Iribemwangi (2020) anasema kuwa Sheng' imesambaa kutoka mitaa iliyoko Mashariki mwa jiji la Nairobi hadi mitaa mingine ya jiji hili na vile vile mashinani. Hii inaashiria kuwa Sheng' inatumika kwingi nchini Kenya. Kwa maoni yetu, kusambaa huku kwa Sheng' nchini Kenya ndio kuliwafanya wanafunzi pia kujipata wakichanganya ndimi katika uandishi wao wa insha. Wanafunzi wanajipata wakitumia maneno ya Sheng' katika insha licha ya kuwa wanajua vizuri kuwa ni makosa. Kwa hivyo, tunaweza kusema kuwa wanafunzi wanachanganya ndimi katika uandishi wao wa insha kutokana na mazoea ya wanakotoka. Ni muhimu kutaja hapa kuwa wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue wanatoka mitaa kama vile Majengo, Muthurwa na Landmawe. Hii ni mitaa ambayo inahusishwa na watu ambao hutumia Sheng' na lugha zingine katika mawasiliano yao. Kwa hali hii basi, wanafunzi hujipata wakitumia lugha mbalimbali katika uandishi wao wa insha. Hii ni athari hasi kwa wanafunzi hasa ikizingatiwa kuwa watahini huwaadhibu kwa kuwatoa alama nusu kwa makosa ya aina hii. Hali hii ndio ilituchochea kutaka kujua sababu ambazo huwafanya wanafunzi kuchanganya ndimi katika uandishi wao wa insha ilhali wanajua kuwa ni kosa. Hii ndio sababu tunashughulikia mielekeo ya wanafunzi kuhusu lugha ya Sheng'.

Wanafunzi wa shule ya msingi ya CGHU na Moi Avenue ni wakazi wa mitaa iliyo jijini Nairobi na ambayo inaaminika kuwa ni kitovu cha matumizi ya Sheng'. Tulionyesha kuwa Sheng' ni kitambulisho cha vijana na ambayo hutumika kuficha siri yao. Tulibaini kuwa wanafunzi huchopeka misamiati ya Sheng' katika uandishi wao insha kwa sababu kama vile, mazoea na kufidia msamiati. Ikumbukwe kuwa Misamiati ya Sheng' huwa sahili na hili ndilo jambo ambalo huwafanya wanafunzi kuitumia lugha hii. Hali hii hurahisisha mawasiliano baina ya wazungumzaji na hii ni athari chanya. Ingawa hivyo, wanafunzi huathirika kwa njia hasi wanapotumia Sheng' katika uandishi wao wa insha.

Kutokana na data ya utafiti huu, tulibaini kuwa wanafunzi wa shule ya msingi ya CGHU na Moi Avenue huchopeka maneno ya Sheng' katika uandishi wao wa insha bila hiari yao. Data tulioikusanya kupitia kwa kuwahoji wanafunzi wa shule hizi inaonyesha kuwa wao huchanganya ndimi katika uandishi wao wa insha kwa sababu ya mazoea ya kutumia Kiingereza, Kiswahili na Sheng' wanapozungumza. Wanafunzi hawa walidhihirisha kuwa wao huchopeka maneno ya Sheng' katika uandishi wa insha kwa sababu hivyo ndivyo wao huzungumza na marafiki zao wanapokuwa nyumbani. Hii ina maana kuwa wanafunzi hawa hujipata wakitumia lugha kwa mtindo mmoja katika mazingira tofauti tofauti. Mazingira haya ni nyumbani na shuleni. Kwa hali hii basi, tunaweza kusema kuwa wanafunzi hawa wanashindwa kutumia lugha kutegemea mahali walipo kwa kusahau kuwa mazingira ni mojawapo wa viamuzi vyta matumizi ya lugha.

### **2.3.2 Mielekeo ya Wanafunzi Kuhusu Kiingereza**

Jukumu la lugha yoyote ile ni kukidhi mahitaji ya kimawasiliano katika taifa fulani. Baadhi ya lugha zimevuka mipaka ya kijamii na kutumiwa katika mawasiliano ya kitaifa na kimataifa. Kiingereza ni lugha ambayo imevuka mipaka ya kijamii na kuwa ya kimataifa. Johnson (2013) anasema kuwa Kiingereza ndio lugha ambayo imepewa hadhi ya kuwa lugha rasmi katika mataifa 67 kote ulimwenguni. Anaendelea kusema kuwa Kiingereza ndio lugha ambayo hutumika katika biashara nyingi za kimataifa na pia hutumiwa kama lugha rasmi katika asasi mbalimbali kama vile Muungano wa Kimataifa. Kiingereza kimekuwa lugha pekee rasmi nchini Kenya kwa muda mrefu hadi mwaka wa 2010 ambapo katiba ilikifanya Kiswahili kuwa lugha ya kwanza rasmi nchini. Kwa mujibu wa katiba ya 2010 ya Kenya ni kuwa nchi hii ina lugha mbili rasmi. Kiingereza ni lugha rasmi ya pili katika taifa la Kenya ambalo ni mionganoni mwa mataifa

yaliyo katika Muungano wa Kimataifa. Kwa hali hii basi, tunaweza kusema kuwa Kiingereza ni lugha ya mawasiliano mapana ulimwenguni.

Kiingereza ndio lugha ambayo hutumika katika ufunzaji na utahini wa masomo mengi ikilinganishwa na Kiswahili na lugha zingine za kigeni. Hali hii inaonyesha kuwa Kiingereza ni lugha ambayo imepewa hadhi katika mtaala wa elimu ikilinganishwa na Kiswahili, lugha za asili na lugha zingine za kigeni kama vile Kichina. Kiingereza pia kinachukuliwa kuwa lugha ya watu ambaao wamesoma huku Kiswahili kikinasibishwa na watu ambaao hawajasoma. Ni kwa misingi hii ambapo tunasema kuwa Kiingereza kinachukuliwa kuwa lugha bora kutokana na athari za ukoloni nchini Kenya. Kwa mujibu wa Rassool na Edwards (2010) matumizi ya Kiingereza katika mataifa mengi Afrika yalisababishwa na ukoloni na ambaao unaendelea kuathiri utekelezaji wa matumizi ya lugha zingine katika sera ya lugha.

Wasomi hawa wanasema kuwa hali hii huathiri uteuzi na matumizi ya lugha katika ufundishaji wa wanafunzi katika mataifa ya ulumbilugha. Kulingana nao, katika mataifa ya Afrika, Kiingereza ni lugha muhimu katika kutimiza malengo ya kiakademia ya wanafunzi na vile vile huwawezesha kutangamana na watu wa mataifa mengine ulimwenguni. Hali hii inaonyesha kwamba lugha ya Kiingereza huchukuliwa kama nguzo muhimu katika mafanikio ya maishani. Kwa hivyo basi, wanafunzi ambaao wanakijua Kiingereza huwa na nafasi bora ya kujiendeleza kimaisha na vile katika mahusiano ya kijamii kwa watu wa jamiilugha mbalimbali.

Lugha ya Kiingereza inachukuliwa kuwa bora hasa kwa wanafunzi wa shule za msingi na zile za upili walio na malengo ya kujiunga na vyuo vikuu kusomea taaluma mbalimbali. Vyuoni, lugha tumizi katika taaluma kama vile ya udaktari na uhandisi huwa Kiingereza. Kwa sababu hii basi, wanafunzi huchukulia kuwa Kiingereza ni lugha ya watu waliosoma. Hali hii inawafanya wanafunzi kutaka kujua Kiingereza zaidi ikilinganishwa na Kiswahili kwa nia ya kujinasibisha na taaluma ambazo wanazichukulia kuwa bora ikilinganishwa na wanaosomea Kiswahili. Hali hii ilidhahirika katika uandishi wa insha za Kiswahili ambapo wanafunzi wanachopeka maneno ya Kiingereza hapa na pale kama tulivyoonyesha katika vijisehemu vilivyopo hapo juu. Hili linajitokeza pia katika Makala ya Molina (2015) anaposema kuwa idadi kubwa ya wanafunzi nchini Kenya huwa na lengo la kuboresha umilisi wao wa lugha ya Kiingereza ili kuweza kujiunga na vyuo vikuu nchini. Molina anaendelea kusema kuwa wanafunzi ambaao wanataka kusomea somo la biashara nchini Kenya huboresha matumizi yao ya Kiingereza kwa kuamini

kuwa kitawawezesha kupata ajira katika mashirika ya kitaifa na kimataifa kama vile Umoja wa Kimataifa. Hii inaonyesha kuwa Kiingereza kinachukuliwa kuwa nguzo muhimu katika kupata ajira katika mashirika yanayowalipa wafanyakazi wake vizuri. Chukulizi za aina hii ndizo ambazo huwafanya wanafunzi kutaka kutumia Kiingereza zaidi ikilinganishwa na Kiswahili. Kwa hivyo basi, Kiingereza kinachukuliwa kuwa lugha ya biashara. Kwa hali hii basi, wanafunzi wanotaka kuwa wajasiriamali watataka kuboea katika Kiingereza zaidi kwa kuamini kuwa kitawawezesha kupata kazi inayowalipa vizuri.

Nchini Kenya, Kiingereza ndio lugha ambayo inatumiwa zaidi katika mawasiliano mbalimbali kukiwemo bungeni na hata mahakamani. Michieka (2016) anadai kuwa Kiingereza ni lugha muhimu kwa kuwa inatumiwa katika nyanja mbalimbali nchini Kenya kukiwemo nyanja muhimu, mawasiliano ya watu binafsi kama vile baina ya viongozi na vile vile katika biashara za kimataifa. Hata hivyo, Michieka anaendelea kusema kuwa Wakenya huwa na mielekeo tofautitofauti kuhusu lugha ya Kiingereza, ingawa ndio lugha ambayo huwawezesha kutangamana na watu wanaofanya kazi tofauti tofauti. Hali hii inaonyesha kuwa Kiingereza ndio lugha muhimu katika kuendeleza shughuli za kila siku nchini Kenya. Hili ni jambo ambalo laweza kuwa na athari hasi kwa wanafunzi wa shule ya msingi kwa kuamini kuwa Kiingereza ndio lugha muhimu kwa wanaotaka kujiunga na vyuo vikuu na hatimaye kupata ajira nzuri baadaye. Imani hii basi huweza kuwafanya wanafunzi wa shule za msingi kutaka kuboresha zaidi Kiingereza chao ikilinganishwa na Kiswahili. Hii ni athari hasi kwa wanafunzi wa shule za msingi kwa kuwa huwafanya kuegemea lugha ya Kiingereza zaidi na kukipuuza Kiswahili. Katika shule ya Moi Avenue, kwa mfano, wanafunzi waliwekewa sera ya kutumia Kiingereza kuanzia Jumatatu hadi Jumatano huku Kiswahili kikitumiwa Alhamisi na Ijumaa. Hii ina maana kuwa watafitiwa wanatakiwa kutumiwa Kiingereza siku tatu kwa juma na Kiswahili kikaachiwa siku mbili. Ikumbukwe pia kuwa masomo mengi hufunzwa kwa Kiingereza ikilinganishwa na Kiswahili na hili ni jambo ambalo huwaathiriwanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue hasa katika uandishi wao wa insha.

Vyombo vya habari na machapisho mbalimbali ni nyenzo muhimu ya kuikuza lugha fulani. Kwa mujibu wa Michieka (2005) matumizi ya Kiingereza ndio hutawala katika vyombo vya habari, elimu, katika mikutano maalum ambapo lugha inachukua jukumu muhimu katika kufasiri na kusambaza ujumbe muhimu. Vile vile, msomi huyu anasema kuwa Kiingereza huchukuliwa

kuwa lugha ya watu waliosoma. Hivyo basi, mtu ambaye hajabobea kwa lugha ya Kiingereza huchukuliwa kuwa ambaye hajasoma. Mwelekeo wa aina hii basi huwafanya wanafunzi wa shule za msingi kuwa na imani potofu na hivyo basi kutaka kutumia Kiingereza zaidi katika mawasiliano yao kwa kuamini kuwa ndio lugha ya wasomi. Chukulizi za aina hii ndizo huwafanya wanafunzi kujipata wakiwasiliana kwa Kiingereza zaidi ikilinganishwa na Kiswahili na hili ni jambo ambalo huathiri uandishi wao wa insha. Athari hizi hasi katika uandishi wa insha hutokana na mazoea ya kutumia Kiingereza zaidi ikilinganishwa na Kiswahili katika mawasiliano. Hali hii huweza kuwafanya kujipata wakichanganya ndimi katika uandishi wao wa insha na hili ni jambo ambalo huchangia kufeli kwao katika mtihani wa Kiswahili. Tunasema hivi kwa sababu wanafunzi huadhibiwa kwa kuchanganya ndimi katika uandishi wao wa insha. Michieka anaendelea kusema kuwa chukulizi hizi ndizo ambazo huwafanya Wakenya wengi kudai kuwa wao huzungumza na kuandika Kiingereza vizuri sana. Ujinasibishaji huu basi huwafanya pia wanafunzi wa shule za msingi kutaka kujua lugha ya Kiingereza zaidi ikilinganishwa na lugha ya Kiswahili.

Linalojitokeza hapa wazi ni kuwa Kiingereza kinapewa hadhi kuu na Wakenya na hivyo basi, wengi wao hujinasibisha na lugha hii hasa vijana. Michieka anasema kuwa vijana wanakichukulia Kiingereza kuwa lugha bora na ambayo mtu anapaswa kuijua vizuri ikilinganishwa na Kiswahili. Ingawa hivyo, Michieka (2005) anasema kuwa watu wa mashambani na wale ambao hawajasoma huwa na mwelekeo hasi kwa lugha ya Kiingereza. Msomi huyu anadai kuwa hali hii inatokana na kuwepo kwa mielekeo hasi kuhusu Kiingereza katika maeneo ya mashambani nchini Kenya. Anaendelea kusema kuwa hata walimu na watu wengine wa mashambani huwa hawatumii Kiingereza sana katika mawasiliano yao. Na kwa hali hii basi, wanafunzi wa maeneo haya hufuata mienendo yao kwa kutopata watu wengine wakitungia Kiingereza sana katika mawasiliano yao katika maeneo wanamolelewa. Hali hii inathhibitisha maoni ya Habwe na wengine (2010) wanaosema kuwa tabaka na malezi ni mojawapo wa viamuvi ya matumizi ya lugha. Tunasema hivi kwa sababu maoni ya wasomi katika kijishehemu hiki yanaonyesha kuwa Wakenya wanaoishi mijini hutumia Kiingereza zaidi katika mawasiliano wakilinganishwa na wenzao wanaoishi mashambani.

Watafitiwa wa utafiti huu ni wanafunzi wa shule ya msingi ya C.G.H.U na ile ya Moi Avenue. Watafitiwa hawa walilelewa mijini na hivyo basi, kutokana na maoni ya Michieka (2005) ni

kuwa watu wa mijini hupendelea matumizi ya lugha ya Kiingereza zaidi ikilinganishwa na ile ya Kiswahili. Kwa hali hii basi, tunaweza kusema kuwa wanafunzi hawa huwa na mwelekeo hasi kwa Kiswahili kwa sababu ya mazingira walimolelewa na hili ni jambo ambalo huathiri uandishi wao wa insha. Katika isimujamii, Kiingereza huwa na majukumu muhimu katika masuala mbalimbali nchini Kenya kukiwemo lugha ya ufunzaji katika viwango vyote vya elimu, mahakamani na vile vile huwawezesha wanafunzi kupita mtihani (Dhillon na Wanjiru, 2013). Wasomi hawa vile vile wanasema kuwa elimu ya Kenya inategemea sana kupita kwa mitihani ya kitaifa. Ikumbukwe kuwa masomo mengi shulenii hufunzwa kwa Kiingereza na hivyo basi wanafunzi huchukulia kuwa ndio lugha itakayowawezesha kupita mitihani husika. Dhillon na Wanjiru wanaendelea kusema kuwa hali hii ya kukithamini Kiingereza zaidi huwafanya wanafunzi kuwa na vitabu vilivyo na misamiati ya Kiingereza. Huu ni mkakati muhimu wa kuwawezesha kuielewa zaidi lugha ya Kiingereza kwa kuamini kuwa itawawezesha kupita mtihani.

### **2.3.3 Mielekeo ya Wanafunzi Kuhusu Kiswahili**

Kiswahili ni lugha ya taifa na vile vile ni lugha rasmi kwa mujibu wa katiba ya Kenya ya 2010. Kiswahili ni lugha ya kwanza rasmi kulingana na katiba hii ya Kenya kama ilivyotajwa katika kifungu cha 7. Hii inaonyesha kuwa Kiswahili ndio lugha inayopaswa kutumiwa zaidi katika mawasiliano yoyote yale ikilinganishwa na lugha zingine nchini Kenya. Kutajwa kwanza katika katiba ya Kenya ya 2010 kunaashiria kuwa Kiswahili ndio lugha yenye hadhi zaidi ikilinganishwa na Kiingereza. Ingawa hivyo, hali hii ni tofauti hasa shulenii ambapo Kiingereza kinatumiwa kutahini masomo yote isipokuwa somo la Kiswahili. Masomo kama vile Hisabati, Sayansi na Somo la Dini hufunzwa na kutahiniwa kwa Kiingereza. Hii ina maana kuwa wanafunzi hufunzwa kwa Kiingereza kwa saa nyingi ikilinganishwa na somo la Kiswahili ambalo huwa kipindi kimoja tu kwa siku. Kwa hivyo basi wanafunzi amba ni wanaulumbilugha hulazimika kutumia Kiingereza na Kiswahili wanapokuwa shulenii na kisha kutumia lugha zao za asili wanapokuwa nyumbani. Hali hii huzua athari hasi na chanya kwa wanafunzi hasa wanapoandika insha zao.

Nchini Kenya, Kiingereza hutumiwa kutahini masomo mengi ikilinganishwa na Kiswahili. Hata hivyo, kwa mujibu wa Kiango (2002), nchini Kenya, Kiswahili kinatumiwa na watu zaidi ya asilimia 80 huku Kiingereza kikitumiwa na watu wasiozidi asilimia 20. Kiswahili kinatumiwa na

watu wengi ikilinganishwa na Kiingereza hasa katika biashara mbalimbali. Walimu wa shule za msingi huwa muhimu katika kutekeleza sera ya lugha ya Kenya. Mirianga (2014) anasema kuwa walimu wa shule za msingi ni wadau muhimu katika kuendeleza sera ya lugha nchini. Sera anayozungumzia Mirianga ni ile ya Kiswahili kuwa lugha ya taifa na vile vile kuwa lugha ya kwanza rasmi kwa mujibu wa Katiba ya Kenya ya mwaka wa 2010. Ingawa hivyo, ni muhimu kutaja hapa kuwa walimu wa shule za msingi hufunza masomo mbalimbali kukiwemo Sayansi ambayo hutahiniwa kwa Kiingereza. Hii inaonyesha kuwa walimu hawa hulazimika kufunza kwa Kiingereza kwa kuwa ndio lugha ya utahini. Walimu wanapofunza masomo ambayo hutahiniwa kwa Kiingereza wakati mwingine hulazimika kutumia Kiswahili kwa baadhi ya misamiati ili waweze kueleweka ipasavyo na wanafunzi wao. Hili hufanyika kwa nia ya kutumia maneno ambayo yanapatikana katika mazingira ya wanafunzi. Kwa mujibu wa Ogechi na Jwan (2004) walimu wa masomo kama vile Hisabati na Sayansi hutumia Kiswahili wanapozungumzia misamiati fulani fulani. Hii ina maana kuwa walimu wanapofunza masomo ambayo hutahiniwa kwa Kiingereza huchanganya ndimi katika ufunzaji wao. Wasomi hawa wanasema kuwa walimu hutumia misamiati ya Kiswahili ambayo inaeleweka na wanafunzi zaidi ikilinganishwa na maneno ya Kiingereza katika somo husika. Kwa hali hii basi, tunaweza kusema kuwa walimu wanaofunza masomo yanayotahiniwa kwa Kiingereza pia hukikuza Kiswahili wanapofunza darasani.

Kiswahili ni lugha ya kwanza rasmi ikifuatiwa na Kiingereza nchini Kenya. Lugha rasmi huwa na majukumu muhimu ambayo yanafaa kutekeleza katika nchi husika. Kulingana na Wardhaugh (1986) lugha rasmi inapaswa kutumiwa katika kuendesha shughuli zote za serikali, kufundishia katika shule za msingi hadi vyuo vikuu na hutumika katika hati zote za serikali. Hii inaonyesha kuwa lugha rasmi inapaswa kutumika kwingi katika mawasiliano rasmi kukiwemo kufundishia katika nchi husika. Hata hivyo, kama tulivyosema awali, Kiingereza ndio lugha inayotumiwa kutahini masomo mengi ikilinganishwa na Kiswahili nchini Kenya. Hii inaashiria kuwa sera ya lugha Kenya haijaweza kutekelezwa kikamilifu na hasa katika elimu ambapo Kiingereza kinatumiwa katika kufundishia na katika utahini katika masomo yote isipokuwa somo la Kiswahili pekee huku Kiswahili kikipuuzwa katika masomo mengine.

Kiswahili ni lugha ya taifa pia nchini Kenya. Lugha ya taifa hutumiwa katika mawasiliano mapana ya nchi husika kama asemavyo Mathooko (2007) kuwa ni lugha iliyovuka mipaka ya

kikabila na hivyo kuwaunganisha Wakenya. Lugha unganishi hutumika kwingi na hili linabainika na Kibui (2014) anaposema kuwa Kiswahili ni lugha sambazi nchini Kenya. Kibui anaendelea kusema kuwa usanifishaji wa mwaka wa 1930 ulikikweza Kiswahili. Ingawa hivyo, wasomi hukidunisha Kiswahili jambo ambalo linakiuka sera ya lugha ya Kenya. Anaonyesha namna Kiswahili kimepewa vipindi vichache shulen ikiinganishwa na Kiingereza. Anasema kuwa katika shule ya upili Kiswahili kina vipindi vitano huku Kiingereza kikiwa na vipindi sita katika kidato cha kwanza na cha pili. Kiswahili kina vipindi sita kinyume na Kiingereza kilicho na vipindi nane katika kidato cha tatu na nne. Hii inaonyesha kuwa wasomi wanakienzi Kiingereza zaidi ikiinganishwa na Kiswahili ambacho kimepewa nafasi fedhehi na Wakenya waliosoma.

Kiswahili kinachukuliwa kuwa muhimu katika uhamasishaji wa Wakenya kuhusu suala fulani. Haya yanabainishwa na Kinoti (2019) anayesema kuwa Kiswahili ni lugha ambayo inafaa kutumiwa katika uhamasishaji wa wananchi katika masuala yote yanayowahusu. Kinoti anasema kuwa Kiswahili kinaeleweka na watu wa tabaka zote nchini Kenya. Anasema pia kuwa matangazo kuhusiana na masuala mbalimbali ya kimazingira na ya kibiashara yanaweza kutolewa kwa lugha ya Kiswahili kwa manufaa ya Wakenya. Kwa mujibu wa Kinoti, Kiswahili ni chombo imara cha kuelimisha umma wa Wakenya kuhusu jambo fulani la kitaifa. Anasema hivi kwa sababu Kiswahili ni lugha ya taifa na sambazi nchini Kenya. Kwa hivyo basi, kutumia Kiingereza katika kutahini masomo mengi ikiinganishwa na Kiswahili ni kukiuka sera ya lugha ya Kenya.

Kwa mujibu wa sera ya lugha nchini Kenya Kiswahili ndio lugha iliyopewa majukumu mawili: lugha rasmi na ya taifa. Kwa hali hii basi, tunaweza kusema kuwa Kiswahili kimekwezwa katika katiba ya Kenya na hivyo basi kinapaswa kutumiwa zaidi hata katika elimu ya shule za msingi. Ontieri (2017) anasema kuwa Kiswahili ndio lugha ambayo inafaa kuwa inaeleweka na kutumiwa na Wakenya wengi na kutumiwa kwa ajili ya mawasiliano ya kila siku kukiwemo kufundishia. Ingawa hivyo, Ontieri anasema kuwa lugha hii ya Kiswahili imekuwa ikipuuzwa na Wakenya na kuchukuliwa kama lugha ya watu wasio na elimu. Hii inaonyesha kuwa watu waliosoma nchini Kenya hukiona Kiswahili kama lugha fedhehi. Hapa Kiswahili kinachukuliwa kuwa cha watu ambao hawajasoma. Hali ya kuupuza na kukidunisha Kiswahili ni jambo ambalo linakiuka sera ya lugha ya taifa la Kenya.

## **2.4 Hitimisho**

Katika sura hii, tuliangazia ulumbilugha na mielekeo kuhusu lugha ya Sheng', Kiingereza na Kiswahili. Ikumbukwe kuwa jukumu kuu la lugha yoyote ile ni kukidhi haja ya kimawasiliano na hivyo basi hakuna lugha duni au yenyе hadhi kuliko nyingine. Tulionyesha kuwa Sheng' hupata misamiati yake kutokana na lugha zingine. Sheng' pia imesambaa na hata kutumiwa na wanafunzi wa shule za msingi na hili ni jambo ambalo linawaathiri wanapoandika insha. Tulionyesha kuwa Kiingereza ni lugha rasmi na hutumiwa katika utahini wa masomo mengi ikilinganishwa na Kiswahili. Kiingereza pia kinachukuliwa kuwa lugha ya wasomi. Kwa upande mwingine, Kiswahili kinachukuliwa kuwa lugha duni na ambayo hutumiwa na watu ambao hawajasoma licha ya kuwa ni lugha ya kwanza rasmi na vile vile ya taifa kwa mujibu wa katiba ya Kenya ya 2010. Kutokana na mielekeo hii kuhusu Sheng', Kiingereza na Kiswahili, tunaweza kusema kuwa wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na ile ya Moi Avenue waliathirika kwa njia hasi na chanya hasa katika uandishi wao. Haya ndio tuliyashughulikia katika sura zifuatazo ambapo tulianza kwa athari za Sheng' na Kiingereza kwa Kiswahili katika mofolojia na sintaksia kama inayojitokeza katika insha za watafitiwa wetu.

## **SURA YA TATU**

### **ATHARI ZA KIINGEREZA NA SHENG' KWA MOFOLOJIA YA KISWAHILI KATIKA UANDISHI WA INSHA**

#### **3.0 Utangulizi**

Katika sura ya pili tulishughulikia mielekeo ya wanafunzi wa shule za msingi kuhusu Sheng', Kiswahili na Kiingereza. Tulionyesha kuwa Sheng' huwa na muundo sahili na hivyo basi wanafunzi hujipata wakifuata mtindo wake wa uundaji wa leksemu katika uandishi wa insha. Sheng' hutumia mbinu mbalimbali kuundia leksemu zake. Mbinu hizi ni kama vile ukopaji kutoka kwa Kiswahili na lugha zingine za asili, ukatizaji au ufupishaji wa maneno, Uambishaji na unyambuaji wa maneno, ubadilishaji silabi, upolisemia, ubunaji, uhulutishaji na akronimu. Mbinu hizi huwa sahili na hivyo basi misamiati ya Sheng' huwa imesahilishwa. Wanafunzi ambao walizoea kutumia Kiingereza na Sheng' katika mawasiliano yao hujipata wakifuata mtindo wa uundaji wa leksemu au kutumia maneno ya lugha hizi wanapoandika insha. Hali hii ndio tulishughulikia katika sura hii ambapo tuliangazia athari hasi na chanya za Sheng' katika uandishi wa insha za wanafunzi wa shule ya msingi ya CGHU na ile ya Moi Avenue. Katika sura hii, tulishughulikia athari ambazo zinajitokeza kimofolojia.

Katika sura ya pili, vile vile tulionyesha kuwa wanafunzi wanachukulia Kiingereza kama lugha yenye hadhi zaidi ikilinganishwa na Kiswahili. Hii ni kwa sababu Kiingereza kinatumwiwa katika utahini wa masomo mengi kukiwemo Hisabati na Sayansi. Hii ina maana kuwa wanafunzi hutumia Kiingereza zaidi wanapokuwa wakifunzwa shulenii ikilinganishwa na Kiswahili. Vile vile, katika sura ya pili tulionyesha kuwa Kiingereza kinachukuliwa kuwa lugha ya wasomi. Kwa hali hii basi, wanafunzi hujipata wakitumia maneno ya Kiingereza wanapoandika insha. Hali hii ni nadra sana wanapoandika insha za Kiingereza yaani 'composition.' Katika utafiti huu, tulibaini kuwa baadhi ya athari za Kiingereza kwa Kiswahili katika uandishi wa insha ni kuchanganya ndimi na kuendeleza maneno kwa kufuata mtindo usiofaa. Katika kuchanganya ndimi, wanafunzi wa shule za msingi hujipata, (bila kukusudia) wakitumia maneno ya Kiingereza wanapoandika insha. Hili husababishwa na mazoea yao ya kutumia lugha zaidi ya moja wanapowasiliiana. Hii ndio sababu tunasema kuwa ulumbilugha huwa na athari hasi na chanya kwa wanafunzi wa shule za msingi. Katika sura hii, tulishughulikia athari hasi na chanya

za Kiingereza na sheng' katika uandishi wa insha katika shule za msingi. Ni kwa misingi hii ambapo tunashughulikia athari za kimofoljia za Kiingereza na Sheng' kwa insha, katika sura hii.

### **3.1. Athari za Sheng' Kimofoljia katika Uandishi wa Insha za Kiswahili**

Katika sura hii, tulishughulikia athari hasi na chanya za Kiingereza na Sheng' katika uandishi wa insha katika shule teule za msingi. Tulijikita kwa namna wanafunzi waliathiriwa na ulumbilugha kwa kuangazia athari za Kiingereza na Sheng' katika Kiswahili wakati wanapoandika insha. Tulionyesha namna wanafunzi wa shule ya msingi ya CGHU na Moi Avenue hutumia baadhi ya leksemu za Kiingereza na Sheng' katika uandishi wa insha. Awali, tulionyesha kuwa Sheng' ni lugha sahili na hivyo basi watumizi wake hujipata wakiutumia mtindo wake wa uundaji wa leksemu hata pasipofaa kama vile katika uandishi wa insha. Athari hasi za Kiingereza na Sheng' ambazo tulizingatia katika sura hii ni ukataji wa silabi za Kiswahili visivyo, Kuandika ukubwa na udogo kwa namna isiyofaa na mnyambuliko wa vitenzi kwa namna isiyofaa. Ikumbukwe kuwa kila lugha ina upekee wake na hasa katika uundaji wa misamiati. Nadharia ya kumudu inadai kuwa mtu huathiriwa kilugha na jamii anamokulia kwa namna anapotumia lugha azijuazo huku akizibadilisha. Kwa mujibu wa nadharia hii ya kumudu, wanafunzi ambao wanaishi katika mazingira ambapo Sheng' inatumiwa zaidi huku wakifunzwa masomo mengi kwa lugha ya Kiingereza shuleni hujipata wakiingiza leksemu za Sheng' na Kiingereza wanapoandika insha zao. Matumizi ya Kiingereza na Sheng' katika uandishi wa insha ni athari inayotokana na jamii anapokulia mwanafunzi. Athari hizi ndizo tulizozishughulikia katika sura hii na tulianza kwa ukataji silabi kwa namna isiyofaa katika sehemu ifuatayo.

#### **3.1.1 Ukataji Silabi za Kiswahili kwa Namna Isiyofaa**

Katika uandishi wa insha, wanafunzi hutakiwa kutumia Kiswahili pekee yake bila kuchanganya ndimi. Hata hivyo, wakati mwingine wanafunzi huathiriwa na mtindo wa kuunda leksemu za Sheng' ambao huwa sahili kiasi cha kujipata wakiufuata wanapoandika insha. Hii ina maana kuwa wao hutumia maneno kwa kifupi au kuunganisha maneno kwa namna isiyofaa bila kujali kuwa kila lugha ina mbinu zake za uandishi na sharti zifuatwe iwapo wanataka kupata alama nzuri. Hali hii sivyo ilivyo katika uandishi wa maneno ya Kiswahili kwa kuwa wanafunzi wa shule ya msingi ya CGHU na Moi Avenue walidhihirisha kuwa waliathiriwa na Kiingereza na Sheng' katika insha zao. Kutokana na data ya utafiti huu, tuligundua kuwa wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue huandika baadhi ya maneno kwa njia sahili na bila

kuzingatia mtindo wa uandishi wa Kiswahili. Hivyo basi watafitiwa wetu waliathirika na ulumbilugha. Kwa mujibu wa nadharia ya uchanganuzi makosa, kosa ambalo lilijitokeza zaidi ni la ukataji wa silabi kwa namna isiyofaa katika insha. Nadharia hii inahoji kuwa makosa yanayofanywa huwa na visababishi vyake. Ukataji wa silabi kwa namna isiyofaa katika uandishi wa insha za Kiswahili unasababishwa na hali ya kutaka kusahilisha mawasiliano. Hali ya kusahilisha mawasiliano hujitokeza katika lugha vipindi ya Sheng' na ndio sababu tunasema kuwa wanafunzi waliathiriwa na ulumbilugha. Hii huwa athari hasi kwa kuwa wanafunzi wa shule ya msingi ya CGHU na wenzao wa Moi Avenue hukata silabi visivyo hasa mwishoni mwa msitari na hili ni jambo ambalo huwafanya kupata alama za chini katika insha zao. Hili lilijitokeza katika dondoo lifuatalo kutoka kwa insha ya mwanafunzi wa darasa la sita, shule ya CGHU:

1. a) **Ilikuwa Jumamosi asubuhi na mapema. Wazazi wangu walipopokeasimu kutoka kijijini mwetu. Kwa vile dada aliyeoleka kwa familia ya matajiri aliweza kujifungu.**

*(Ilikuwa Jumamosi asubuhi na mapema. Wazazi wangu walipopokeasimu kutoka kijijini mwetu. Kwa vile dada aliyeolewa kwa familia ya Matajiri alijifungua.)*

Dondoo 1a) ni kutoka kwa insha ya mwanafunzi wa shule ya msingi ya CGHU na limenukuliwa bila kufanyiwa marekebisho yoyote. Mwanafunzi huyu amelikata neno **wazazi** (**waz-azi**) visivyo kwa sababu ya kutaka kusahilisha uandishi wake. Mwanafunzi alitakiwa kuliandika neno hili kwa namna sahihi ambayo huhusisha kukata silabi nzima kama ifuatavyo **waza-zi** au **wa-zazi**. Athari hii inasababishwa na mazoea ya kutumia Sheng' kwa kuwa watumizi wake husahilisha misamiati. Tulisema hivi kwa kuwa wanafunzi walizoea kutumia Sheng' ambayo leksemu yake ni sahili na hivyo basi walifuata mtindo uo huo husika hata katika Kiswahili. Kwa mfano, baadhi ya maneno ya Sheng' huwa na silabi fungo kwa kuwa huishia kwa konsonanti. Maneno haya ni kama vile:

2. Sheng'	silabi	Kiswahili
Dem	de-m	msichana
Myeng'	m-ye-ng'	mrembo

Dom	do-m	bangi
Shash	sha-sh	bangi
Kitos	ki-to-s	tumbako

Linalojitokeza katika mifano 2) ya misamiati ya Sheng' ni kuwa maneno yanaishia kwa silabi funge. Athari hizi za kukamilisha neno kwa silabi funge zinawafanya wanafunzi kukata maneno visivyo katika sentensi. Kutokana na data ya utafiti huu, tulipata kuwa wanafunzi wa shule za msingi za CGHU walikata maneno visivyo bila kuzingatia muundo wa silabi za Kiswahili kama tulivoonyesha awali katika kijisehemu hiki. Mifano mingine ni kama vile, **daras-ani** badala ya da-ra-sa-ni, **bib-i** badala ya bi-bi na **har-usi** badala ya ha-ru-si. Ni kwa misingi hii ambapo tunasema kuwawatafitiwa wetu wanahamisha sifa za Sheng' ambayo ni lugha vipindi kwa Kiswahili na hili ni jambo ambalo liliwafanya kupata alama za chini ikilinganishwa na wenzao wanaofuata kanuni za ukataji neno wanapofika mwishoni mwa msitari katika uandishi wa insha. Ni kwa misingi hii ambapo tunasema kuwa matumizi ya Sheng' huwaathiri wanafunzi wa shule za msingi kwa njia hasi hasa katika uandishi wao wa insha.

Tulikumbana pia na athari hasi ya Sheng' ya kusahilisha neno na kulikata kwa namna isiyofaa katika insha za wanafunzi wa shule ya msingi ya Moi Avenue. Wanafunzi hawa, kama wenzao wa CGHU pia walikata silabi kwa namna isiyofaa kama inavyobainika katika insha ifuatayo ya mmoja wao:

### 3. a) Paka wangu alizaa watoto waw-

**ili wote walikuwa wasichana.** (Paka wangu alizaa watoto wa kike wawili)

Mwanafunzi amekata neno **wawili** visivyo. Neno hili lina silabi tatu- wa-wi-li ila mwanafunzi analiandika kama **waw-ili**. Hili ni kosa ambalo linatokana na athari ya Sheng' ya kurahisisha mawasiliano kama tulivoonyesha katika mifano ya misamiati ya Sheng' bila kuzingatia kuwa kila lugha ina upekee wake. Hii ni athari iliyotokana na ulumbilugha kiasi cha kuwafanya wanafunzi wa shule za msingi kutozingatia mtindo wa ukataji wa silabi katika Kiswahili. Katika Kiswahili, mwanafunzi anatakiwa kukata silabi nzima iwapo neno halitoshei katika msitari husika. Vile vile, mwanafunzi anaweza kuanza neno katika msitari unaofuata iwapo anaona kuwa haliwezi kutoshea katika nafasi iliyobaki. Hata hivyo, hali hii ni kinyume kutokana na data

ya utafiti huu ambapo wanafunzi wanakata herufi badala ya kuzingatia silabi. Wapo watafitiwa ambao walikata silabi nzima na hifuata mtindo unaokubalika katika Kiswahili. Kwa mfano:

**4 a) Siku ya shere-**

**he tuliamka alfajiri na kupata stftahi.**

**b) Mimi hupenda kuchunga mbu-**

**zi wangu kila wakati wa jioni.**

Mifano 4a), na b), kutoka kwa insha ya mwanafunzi wa Moi Avenue inaonyesha kuwa watafitiwa wanazingatia kanuni za Kiswahili za ukataji silabi wanapofika mwishoni mwa msitari kinyume na tulivyoonyesha awali ambapo wanafunzi wanakata sauti. Ikumbukwe kuwa wanafunzi hawa wote ni wanaulumbilugha. Licha ya kuwa watafitiwa wetu ni wanaulumbilugha, baadhi yao wanafuata kanuni zifaazo za Kiswahili za kuandika insha huku wengine wakishindwa kumudu Kiswahili. Kwa mujibu wa nadharia ya kumudu, upo umudu lugha wa kibinafsi ambapo mtu binafsi hifuata kanuni za lugha husika. Kwa hivyo basi, kutokana na data ya utafiti huu, tunaweza kusema kuwa wanafunzi ambao walizingatia kanuni za uandishi katika insha walidhihirisha umudu lugha wa kibinafsi kinyume na wale ambao walikosa kuzingatia kanuni za uandishi wa insha za Kiswahili. Watafitiwa wa utafiti huu walikulia katika jamii ambamo watu ni wa jamiilugha mbalimbali na hivyo basi ni wanawingilugha. Athari ya mazingira wanamolelewa inajitokeza wakati ambapo watafitiwa wanashindwa kumudu lugha ya Kiswahili kutokana na athari za wingilugha ingawa hivyo, wapo wengine ambao wanamudu lugha zote na hivyo basi wanajua upekee wa lugha fulani. Athari hii hasi huwafanya wanafunzi kupata alama za chini ikilinganishwa na wenzao ambao hawajaathiriwa na ulumbilugha.

### **3.1.2.0 Kuandika Ukubwa na Udogo wa Nomino kwa Namna Isiyofaa**

Kiswahili kina namna yake ya kuandika maneno katika hali ya ukubwa na udogo. Hata hivyo, tulibaini kuwa wanafunzi huendeleza maneno haya katika hali ya ukubwa na udogo kwa kufuata mtindo wa Sheng'. Hii ni athari ambayo inatokana na kuishi katika mazingira ambamo Sheng' inazungumzwa. Mazingira ni mojawapo wa mambo ambayo huchangia katika matumizi ya lugha. Hili libainika wakati ambapo wanafunzi wanakuwa na mtindo tofauti wa kuendeleza maneno katika hali ya ukubwa na udogo. Wanafunzi walifuata mtindo sahili wa kuandika

maneno katika hali ya udogo au ukubwa. Mojawapo wa mihimili ya nadharia ya kumudu ni wanaulumbilugha huamua lugha ipi itumike wapi na itumike vipi. Umilisi wa lugha zaidi ya moja huwapa watu uhuru wa kuteua na kutumia lugha fulani kutegemea mazingira. Ingawa hivyo, data ya utafiti huu ilionyesha kuwa watafitiwa wetu huathiriwa kwa njia hasi na ulumbilugha wanapoandika insha. Insha za wanafunzi wa CGHU na Moi Avenue waliathiriwa na Sheng' na hivyo kujipata wakiendeleza misamiati ya Kiswahili kwa namna isiyofaa. Tunasema hivi kwa sababu watumizi wa Sheng' huunda misamiati kwa njia sahili. Hali hii inawafanya wanafunzi ambao walilelewa katika mazingira yaliyojaa matumizi ya Sheng' kufuata mtindo usiofaa wa kuandika ukubwa au udogo wa nomino katika uandishi wa insha. Tulianza kwa kuandika ukubwa wa nomino kwa namna isiyofaa katika kisehemu kifuatacho:

### **3.1.2.1 Kuandika Ukubwa wa Nomino kwa Namna Isiyofaa**

Katika Kiswahili, nomino huwa katika hali ya kawaida, ukubwa au udogo. Katika ukubwa, nomino hurejelea hali yenye ukubwa na sifa zisizo za kawaida. Ukubwa wa nomino hubainishwa kwa kutumia kiambishi awali **Ji-** katika hali ya umoja na **ma-** katika wingi. Kwa mfano, Ukubwa wa neno mbwa ni **jibwa** katika hali ya umoja na **majibwa** katika wingi. Hii ina maana kuwa nomino za Kiswahili huwa katika ngeli ya li-ya zinapobadilishwa katika hali ya ukubwa. Ingawa hivyo, hali hii ni tofauti katika uandishi wa insha za wanafunzi ambao wanafuata mtindo sahili wa kuandika neno katika hali ya ukubwa. Hii ni kutohana na athari za ulumbilugha katika mawasiliano yao jambo ambalo huwafanya kuendeleza maneno bila kuzingatia kuwa kila lugha ina jinsi yake ya kuendeleza maneno.

Watumizi wa Sheng' katika mawasiliano yao hutumia kiambishi **li-** kurejelea ukubwa wa nomino. Hali hii haipaswi kujitokeza katika Kiswahili na inapo jitokeza katika insha, basi, wanafunzi huadhibiwa kwa kutolewa alama za kosa la sarufi. Katika utafiti wetu, tulibaini kuwa wanafunzi wa shule ya msingi ya CGHU na ile ya Moi Avenue wanatumia viambishi tofauti kuandika katika hali ya ukubwa. Tuligundua kuwa wanafunzi wanatumia kiambishi **li-** kuandika katika ukubwa badala ya **ji-**. Hali hii inabainika katika insha ya mwanafunzi wa shule ya Moi Avenue kama ifuatavyo:

#### **5. Alice alikuja kutupokea, sasa walikuwa na jumba likubwa la kushanganza.**

(Alice alitupokea kwa jumba kubwa ajabu)

Dondoo 5), la insha ya mwanafunzi linaonyesha athari ya Sheng' katika uandishi wa nomino katika hali ya ukubwa. Mwanafunzi anatumia kiambishi **li-** kurejelea ukubwa wa nomino nyumba. Mwanafunzi ameathirika na ulumbilugha kiasi cha kukosa kujua kuwa neno **jumba** ambalo amelitumia linaashiria hali ya ukubwa wa nomino nyumba. Hii inaashiria kuwa mwanafunzi aliathiriwa na ulumbilugha na hasa kutokana na kuishi katika mazingira ambamo Sheng' inatumiwa katika mawasiliano.

Vile vile tulikumbana na matumizi ya kiambishi **li-** kurejelea ukubwa katika insha ya wanafunzi wa shule ya CGHU. Hii ilionyesha kuwa wanafunzi wa shule za msingi waliathiriwa na ulumbilugha na hili ni jambo ambalo linawafanya kuadhibiwa kwa kutolewa nusu alama kwa kosa la kisarufi. Katika insha za wanafunzi wa shule ya msingi ya CGHU, tuligundua kuwa wanafunzi walitumia kiambishi **li-** kurejelea ukubwa wa nomino mtoto. Hili linabainika katika insha ifuatayo yenye mada Mnyama Nimpendaye:

**6. Mimi humfungia ng'ombe wangu na litoto lake likubwa katika nyumba yao usiku.** (Mimi humfungia ng'ombe na jindama lake kubwa ndani ya nyumba usiku)

Athari ya ulumbilugha inajitokeza hapa wazi ambapo mwanafunzi anatumia kiambishi **li-** kurejelea ukubwa wa nomino ndama. Mwanafunzi anatumia kiambishi **li-** pia katika neno **kubwa**, na hili ni kosa kwa kuwa ameliendeleza neno visivyo.

Pia wanafunzi wa shule ya msingi ya Moi Avenue wanaandika maneno katika ukubwa kwa namna isiyofaa kutokana na athari za Sheng'. Wanafunzi hawa, kama wenzao wa shule ya msingi ya CGHU wanatumia kiambishi **li-** visivyo kurejelea ukubwa wa nomino za Kiswahili kama ifuatavyo:

**7. Niliweka nguo zetu lisanduku lililokuwa kwetu.** (Nilitia nguo zetu ndani ya jisanduku lililokuwa nyumbani kwetu).

Mtafitiwa ameliandika neno sanduku katika mfano 7), visivyo katika hali ya ukubwa na hili ni jambo linaloonyesha kuwa aliathiriwa na ulumbilugha. Mtafitiwa alitumia kiambishi **li-**badala ya **ji-** ambacho hutumiwa kuandika ukubwa wa nomino katika Kiswahili. Vile vile, katika shule hiyo hiyo, mfano 8), mwanafunzi ameliandika neno shimo visivyo katika ukubwa Ifuatavyo:

### **8. Aladdin akaingia ndani kwenye lishimo.... (Aladdin aliingia ndani ya jishimo)**

Mtafitiwa pia anatumia kiambishi **li-** kubadilisha nomino kutoka hali ya wastani hadi kwa ukubwa. Hili ni kosa kwa kuwa anatumia mtindo wa Sheng' kuendeleza maneno katika hali ya ukubwa. Watumizi wa Sheng' hutumia kiambishi **li-** kurejelea ukubwa wa nomino kama vile **limama** na **libaba**. Kutokana na mifano hii, kiambishi **li-** kimetumiwa kurejelea ukubwa wa nomino mama na baba mtawalia. Katika Kiswahili, kiambishi **ji-** hutumiwa kuandika nomino katika hali ya ukubwa, kwa mfano jitoto, jibaba, jitabu na kadharika. Ni kwa misingi hii ambapo tunasema kuwa mtafitiwa alikosea kwa kuhamisha mtindo wa uundaji wa leksemu wa lugha vipindi ya Sheng' hadi kwa Kiswahili na hii ni athari hasi kwa kuwa anaadhibiwa kwa kutolewa alama.

Tulionyesha kuwa wanafunzi wa shule ya msingi ya CGHU na ya Moi Avenue huandika nomino katika ukubwa kwa namna isiyofaa kutokana na athari za ulumbilugha. Nomino ambazo zimeendelezwa visivyo ni kama vile mtoto, kitabu, sanduku na shimo. Maneno haya yanapaswa kuandikwa ifuatavyo kwa ukubwa katika Kiswahili, katika hali ya umoja na wingi:

## **9. Umoja            ukubwa            Matumizi yake katika insha**

Jitoto	majitoto	litoto
Jitabu	majitabu	litabu
Jisanduku	majisaduku	lijisanduku
Jishimo	majishimo	lishimo

Mifano 9), inaashiria kuwa wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue hufuata mtindo tofauti wa kuandika nomino katika ukubwa kinyume na ilivyo katika lugha ya Kiswahili. Kulingana na nadharia ya uchanganuzi makosa, makosa yanayojitokeza katika mawasiliano huwa na visababishi vyake kukiwemo mazingira. Visababishi hivi husababisha makosa ya kisarufi. Watafitiwa wa utafiti huu wanaishi katika mazingira ambamo jamii huchanganya ndimi katika mawasiliano yao. Wanafunzi hawa basi walijipata wakifuata kanuni za lugha ya Sheng' kiasi cha kuwafanya kutumia kiambishi awali ma- kurejelea ukubwa badala ya li-. Athari hasi ya Sheng' inawafanya watafitiwa kutumia kiambishi li- kuandika ukubwa badala ya ji-. Kando na kuwa nomino za Kiswahili huweza kuandikwa katika ukubwa, nomino pia hubadilika katika hali ya udogo kama tuliavyoonyesha katika kisehemu kifuatacho:

### **3.1.2.2 Kuandika Udogo wa Maneno kwa Namna Isiyofaa**

Nomino za Kiswahili huandikwa kwa udogo kwa kutumia kiambishi **ki-** katika umoja na **vi-** katika hali ya wingi. Hii ina maana kuwa nomino za Kiswahili huwa katika ngeli ya ki-vi zinapobadilishwa katika hali ya udogo. Hata hivyo, utafiti huu ulibaini kuwa wanafunzi hutumia mtindo tofauti kuandika nomino katika hali ya udogo. Hali hii ilisababishwa na athari hasi za ulumbiluga ambazo huwafanya wanafunzi wasizingatie kanuni za Kiswahili katika uandishi wa maneno katika udogo. Katika utafiti huu, tulibaini kuwa wanafunzi hutumia kiambishi **ka-** au **tu-** wanaporejelea nomino katika udogo. Hii ni athari iliyowafanya kupoteza alama kwa kuendeleza maneno visivyo. Hili lilijitokeza katika insha ya mwanafunzi wa CGHU ifuatayo:

## **10. Mimi ukuzanya mbegu zote tulizokula na kunzi anika. ..... mbegu zangu na kuzieka kwa tusuku na kuweka mchanga kwenye tusuku**

**zangu na kuzipanda mbegu zangu.**(Mimi hukusanya mbegu zote na kuzianika kisha huzipanda kwa vijikasuku vilivyo na mchanga.)

Mfano 10), ulidondolewa kutoka kwa insha ya mwanafunzi wa darasa la tano wa shule ya msingi ya CGHU. Mada ya insha ilikuwa Jinsi ya Kutunza Mimea. Kasuku ni mkebe ambaa huuzwa ukiwa na mafuta ya kupika kwa jina ‘Kasuku.’ Mkebe huu unapoisha mafuta unaweza kutumiwa kwa shughuli zingine kama vile kuchota maji au pia watoto hupanda mimea ndani hasa kwa kufanya kazi ya somo la Sayansi. Neno kasuku linapaswa kundelezwa ipasavyo katika umoja na wingi katika hali ya udogo. Nomino hii huingia katika ngeli ya ki-vi inapoandikwa katika udogo kwa maana kuwa neno hili litaanza kwa kiambishi **ki-** katika hali ya umoja na **vi-** katika wingi. Ingawa hivyo, kutokana na athari hasi ya Sheng’ wanafunzi wanatumia kiambishi ka- kuandika udogo wa nomino katika umoja na **tu-** katika wingi kama ilivyobainika katika mifano ifuatavyo:

## 11. Kiswahili **Sheng'**

<b>Umoja</b>	<b>wingi</b>	<b>Umoja</b>	<b>Wingi</b>
Kijikasuku	vijikasuku	kakasuku	tukasuku
Kijigari	vijigari	kagari	tugari
Kivulana	vijivulana	kavulana	tuvulana

Kutokana na data ya utafiti huu, tuligundua kuwa watafitiwa wetu wanatumia kiambishi**ka-**kuashiria udogo wa nomino katika hali ya umoja **natu-**kuashiria wingi wa nomino husika kama ambavyo tulionyesha katika mifano 11), hapo juu. Katika Kiswahili, viambishi mbalimbali huwa na matumizi maalum katika sentensi. Kiambishi **ka-**huonyesha vitendo kadhaa vikitokea kwa mfuatano. Kwa mfano, **Tulifika** nyumbani mapema, **tukaosha** vyombo, **tukafua** nguo na **tukapika** chajio. Sentensi hii iko katika wakati uliopita ambapo kiambishi **ka-** kinajitokeza kwa vitenzi vitatu katika sentensi hii. Pia, sababu sentensi hii iko katika wakati uliopita, kiambishi **ka-** kinatumika kuonyesha mfuatano wa vitendo katika wakati uliopita. Hata hivyo tulibaini kuwa wanafunzi walioathirika na ulumbilugha hutumia kiambishi **ka-** kurejelea udogo wa nomino mbalimbali. Haya tuliyashuhudia katika insha za wanafunzi wa shule ya msingi ya CGHU na Moi Avenue kama ifuatavyo:

**12. Tulipofika njiani, tulikutana na kamtoto kengine kakatuonyesha mahali kanisa ilikuwa.** (Tulipofika njiani, tulielekezwa kanisani na kijitoto kingine)

Mfano 12), ni sehemu ya insha yenye mada ‘Siku ya Furaha’ ya mwanafunzi wa shule ya msingi ya CGHU. Mtafitiwa ametumia kiambishi **ka-** kuonyesha udogo wa nomino mtoto. Hii ni athari hasi inayotokana na kuishi katika mazingira ambamo watu wanatumia Sheng’ katika mawasiliano yao. Kutokana na athari ya ulumbilugha wanafunzi hujipata wakifuata mtindo wa uundaji wa leksemu wa Sheng’ na kusahau kuwa kila lugha ina upekee wake kama tulivyoonyesha katika mifano iliyo hapo juu ya kuandika nomino katika udogo katika Kiswahili na Sheng’. Pia tulikumbana na matumizi ya kiambishi **ka-** katika insha ya wanafunzi wa shule ya msingi ya Moi Avenue. Wanafunzi hawa pia walikuwa wametakiwa kuandika insha kuhusu Siku ya Furaha na kutokana na athari za ulumbilugha, wanatumia viambishi visivyo kama ifuatavyo:

**13. Tulipokuwa tuking’ang’ania keki, rafiki yangu Brian alianguka kwa kashimo kadogo hapo nje ya kanisa.** (Rafiki yangu alianguka kwa kijishimo tulipokuwa tuking’ang’ania keki.)

Katika mfano 13), nomino shimo imeandikwa visivyo katika hali ya udogo. Kutokana na athari za ulumbilugha, mwanafunzi anashindwa kuthibiti matumizi yake ya Kiswahili katika uandishi wa insha. Athari hii ya ulumbilugha ni hasi kwa kuwa mwanafunzi anakosa kuzingatia upekee wa Kiswahili wanapoandika nomino katika hali ya udogo. Hii ndio maana wanafunzi wanatumia kiambishi **ka-** badala ya **ki-** wanaporejelea nomino za Kiswahili katika hali ya udogo.

Maneno ambayo yameandikwa katika hali ya udogo visivyo katika insha za watafitiwa wetu ni mengi, kukiwemo mtoto, shimo na msichana. Maneno haya yanapaswa kuendelezwa ifuatavyo katika udogo, umoja na wingi:

**14. Kiswahili** **Matumizi yake katika insha**

<b>Umoja</b>	<b>Wingi</b>	<b>Umoja</b>	<b>Wingi</b>
Kijitoto	vijitoto	kamtoto	tumtoto
Kijishimo	vijishimo	kashimo	tushimo
Kisichana	Vijisichana	kasichana	tusichana

Mfano 14), unaashiria mtindo sahihi wa kuandika nomino za Kiswahili katika hali ya udogo. Hii inaonyesha kuwa nomino hubadilika na kuwa kwa ngeli ya ki-vi inapoandikwa katika hali ya udogo. Ingawa hivyo, tulionyesha kuwa wanafunzi wa shule ya msingi ya CGHU na ya Moi Avenue hutumia kiambishi **ka-** kuandika nomino katika udogo. Hivyo basi, tunaweza kusema kuwa athari za Sheng' zinajitokeza kwa wanafunzi wa shule za msingi kupitia kwa kuendeleza nomino katika udogo kwa namna isiyofaa. Nomino inapoandikwa kwa namna isiyofaa basi inakuwa katika ngeli ambayo haipatikani katika Kiswahili. Kwa mfano, data ya utafiti huu 15a) na b) inabainisha kuwa nomino msichana na mtoto huwa katika ngeli ya **ka-tu** katika hali ya udogo badala ya Ki-Vi ambayo hupatikana katika Kiswahili. Tulisema hivi kwa sababu tulikumbana na insha za watafitiwa wetu ambazo zilikuwa na sentensi zifuatazo:

- 15. a) Tusichana tulikuwa tunamatch vizuri sana.** (Vijisichana vilikuwavinatembea vizuri)
- b) Tutoto tuliwekewa juice kwa kikombe ya plastiki.** (Vijitoto viliwekewa sharubati kwa vikombe vya plastiki.)
- c) Nilichimba kashimo nikaweka mahindi mbili ndani.** (Nilichimba kijishimo na kuweka punje mbili za mahindi.)

Uptanisho wa kisarufi katika mifano hii uko sawa ila hamna ngeli ya **ka-tu** katika Kiswahili. Matumizi ya kiambishi **ka-** na **tu-** katika kuandika udogo, hali ya umoja na wingi ni kosa linalosababishwa na tatizo la kumudu lugha mahsus kwa kulelewa katika mazingira ambamo lugha inatumiwa kiholela tu. Mojawapo wa mihimili ya nadharia ya umudu lugha ni kuwa wanaulumbilugha huamua lugha ipi itumike wapi na vipi. Uamuzi huu huu unaonyesha kuwa mtumizi lugha huwa na uhuru wa kuteua na kutumia lugha kwa namna fulani. Hata hivyo, wanafunzi wa shule za msingi hawapaswi kuwa na uhuru huu hasa wanapoandika insha kwa kuwa wanatakiwa kutumia lugha ya Kiswahili kwa kufuata kanuni zake. Hii inaonyesha kuwa wanafunzi walishindwa kuzingatia kanuni za uandishi za Kiswahili na badala yake kufuata zile za Sheng' ambazo hazitakiwa kutumiwa shulen. Wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue huishia kuendeleza sentensi visisvyo na hivyo basi kukosa kuzingatia ngeli za nomino wanapoandika insha hasa waliporejelea maneno katika udogo. Mnyambuliko wa vitenzi kwa namna isiyofaa pia ni athari hasi za ulumbilugha kama zinavyobainika katika insha za watafitiwa wetu kama tulivyoonyesha katika kijisehemu kifuatacho:

### **3.1.3 Mnyambuliko wa Vitenzi kwa Namna Isiyofaa**

Kiswahili ni lugha ambishi-bainishi. Hii ina maana kuwa leksemu za Kiswahili na hasa vitenzi huweza kuongezewa viambishi na hivyo basi neno husika hupata maana nyingine. Mnyambuliko wa vitenzi ni mbinu mojawapo ya uundaji wa msamiati katika Kiswahili. Mnyambuliko wa vitenzi ni hali ya kukirefusha kwa kuongezea viambishi katika mzizi wa kitenzi. Katika mnyambuliko wa vitenzi, maana mbalimbali hubainishwa ingawa mzizi wa neno haubadiliki. Kutohakani na utafiti wetu, tulibaini kuwa wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue hunyambua vitenzi kwa kufuata mtindo usiofaa katika Kiswahili. Hii ni kutohakani na athari za ulumbilugha katika mawasiliano yao hasa ikizingatiwa kuwa wanafunzi hawa hutoka kwenye mazingira ambamo Sheng' hutumiwa ikilinganishwa na Kiswahili. Nadharia ya uchanganuzi makosa inadai kuwa mtafiti anatakiwa kutambua makosa ya kimawasiliano na kuelezea makosa hayo na hasa ya kisarufi. Mnyambuliko wa vitenzi kwa namna isiyofaa huzua makosa ya kisarufi kama tulivoonyesha katika mifano ifuatavyo ya insha za wanafunzi wa shule ya msingi ya Moi Avenue na ile ya CGHU.

Katika Kiswahili kuna kauli mbalimbali kukiwemo kutenda, kutendea, kutendewa, kutendeana na kutendesha. Katika kauli ya kutenda, maneno huwakilishwa na kiambishi -a. Kauli ya kutendea huwakilishwa na viambishi tamati -e-, -i, -li na -le. Wakati wa kunyambua maneno katika kauli ya kutendewa, mwanafunzi anapaswa kutumia viambishi kama vile -ew, -liw na -lew. Katika maneno, kauli hizi hujitokeza ifuatavyo:

#### **16. Kutenda      Kutendea      Kutendewa**

Soma                somea                somewa

Shona Shonea                Shonewa

Paka                Pakia                Pakiwa

Kutohakani na mfano 16), tuliweza kusema kuwa kauli mbalimbali hunyambuliwa kwa njia maalum katika Kiswahili. Hata hivyo, tulikumbana na insha za wanafunzi ambapo maneno yalinyambuliwa visivyo. Tulibaini hili kutohakani na matumizi ya maneno husika katika muktadha wa sentensi kama ifuatavyo:

**17. a) Mhubiri alitukatizia ngoma wakati alipochukua kipasa sauti.....**

(Mhubiri alikatiza ngoma wakati alipochukua kipaza sauti.. )

**b) Baba ya bibi harusi alipatiliwa keki na bwana harusi.** (Babake bibi harusi alipewa/alipatiwa keki na bwana harusi)

**c) Rafiki yangu hunipandishia mboga na kuniletea....** (Rafiki yangu hupanda mboga ambayo huniletea...)

Katika sentensi ya 17a), hapo juu mtafitiwa anaendeleza neno *alitukatizia* kwa namna isiyofaa. Neno hili hutumiwa katika Sheng' kwa maana ya kuachisha au kumfanya mtu aache kufanya jambo fulani. Ingawa hivyo, kutokana na muktadha wa matumizi ya neno hili, mtafitiwa alikuwa na nia ya kuliandika katika kauli ya kutendesha. Katika kauli ya kutendesha, neno **kata** linapaswa kuandikwa kama **katiza** na wala sio katizia. Kiambishi -i- kimechoppekwa pasipofaa katika lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo basi, tunaweza kusema kuwa mtafitiwa ameathiriwa na Sheng' na ndiposa anatumia misamiati ya lugha hii ya vipindi anapoandika insha na hili ni jambo linalodhahirisha kuwa hajazingatia kanuni za mnyambuliko wa vitenzi katika Kiswahili. Katika sentensi ya 17b), mtafitiwa anakosea anapoandika neno *alipatiliwa*. Mtafitiwa alikuwa na nia ya kutumia kauli ya kutendewa (patiwa) ila akaliendeleza vibaya kwa kuongezea kiambishi -li- na hili linatufanya kusema kuwa ameathiriwa na Sheng'. Katika sentensi ya 17c), mtafitiwa amekiendeleza kitenzi kwa namna isiyofaa hasa ikizingatiwa kuwa alikuwa anataka kuandika katika kauli ya kutendea. Kitende, *hunipandishia* kimewekwa katika kauli ya kutendeshea ilhali, kwa mujibu wa muktadha wa matumizi ya neno hili, linalojitokeza ni hali ya kutendea. Neno sahihi ambalo linaashiria kauli ya kutendea ni *pandia* ila kutokana na athari hasi za Sheng' mtafitiwa anaongezea viambishi vya kauli ya kutendeshea. Mifano mingine, kutoka kwa insha za wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue, ambayo inaashiria mnyambuliko wa vitenzi kwa namna isiyofaa ni kama ifuatayo:

kitenzi	Matumizi yake katika insha	Kauli mnyambuliko sahihi
Tembea	Tembeleananga	Kutendeana tembeleana

Patia	patiliana	Kutendeana patiana
lima	limana	Kutendeana limiana
kata	kataniza	Kutendesha katanisha
soma	somaniwa	Kutendewa somewa

Kutokana na mifano hii, ni wazi kuwa, wanafunzi wa shule ya msingi ya CGHU na Moi Avenue, waliathiriwa na kwa njia hasi na Sheng' na ndiposa wanakosa kufuata mtindo wa uundaji wa maneno katika Kiswahili. Tuligundua kuwa, wanafunzi hawa wa shule za msingi walifuata mtindo sahili wa Sheng' katika uundaji wa maneno ya Kiswahili. Makosa yanayojitokeza hapa yanafafanuliwa katika nadharia ya uchanganuzi makosa ambapo tulionyesha kuwa visababishi vyta matumizi ya lugha kwa mtindo fulani katika mawasiliano husababishwa na mambo kama vile mazingira. Kwa upande mwingine, nadharia ya kumudu inadai kuwa umudu lugha wa jamii huathiri umudu lugha wa kibinagsi na ndio sababu wapo wanafunzi ambao wanafuata kanuni za Kiswahili wanapoandika insha ilhali wengine wanashindwa kumudu na kuishia kufanya makosa ya kimofolojia. Tulishughulikia namna watafitiwa wetu walivyoweka vitenzi kwa kauli mbalimbali bila kuzingatia mtindo wa lugha ya Kiswahili kutokana na athari hasi za Sheng'. Vile vile, tulibaini kuwa wanafunzi wa shule ya msingi ya CGHU na Moi Avenue hutohoa maneno kutoka kwa lugha ya Kiingereza. Haya ni maneno ambayo yana msamiati wake maarufu katika Kiswahili ila kutokana na kuathiriwa na Kiingereza wanajipata wakitumia utohozi hata pasipofaa kama tulivyoonyesha katika kisehemu kifuatacho:

### **3.2 Athari za Kiingereza Kimofolojia katika Uandishi wa Insha za Kiswahili**

Tulionyesha katika sehemu ya 3.1 namna wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue waliathiriwa na Sheng' katika uandishi wao wa insha za Kiswahili. Kutokana na data ya utafiti huu, tulibaini pia kuwa wanafunzi hawa waliathiriwa na Kiingereza. Makosa haya yanaangaziwa katika mhimili wa tatu wa nadharia ya kumudu kuwa wanaulumbilugha hutumia lugha kutegemea uwezekano wa kutumia lugha hiyo katika muktadha husika. Wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue hutumia lugha kwa kuzichanganya bila kuzingatia kaida za utahini wa insha za Kiswahili. Tuligundua kuwa wanafunzi wa shule za msingi za

CGHU na Moi Avenue waliswahilisha neno ambalo lina msamiati mahsus i katika Kiswahili. Vile vile, watafitiwa wetu hutumia konsonanti na maneno ya Kiingereza katika insha za Kiswahili licha ya kuwa walipewa maagizo ya kutumia Kiswahili tu. Haya ndiyo tuliyashughulikia katika visehemu vifuatavyo:

### **3.2.1 Kuswahilisha Neno Kutokana na Msamiati wa Kiingereza**

Katika sehemu hii, tulitumia dhana kuswahilisha neno kwa maana ya kutumia maneno ya Kiingereza na kuyaendeleza kwa kufuata mtindo wa Kiswahili. Hii ni athari hasi kwa kuwa wanafunzi hutumia misamiati ambayo haifai wanapoandika maneno ambayo ni maarufu kwa Kiswahili na hivyo basi kupata alama za chini ikilinganishwa na wenzao ambao hufuata maagizo. Tulibaini kuwa wanafunzi pia huchukua mzizi wa neno la Kiingereza na kuongezea viambishi awali na tamati vya Kiswahili. Hii ni athari inayotokana na ulumbilugha na hivyo wanafunzi walishindwa kuthibiti matumizi ya Kiswahili walipoandika insha. Wanafunzi walioathiriwa na Kiingereza hujipata wakiswahilisha neno ambalo lina msamiati tumizi katika Kiswahili. Hili libainika katika insha ifuatayo ya mwanafunzi wa shule ya msingi ya CGHU:

#### **18. Babangu alitubaiya nguo mzuri na kiatu na dadangu pia siku ya harusi ilipofika mimi na dadangu tulikuwa wa kwanja kuamka mapema.**

(Babangu alitununulia nguo nzuri na viatu. Siku ya arusi ilipofika, mimi na dadangu tulikuwa wakwanza kuamka.)

Katika dondo 18), la insha ya mwanafunzi wa shule ya msingi ya CGHU, tunaweza kusema kuwa ameathiriwa na Kiingereza na ndio maana alichanganya ndimi kwa kutumia neno *alitubaiya*. Mwanafunzi alitumia neno la Kiingereza *buy* ila analiswahilisha kwa kulifanya litamkike kama la Kiswahili. Ni muhimu kutaja hapa kuwa neno hili lina msamiati wa Kiswahili *nunua* na ambalo hutumiwa sana katika mawasiliano. Kwa hivyo basi, haiwezekani kuwa wanafunzi hawajui msamiati huu mwafaka ila wao hutumia maneno ya Kiingereza na kuyaswahilisha kwa sababu ya kuathiriwa kwa njia hasi na ulumbilugha. Mfano mwingine ni kutoka kwa insha za wanafunzi wa shule ya msingi ya Moi Avenue ambapo watafitiwa wanatohoa maneno ya Kiingereza na kuyaongezea viambishi vya Kiswahili kama ifuatavyo:

#### **19. a) Mwalimu alikuwa ametusetia mtihani mzuri...(mwalimu alikuwa ametahini mtihani mzuri.)**

**b) Mlinzi alikuwa ametucheki sisi na tukaambiwa tuingie harusini. (Mlinzi alikuwa ametukagua na tukaruhusiwa kuingia)**

Kutokana na mifano 19a) na b), watafitiwa waliswahilisha maneno *ametusetia* na *ametucheki*. Neno *ametusetia* limetokana na kitenzi cha Kiingereza *set*. Mtafitiwa ameliswahilisha kwa kuongezea viambishi awali **ametu-** na viambishi tamati **-ia**. Neno ametucheki limetokana na kitenzi cha Kiingereza *check* ila likaswahilishwa kwa kudondo konsonanti **c** ambayo ni ya Kiingereza na kisha kuongezea viambishi awali na tamati vya Kiswahili. Nia kuu ya kuongeza viambishi awali na tamati vya Kiswahili ni kufanya neno lifuate mtindo wa uundaji wa silabi za Kiswahili ambao huhusisha:

**20.** a) Konsonanti, vokali, kama vile neno baba ambalo lina silabi mbili- ba-ba

b) Vokali, kwa mfano ua, (u-a)

c) Konsonanti, konsonanti, vokali, kama vile mbele (mbe-le).

d) Konsonanti, kama vile maalum (ma-a-lu-m)

e) Konsonanti, konsonanti, konsonanti, vokali, kwa mfano, mbwa.

Silabi za Kiingereza hifuata mtindo wake mahususi na ndiposa tunasema kuwa wanafunzi wa shule za msingi huswahilisha neno kwa kuongeza viambishi awali na tamati vya Kiswahili. Kando na kuswahilisha neno la Kiingereza ambalo lina msamiati maarufu wa Kiswahili, tulibaini kuwa watafitiwa wakati mwingine hutumia konsonanti za Kiingereza kwa Kiswahili wanapoandika insha. Tuligundua kuwa wanafunzi wa shule ya msingi ya CGHU na Moi Avenue wakati mwingine hukanganyikiwa na kuandika konsonanti za Kiingereza badala ya zile za Kiswahili. Hali hii ndio tuliyoishughulikia katika kisehemu kifuatacho.

### **3.2.2 Matumizi ya Konsonanti za Kiingereza Katika Uandishi wa Insha za Kiswahili**

Katika lugha kuna aina mbili kuu za sauti na ambazo ni konsonanti na irabu. Kila lugha ina jinsi yake ya kuandika na kutamka sauti zake, ziwe konsonanti au irabu. Maneno ya Kiswahili hutamkwa kama yalivyoandikwa kinyume na ilivyo kwa Kiingereza ambapo maneno hutamkwa kwa upekee wake kutegemea sauti zinazoyaunda. Kila lugha ina sauti zake. Zipo sauti ambazo

hufanana na zingine hutofautiana kutoka lugha moja hadi nyingine. Kwa mfano, Kiswahili hakina konsonanti **C**, ila kuna herufi **Ch**. **C** ya Kiingereza inapotumiwa katika neno, hutamkwa kama **K** ya Kiswahili. Hii ina maana kuwa mwanafunzi anaweza kuathiriwa kiasi cha kutumia sauti za lugha fulani kwa nyingine, kwa mfano, sauti za Kiingereza kutumiwa katika uandishi wa insha. Haya tuliyabaini kutokana na data ya utafiti wetu ambapo mwanafunzi mmoja wa darasa la nane wa Shule ya msingi ya CGHU ameathiriwa na Kiingereza kiasi cha kutumia konsonanti za Kiingereza katika Kiswahili kama ifuatavyo:

**21 a) Waca vaalicana peete. Tuca cagilia, baada ya cumaliza tuca enda...**

(Wakavishana pete. Tukashangilia, baada ya kumaliza tukaenda....)

**b) Baada cumaliza harusi tuca leetew cacula na vinuaji, matunda na**

**tuca cata kaaki tu cucula zote.** (Baada ya kumaliza harusi, tukaletewa chakula na vinywaji, matunda na tukakata keki tukakula yote.)

**c) Baada ya cucula tuca amuca cuceza mziki.** (Baada ya kukula

tukaamka kucheza mziki)

Mifano 21a), b) na c), ni kutoka kwa aya tatu za mwanzo za insha ya mtafitiwa. Mtafitiwa ametumia konsonanti **C** kuandika maneno badala ya **K**. **C** ni sauti ambayo inatumia katika Kiingereza na wala haitumiki katika Kiswahili. Hata hivyo, mwanafunzi huyu ametumia sauti hiyo katika insha yake jambo ambalo linaashiria kuwa ameathiriwa na Kiingereza. Athari hii hasi inamfanya asitofautishe baina ya konsonanti **K** ya Kiswahili na **C** ya Kiingereza katika maneno kama vile *waca, cucula na amuca*. Maneno haya hayaeleweki maana hayako katika Kiswahili ila kama watafiti tunaelewa kuwa mwanafunzi alitaka kutumia **K** ya Kiswahili ila akachanganyikiwa kwa sababu pia amesoma sauti za Kiingereza. Pia, mtafitiwa anatumia sauti **C** mahali pa sauti **sh** na **ch** katika maneno *vaalicana, cagilia* na *cuceza* mtawalia. Mifano hii inadhihirisha athari hasi za ulumbilugha ambapo mtafitiwa anatumia sauti za Kiingereza anapoandika insha na kuifanya kuonekana kuwa na makosa mengi. Kutokana na makosa haya, mtafitiwa anapata alama kidogo sana kama vile 01 juu ya alama 30.

Mifano hii ya matumizi ya herufi za Kiingereza katika uandishi wa insha inaonyesha athari hasi za ulumbilugha. Mwanafunzi huyu wa shule ya msingi ya CGHU anashindwa kutofautisha baina ya herufi **K** ya Kiswahili na **C** ya Kiingereza. Mifano hii tulitoa kwenye aya ya kwanza na ya

pili kwenye insha ilio na aya sita. Mwanafunzi ametumia herufi **C** ya Kiingereza katika aya za kwanza mbili ila katika aya zinazofuatia, anatumia konsonanti **K** ya Kiswahili. Kwa mfano, katika mfano wa 21b), hapo juu, mtafitiwa anarejelea mlo waliopewa harusini kwa kutumia **C** ya Kiingereza na kuliendeleza kama *cacula*. Hata hivyo, katika aya ya tatu ya insha ii hii, mtafitiwa anatumia konsonanti **K** na **Ch** za Kiswahili ifuatavyo:

**22. a) Lakini kila kunapokosekana chakula cha kutosha nyumbani....**

**Maharusi hao wanajua kwamba mkono mzito au mkono wa birika  
haufai katika maisha ya ndoa.**

Mifano hii inaonyesha kuwa mwanafunzi huyu ameathirika tu na ulumbilugha. Tunasema hivi kwa sababu, kutokana na data kutoka kwa insha hii husika, mwanafunzi ametumia **C** badala ya **K** katika aya tatu za mwanzo, kisha aya zinazofuatia ametumia konsonanti ya Kiswahili ipasavyo. Hali hii inaashiria kuwa mtafitiwa huyu aligundua kuwa alikuwa anaandika Kiswahili na hivyo basi akaanza kutumia konsonanti za Kiswahili. Hata hivyo, mwanafunzi huyu pia inaelekea kuwa hakuwa na hakika na ndio sababu hakufanya marekebisho katika aya tatu za kwanza na hivyo basi, akaacha kwa nia ya kubahatisha tu. Kutokana na mifano ambayo tulitoa hapa ni wazi kuwa mtafitiwa alikuwa ameathiriwa na Kiingereza kwa njia hasi katika aya za kwanza tatu.

Wanafunzi wa shule ya msingi ya Moi Avenue pia walidhihirisha kuwa waliathiriwa na ulumbilugha kwa kutumia konsonanti za Kiingereza katika uandishi wao wa insha. Tuligundua kuwa wao pia walikuwa wameathiriwa na Kiingereza na hivyo basi, badala ya kutumia konsonanti **K** anatumia **C** ya Kiingereza kama inavyojitokeza katika insha ifuatayo:

**23a) Alijiunga na shule ya secondari shule ya Alayans boys.** (Alijiunga na shule yasekondari ya wavulana ya Alliance.)

**b) Nilipoenda secondarini nilika miaka mitatu secondarini na miaka wa nne nikafanya....** (Nilipojiunga na shule ya sekondari nilikaa miaka mitatu na mwaka wa nne)

Mifano 23a) na b), inaashiria athari hasi za Kiingereza katika uandishi wa maneno ya Kiswahili ambayo yana herufi k. Mtafitiwa huyu anaandika neno **secondari** kwa kuweka herufi c badala ya **k** ambayo ndio ya Kiswahili na inayopaswa kutumiwa katika uandishi wa insha. Athari hii hasi

ya Kiingereza inamfanya mtafitiwa kushindwa kutofautisha herufi ambazo anatakiwa kuzitumia anapoandika insha ya Kiswahili. Makosa haya yalishughulikiwa katika nadharia ya kumudu na ile ya uchanganuzi makosa. Nadharia ya kumudu inaonyesha kuwa mwanafunzi anayetumia sauti za Kiingereza katika Kiswahili ni kosa linalosababishwa na hali ya kushindwa kumudu lugha anazozijua. Nadharia ya uchanganuzi nayo inashughulikia chanzo cha makosa haya na kuonyesha kuwa wanafunzi waliathiriwa na mazingira alimokulia hasa ikizingatiwa kuwa wao hufunzwa masomo mengi kwa Kiingereza ikilinganishwa na Kiswahili.

Tulionyesha kuwa wanafunzi wa shule ya msingi ya CGHU na wenzao wa Moi Avenue huathiriwa na Kiingereza kiasi cha kutumia konsonanti za Kiingereza katika Kiswahili na hili huwapelekea kupata alama za chini ikilinganishwa na wenzao wanaozingatia maagizo ya uandishi wa shule kama vile kutumia Kiswahili pekee yake. Vile vile, kutokana na data ya utafiti huu tuligundua kuwa wakati mwingine watafitiwa wetu hutumia maneno ya Kiingereza wanapoandika insha. Matumizi ya maneno ya Kiingereza katika insha hayaruhisiwi na ndio sababu mojawapo ya maagizo huwa “Insha iandikwe kwa Kiswahili.” Hata hivyo tulibaini kuwa wanafunzi wa shule ya msingi ya CGHU na wenzao wa Moi Avenue waliathiriwa na Kiingereza ambacho hutumiwa kufunzia na kutahini masomo mengi ikilinganishwa na Kiswahili. Ni kutokana na athari hii ambapo watafitiwa wanaandika maneno ya Kiingereza katika insha kama tulivyoonyesha katika kisehemu kifuatacho.

### **3.2.3 Kuchanganya Ndimi katika Uandishi wa Insha**

Katika sehemu hii, dhana kuchanganya ndimi katika uandishi wa insha ina maana ya mtindo unaohusu wanafunzi kutumia maneno ya Kiingereza hapa na pale. Hii ni licha ya kuwa wanajua kuwa insha inapaswa kuandikwa kwa Kiswahili pekee yake na wala hawaruhusiwi kuchanganya ndimi. Mojawapo wa maagizo katika karatasi ya insha, kama tulivyosema awali ni ‘Tumia Kiswahili kuandika insha.’ Hii ni njia moja ya kuonyesha kuwa wanafunzi wana mazoea ya kutumia maneno kutoka kwa lugha zingine na ndiposa wanaandikiwa maagizo kwa nia ya kukumbushwa. Katika sehemu hii, tulijikita katika insha za wanafunzi wa shule ya msingi ya CGHU na ile Moi Avenue ambao walichanganya ndimi. Katika shule ya msingi ya CGHU, tulikumbana na uchanganyaji ndimi katika insha yenye mada ‘Siku ya Furaha.’

**24.“.... Tulivaa mask na tulipofika church tuliwekewa sanitizer na ndiposa tukapewa nafasi ya kuingia kanisani.”**

Katika dondo 24), mwanafunzi ametumia maneno matatu ya Kiingereza ambayo ni **mask**, **church** na **sanitizer**. Kutohana na matumizi ya maneno haya ya Kiingereza, tunaweza kusema kuwa, mwanafunzi alikosa msamiati mwafaka. Hii ndio sababu anachanganya ndimi kwa kutumia maneno ya Kiingereza anapoandika insha ilhali anajua kuwa anapaswa kutumia Kiswahili pekee yake. Vile vile, tunaweza kusema kuwa wanafunzi walitumia maneno *mask* na *sanitizer* kwa kuwa ndio msamiati unatumia na viongozi wanapozungumzia janga la virusi vya korona. Kwa hivyo, wanafunzi walitumia maneno ambayo walikuwa wakiyasikia wakati wa uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya janga la korona. Kutohana na maoni yetu, wanafunzi hawa hawachukulii kuwa wamechanganya ndimi bali wanaona kuwa walitumia msamiati sahihi na kuwafanya kurudiarudia maneno haya katika insha zao. Tunasema hivi kwa sababu tulikumbana na maneno haya mawili katika insha za wanafunzi waliokuwa wakizungumzia namna harusi ilivyokuwa ikiendeshwa wakati wa janga la korona katika uandishi wao na ni kwa sababu hii tunasema kuwa wao hawachukulii kuwa ni kosa.

Wanafunzi pia walitumia neno **Christmas** katika insha zao. Hili ni neno ambalo limetumiwa katika insha yenye mada “Siku ya Furaha.” Wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue wanatumia neno hili bila kudhahania kuwa ni kosa. Tulikumbana na neno hili katika insha za wanafunzi wote ambao walikuwa wanazungumzia sherehe za krismasi. Matumizi ya maneno ya Kiingereza katika uandishi wa insha za Kiswahili yanabainisha kuwa wanafunzi waliathiriwa na ulumbi-lugha kimofolojia. Hili linabainika katika insha ifuatayo ya wanafunzi wa shule ya msingi ya CGHU:

**25. Siku hiyo nilikuwa nimeigojea kwa hamu na gamu. Siku hiyo ilikuwa siku ya Christmas.**

Mtafitiwa huyu ametumia Kiswahili katika sentensi hizi mbili ila akatumia neno moja la Kiingereza. Mwanafunzi huyu anatumia neno la Kiingereza, *Christmas* katika insha ilhali maagizo yanasema kuwa insha iandikwe kwa Kiswahili. Matumizi ya neno hili la Kiingereza yanamfanya mwanafunzi kupata alama za chini ikilinganishwa na wenzake ambao wanatumia Kiswahili katika uandishi wao wa insha. Neno lingine la Kiingereza ambalo tulikumbana nalo

katika insha ni *wedding* na ambalo limeongezewa kiambishi awali **ku-**. Mtafitiwa wa shule ya msingi ya CGHU anatumia kitenzi cha Kiingereza katika insha yake kama ifuatavyo:

**26. .... nijitayarische tunaenda kuwend ufaransa.** (Nijitayarische tunaenda Ufaransa kwa ajili ya harusi)

Mtafitiwa anachanganya ndimi katika insha yake na hili ni jambo ambalo haliruhusiwi katika Kiswahili. Neno *wedding* lina msamiati wake wa Kiswahili na ambao unatumia sana katika mawasiliano. Hivyo ni kusema kuwa, mtafitiwa amewahi kusikia msamiati wa Kiswahili, yaani harusi, maishani mwake. Kwa hivyo basi, mwanafunzi alitakiwa kutumia msamiati wa Kiswahili badala ya kuongezea kiambishi awali ku- kwa mzizi wa neno la Kiingereza. Hii inaashiria kuwa, mtafitiwa ameathiriwa na Kiingereza na ndio maana anatumia msamiati wake anapoandika insha. Hali ya kuchanganya ndimi katika uandishi wa insha pia inajitokeza katika insha za wanafunzi wa shule ya msingi ya Moi Avenue. Watafitiwa hawa wa Moi Avenue kama wenzao wa CGHU walitakiwa kuandika insha kuhusu ‘Siku ya Furaha.’ Watafitiwa hawa pia walitumia maneno yale yale ya Kiingereza yaliyotumiwa na wanafunzi wa shule ya msingi ya CGHU kama inavyobainika katika mfano 27), ufuatao:

**27). Ni siku ya December siku ya watu kushereka na kuanza mwaka**

**inayofuata.** Ni siku ya Disemba ambapo watu hushereheke na kujitayarisha kuanza mwaka mpya)

Mtafitiwa anairejelea siku ya krismasi ambayo husherehekewa mwezi wa Disemba tarehe ishirini na tano ya kila mwaka. Wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue wanaliendeleza neno Disemba kama linavyoandikwa katika Kiingereza yaani *December*. Hii ina maana kuwa wanafunzi waliathiriwa na Kiingereza kiasi cha kushindwa kuthibiti athari zao wanapoandika insha. Athari hizi ni hasi kwa kuwa zinawafanya watafitiwa kupata alama za chini ikilinganishwa na wenzao ambao hawachanganyi ndimi wanapoandika insha. Kwa mujibu wa nadharia ya uchanganuzi makosa, makosa ya kimawasiliano yanayobainika katika sehemu hii ni ya kuchanganya ndimi. Hali ya kuchanganya ndimi katika insha za Kiswahili inasababishwa na ulumbilugha na hivyo basi, mwanafunzi anashindwa kumudu matumizi ya lugha kutegemea muktadha.

Tulishughulikia uchanganyaji ndimi katika uandishi wa insha na kuonyesha kuwa wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue hutumia baadhi ya maneno ya Kiingereza

wanapoandika insha licha ya kuwa waliagizwa kutumia Kiswahili pekee yake. Athari nyingine inayotokana na ulumbilugha ni kuongeza mofu kwa maneno ya Kiswahili visivyo kama tulivyobainisha katika kisehemu kifuatacho.

### **3.3 Uambishaji**

Kiswahili ni lugha ambishi-bainishi. Uambishaji ni mbinu mojawapo ya uundaji wa msamiati katika Kiswahili. Uambishaji huhusisha kuongeza mofu katika neno ili kupata maana nyingine. Kutohakana na data ya utafiti wetu, tulibaini kuwa wanafunzi hufanya makosa ya kimofolojia kwa kuambisha maneno ya Kiswahili visivyo. Mofu ambazo huongezwa katika maneno ya Kiswahili huleta maana tofauti na ilivyokusudiwa. Uongezeaji wa mofu katika maneno ya Kiswahili ni athari inayotokana na ulumbilugha ambapo wanafunzi huhamisha kanuni za Sheng' katika Kiswahili. Hililinajitokeza katika insha ya mwanafunzi wa shule ya msingi ya Moi Avenue na ile ya CGHU kama ifuatavyo:

**28.a) Tulika ufaransa siku machache tukaondoka tukaenda uchaina.** (Tulikaa

Ufaransa siku chache kisha tukaenda Uchina)

- b) Nilimeza funda makubwa kwa sababu sikuwa nataka kuachwa nyuma.**  
(Nilimeza funda kubwa ili nisiachwe.)
- c) Mavijana walikuwa wamejikwatua vilivyo.** (Vijana walikuwa wamejikwatua)

Kutohakana na mifano 28a),b), na c), mwanafunzi huyu ameongeza mofu kwa maneno kama vile *machache, Uchaina, makubwa na mavijana*. Katika maneno *machache*, na *makubwa*, mofu ma-haiapaswi kuandikwa kwa kuwa hivi ni vivumishi vinavyorejelea nomino siku na funda mtawalia. Katika Kiswahili, mofu ma- hutumiwa kuonyesha wingi wa ukubwa wa nomino. Ingawa hivyo, katika dondo hili, mofu hii imetumiwa kwa vivumishi katika sentensi zilizo katika hali ya wastani. Vile vile, mofu a- haipaswi kuwa kwa neno Uchina. Mofu a- hutumiwa kuonyesha wakati uliopo na kuwa kitendo kinaendelea kutendeka. Ni kwa misingi hii ambapo tunasema kuwa wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue waliathiriwa na ulumbilugha kwa njia hasi.

Tulishughulikia athari hasi za ulumbilugha kama zinavyojitokeza katika insha za wanafunzi wa shule ya msingi ya CGHU na ile ya Moi Avenue. Tulionyesha kuwa wanafunzi waliathiriwa na

Kiingereza na Sheng' hivi kwamba wanaandika visivyo katika insha na kuwafanya kupata alama za chini. Hata hivyo, tulibaini kuwa zipo athari chanya pia za ulumbilugha kwa wanafunzi wa shule ya msingi ya CGHU na Moi Avenue kama tulivyoonyesha katika kisehemu kifuatacho:

### **3.4 Athari Chanya za Ulumbilugha Kimofolojia Katika Uandishi wa Insha za Kiswahili**

Kutokana na data ya utafiti huu, tulibaini kuwa kuna athari chanya za ulumbilugha. Ingawa hivyo, athari chanya za ulumbilugha ni chache ikilinganishwa na hasi kwa wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue. Tuligundua kuwa wanafunzi wa shule hizi za msingi ni wanaulumbilugha na hivyo basi athari zake zilijitokeza katika uandishi wao wa insha. Katika sehemu hii, tulishughulikia athari chanya za ulumbilugha kama zilivyobainika katika insha za wanafunzi wa shule ya Moi Avenue na CGHU. Tulibaini kuwa athari chanya za ulumbilugha zilizojitokeza katika insha za watafitiwa wetu ni kutohoa maneno ambayo hawajui msamiati wake kwa Kiingereza na hivyo basi hawashindwi kuendeleza insha zao kwa kukosa msamiati mwafaka wa Kiswahili. Pia, tuligundua kuwa wanafunzi wa shule za msingi ambao ni wanaulumbilugha wanaelewa maana za maneno ambayo yametoholewa na kuwa wanaweza kutofautisha aina za maneno. Haya ndio tuliyaangazia katika kisehemu kifuatacho:

#### **3.4.1 Ufahamu wa Maana za Maneno**

Data ya utafiti huu ilikusanywa wakati wa janga la korona. Kwa hivyo basi wanafunzi pia walikuwa wanahamasishwa dhidi yake kiasi cha kusikia na kuona misamiati ya virusi vya korona hata shulen. Hali hii iliwafanya wanafunzi kutumia misamiati hii hata katika insha zao. Lililobainika ni kuwa ulumbilugha uliwawezesha wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue kuelewa maana ya maneno yanayohusiana na janga la korona. Kutokana na msambao wa virusi vya korona, shule zilifungwa ili kuzuia maambukizi zaidi, mwezi wa Machi, 2020. Wanafunzi walisalia nyumbani bila kuenda shulen ila wale wa darasa la nne na la nane walirudi shulen mwezi wa Oktoba. Wanafunzi hawa walikuwa wakihamasishwa namna ya kujikinga dhidi ya virusi vya korona. Wanafunzi walianza kutumia barakoa na hata mazingira ya shule yalibadilishwa kama vile kuwa na mahali pa kunawa mikono na pia kukaa umbali wa mitaa moja. Katika uhamasishaji wa Wakenya dhidi ya janga la korona misamiati ya Kiingereza ndio ilitumiwa zaidi na viongozi ikilinganishwa na ya Kiswahili. Shulen pia mabango ya kuwahamasisha wanafunzi yameandikwa kwa Kiingereza. Hata hivyo, wanafunzi walielewa na

kutumia maneno ipasavyo katika uandishi wao wa insha. Hali hii ilibainika katika mifano ya insha zifuatazo za watafitiwa:

- 29. a) Tulivaa barakoa na tukaingia gari ya bibiarusi.**
- b) Kila mtu aliambiwa avae maski yake ndio asipate korona.**
- c) Siku ya krismasi tulikaa tu nyumbani na hatukuenda hata kutembea juu ya korona.**

Katika mifano 29a), b) na c), wanafunzi walitumia maneno kwa namna ambayo inaonyesha kuwa wanajua maana zake. Maneno haya ni kama vile barakoa, maski, krismasi na korona. Maneno, *krismasi* na *korona* yametoholewa kutoka kwa Kiingereza. Wanafunzi waliyatumia ipasavyo katika insha hii ambapo walikuwa wametakiwa kuandika kuhusu ‘Siku ya Furaha.’ Maneno haya pia hayana msamiati maalum wa Kiswahili na unaoweza kujulikana na wanafunzi wa shule za msingi. Ni kwa sababu hii ambapo tunasema kuwa wanafunzi ambao ni wanaulumbilугha wanafahamu maana za maneno ambayo hutumiwa wakati fulani, yaani misimu. Katika sehemu ya 29b), mwanafunzi pia ametohoa neno maski kutoka kwa Kiingereza. Mtafitiwa ameliswahilisha neno kwa kufuata mpangilio wa silabi za Kiswahili katika neno. Hii ndio maana anaongezea irabu i mwishoni mwa neno la Kiingereza *mask*. Kwa hali hii mtafitiwa hawezi kuadhibiwa kwa kuwa ameliswahilisha neno hili ipasavyo kiasi cha kudumisha mtindo wa uandishi wa silabi za Kiswahili.

Athari chanya za ulumbilughha katika utafiti huu zinaashiria kuwa wapo wanafunzi ambao ni wanaulumbilughha walio na uwezo kumudu lugha. Kutohana na mifano iliyopo hapo juu, tunaweza kusema kuwa, katika 29)a, mwanafunzi anajua maana ya neno *barakoa* kinyume na mwenzake ambaye amelitohoa. Neno, barakoa, limetumiwa sana na wanaowahamasisha Wakenya dhidi ya janga la korona. Kwa hivyo, tunaweza kusema kuwa mtafitiwa analitumia kwa insha yake kwa kuwa anajua maana na matumizi yake kutohana na neno la Kiingereza. Hii ni athari chanya ya ulumbilughha kwa kuwa tulionyesha kuwa mwanaulumbilughha anafahamu maana za maneno hasa kwa kuwa ameyasikia katika Kiingereza na hivyo basi anaweza kutumia misamiati sawia na hiyo kwa Kiswahili katika insha. Tunasema hivi kwa sababu janga la korona lilisambaa Kenya, Machi, 2020 na ndio wakati viongozi wakiongozwa na Waziri wa Afya walichukua jukumu la kuwahamasisha Wakenya. Huu ndio wakati maneno kama vile barakoa na kieuzi yalianza kutumiwa zaidi ila yalitajwa sana kwa Kiingereza. Watafitiwa wetu ni

wanaulumbilugha na hivyo basi waliweza kuelewa maneno haya kwa lugha zote kama inavyodhihirika katika insha zao.

### **3.5 Hitimisho**

Katika sura hii, tulichanganua athari hasi na chanya za Sheng' na Kiingereza kwa Kiswahili kwa kujikita kwa mofolojia. Tulionyesha namna ambavyo wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue wanavyofanya makosa katika insha zao kutokana na athari za ulumbilugha. Athari hizi za ulumbilugha zinawafanya wanafunzi kufanya makosa kwa kushindwa kuimudu lugha ya Kiswahili kutokana na hali ya kulelewa katika mazingira ambamo usanifu wa lugha hauzingatiwi. Ingawa hivyo, tulionyesha kuwa wapo wanafunzi ambao huzingatia kanuni za uandishi wa lugha ya Kiswahili wanapoandika insha kutokana na hali ya umudu lugha wa kibinagsi. Tulionyesha kuwa katika mofolojia, wanafunzi hawa hufanya makosa kama vile: kukata silabi kwa namna isiyofaa katika Kiswahili, kubadilisha nomino katika hali ya ukubwa na udogo kwa kufuata mtindo usiofaa, kunyambua vitenzi visivyo, kuswahilisha neno ambalo lina msamiati wake kwa lugha ya Kiswahili, kuchanganya ndimi na vile vile kuambisha maneno ya Kiswahili visivyo katika uandishi wa insha. Tulionyesha kuwa wanafunzi wa shule ya CGHU na ile ya Moi Avenue hukosa kuzingatia kanuni za kukata silabi katika Kiswahili kwa kutaka kufuata mtindo sahili ambao hutumiwa na watumizi wa Sheng' kuundia leksemu zake. Hizi ni athari hasi kwa kuwa zinamfanya mwanafunzi kupata alama za chini akilinganishwa na wenzao ambao hawajaathiriwa na ulumbilugha.

Tulishughulikia pia athari chanya za ulumbilugha kama zilivyobainika katika insha za wanafunzi. Athari hii chanya ni ile ambayo huwawezesha wanafunzi ambao ni wanaulumbilugha kutofautisha maana za maneno na kuyatumia ipasavyo katika insha. Tulishughulikia maneno ambayo yalitumika zaidi wakati wa kuzungumzia janga la korona. Tulionyesha kuwa wanafunzi wa shule ya msingi ya CGHU na wenzao wa Moi Avenue waliweza kutumia maneno kama vile barakoa au maski ipasavyo. Vile vile, tulionyesha kuwa ulumbilugha uliwawezesha wanafunzi wa shule ya msingi ya CGHU na Moi Avenue kutohoa maneno na kuyatumia ipasavyo katika insha zao. Katika sura hii, tulishughulikia athari hasi na chanya za ulumbilugha kama zilivyojitekeza katika mofolojia. Hata hivyo tulibaini kuwa wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue pia waliathirika kisintaksia kama tulivyoonyesha katika sura ifuatayo.

## **SURA YA NNE**

### **ATHARI ZA KIINGEREZA NA SHENG' KISINTAKSIA KATIKA UANDIKAJIINSHA ZA KISWAHILI**

#### **4.0 Utangulizi**

Kutokana na utafiti wetu, tuligundua kuwa athari ya ulumbilugha hujitokeza kwa kila kiwango cha kiisimu na hili ni jambo ambalo huathiri tungo mbalimbali. Utafiti wetu uliangazia athari za ulumbilugha zinazojitokeza katika insha za Kiswahili za wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue. Katika sura hii, tuliangazia athari za Kiingereza na Sheng' katika sintaksia kama zinavyobainika katika insha za wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue. Kutokana na data ya utafiti wetu, tulibaini kuwa wanafunzi hufanya makosa ya kisintaksia kwa kukosa kuzingatia upatanisho wa kisarufi. Katika sura hii, dhana upatanisho wa kisarufi ina maana ya uwiano unaopatikana kati ya nomino na maneno mengine katika sentensi. Uainishaji wakisintaksia hutokana na ngeli kwa kuzingatia uhusiano wa nomino na maneno mengine katika sentensi husika ambao hurejelewa kama upatanisho wa kisarufi. Katika upatanisho wa kisarufi, mwanafunzi anapaswa kuandika kitendi kwa kutumia kiambishi kinachofungamana na ngeli ya nomino iliyio na uamilifu wa kiima katika sentensi. Kuna mwingiliano mkubwa baina ya mofolojia na sintaksia katika Kiswahili kwa kuwa hii ni lugha ambishi-bainishi. Mwingiliano huu hubainika katika upatanisho wa kisarufi ambapo nomino huwa msingi na ndio huamua viambishi vya upatanisho. Uanishaji wa nomino kisintaksia hutilia mkazo zaidi uamilifu wa maneno katika sentensi badala ya umbo la nomino husika.

Athari za ulumbilugha katika uandishi wa insha, kisintaksia hutokea pale ambapo upatanisho wa kisarufi haujazingatiwa. Katika sura hii, tulizingatia sintaksia katika insha za wanafunzi wa shule ya msingi ya CGHU na ile ya Moi Avenue. Tulijikita katika upatanisho wa kisarufi kwa kutumia nomino halisi na vile vile viambishi vya nafsi. Katika nomino halisi, tunazingatia maneno kamili huku tukishughulikia viwakilishi vya nafsi katika ngeli ya kwanza na ya pili. Tulijikita zaidi katika nadharia ya uchanganuzi makosa kwa kujikita katika hatua ya tatu inayohusu kuelezea makosa hasa yale ya kisarufi. Vile vile, nadharia ya uchanganuzi makosa hujikita katika vitengo mbalimbali vya makosa kama vile, ujumlishaji wa kiholela, kutumia sheria ambazo hazitoshelezi mahitaji ya kimawasiliano, kutozingatia kaida za lugha husika na kubuni mambo yasiyo ya kweli. Makosa mengi ya kisintaksia ambayo yalibainika katika insha za wanafunzi wa shule za

CGHU na Moi Avenue ni ya kutozingatia kaida za uandishi wa lugha ya Kiswahili kukiwemo matumizi yasiyofaa ya vivumishi, virejeshi, viunganishi na vihusishi na pia ukiushi wa viambishi upatanisho vya ngeli. Makosa haya hujitokeza kutokana na athari za ulumbilugha kama tulivyobainisha katika vijisehemu vifuatavyo tukianza na athari za Kiingereza:

#### **4.1 Athariza KiingerezaKisintaksia katika Uandishi wa Insha za Kiswahili**

Kutokana na data ya utafiti huu, tuligundua kuwa wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue waliathiriwa na Kiingereza. Wanafunzi hawa walishindwa kumudu matumizi ya lugha ya Kiswahili wanapoandika insha. Tulibaini kuwa wanafunzi waliendeleza sentensi visivyo bila kuzingatia kanuni za uundaji wake katika Kiswahili. Kwa misingi ya nadharia ya uchanganuzi makosa, makosa haya yanatokea kwa sababu ya kutozingatia kaida za lugha husika. Wanafunzi amba ni wanaulumbilugha wanatumia kaida za lugha ya Kiingereza wanapoandika insha. Kwa mfano, katika Kiingereza, sentensi huanza kwa kivumishi kiashiria ilhali Kiswahili huanza kwa nomino. Mifano katika sentensi ni kama vile:

- 1. a) The teacher is in class.** (*Mwalimu yu darasani*)
- b) That cat is big.** (*Paka huyo ni mkubwa*)

Kutokana na mfano 1a) na b), neno *the* na *that* yametumiwa mwanzoni mwa sentensi za Kiingereza ilhali nomino Mwalimu na Paka zinaanza katika Kiswahili. Hali hii huwachanganya wanafunzi na hivyo basi waohuendeleza sentensi visivyo katika insha. Wanafunzi hujipata wakiongezea viambishi au vivumishi kimakosa katika sentensi wakati wanapoandika insha za Kiswahili. Hii ndio maana tuliangazia matumizi mabaya ya viambishi vya nafsi na vivumishi kama inavyojitokeza katika insha za Kiswahili za wanafunzi wa CGHU na Moi Avenue.

##### **4.1.1 Athari za Ulumbilugha Katika Kuandika Viambishi vya Nafsi**

Viambishi vya nafsi huwa muhimu katika upatanisho wa kisarufi. Viwakilishi hivi vya nafsi hubainishwa katika ngeli za kwanza na ya pili. Katika Kiswahili nafsi huhusisha viambishi au maneno ifuatavyo katika wingi na umoja

Umoja	Wingi
-------	-------

Mimi	sisi
Wewe	nyinyi
Yeye	wao

Katika kingereza ni ifuatavyo

Singular	Plural
I	we
You	you
He/she/it	they

Maneno ambayo yanawakilisha nafsi katika sentensi na ambayo ni muhimu katika upatanisho wa kisarufi yameonyeshwa katika jedwali hapo juu. Nafsi huwa viwakilishi vya nomino na hivyo basi huwa katika ngeli ya nomino husika. Ingawa hivyo, tuligundua kuwa wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue huandika sentensi ambazo sio sahihi kisarufi kwa kukosa kuzingatia ngeli hasa katika viwakilishi nafsi vya ngeli. Katika utafiti huu, tuliangazia athari za ulumbiluga katika viambishi vya nafsi kamainavyojitokeza katika sentensi. Wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue hufanya kosa wanapotumia viambishi vya viwakilishi nafsi kwa kukosa kuzingatia ngeli ya nomino husika. Makosa haya huifanya sentensi kukosa upatanisho wa kisarufi kama inavyobainika katika sentensi zifuatazo:

**2. a).... kuku yangu kama ime taga vifaranga au kama mwewe ameyala.**

**b).... siku ya watu kusherekna kuanza mwaka inayofuata.**

**c).... chenda la ndizi na vitu zingine.**

**d) .... Mkate ilikuwa imearibika.**

Katika sentensi hizi wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue waliendeleza sentensi visivyokwa kutumia viwakilishi nafsi ambavyo havirandani na ngeli ya nomino husika. Katika mfano wa 2a), Hapo juu “.... **kuku yangu kama ime taga vifaranga au kama mwewe ameyala,**” mwanafunzi anarejelea nomino **kuku** ambayo iko katika ngeli ya A-WA. Kwa hivyo basi mwanafunzi alipaswa kutumia kiambishi nafsi **a-** katika kitenzi badala ya **i-**. Sentensi hii inapaswa kuandikwa ifuatavyo: Kuku wangu kama ameangua vifaranga na kuliwa na mwewe. Hata hivyo mwanafunzi anaandika kama kwamba anarejelea nomino iliyo katika ngeli ya I-ZI ambayo huhusisha vitu visivyokuwa na uhai kama vile kalamu, karatasi na kamusi. Kwa hivyo basi sentensi hii imekosa kuzingatia upatanisho wa kisarufi kwa kurejelea nomino kuku kama kitu kisichokuwa na uhai.

Hali ya kutumia viwakilishi nafsi kwa namna isiyofaa inajitokeza katika mfano wa 2b), mwanafunzi anaandika kuwa “.... **siku ya watu kushereka na kuanza mwaka inayofuata.**” Nomino inayorejelewa hapa ni **mwaka**. Kimsingi, nomino hii huwa katika ngeli ya U-I. Sentensi hii pia inakosa umantiki kwa kuandika kitenzi kwa namna isiyofaa. Mwanafunzi alinuia kuandika kuwa, ..... siku ya watu kusherehekeea na kuanza mwaka unaofuata. Nomino mwaka iko katika hali ya umoja na ndio maana tunasema kuwa kiwakilishi nafsi i- hakifai kwa sababu hutumiwa nomino hii inapokuwa katika hali ya wingi.

Nomino **vitu**, huwa katika ngeli ya KI-VI katika mfano 2c). Hii ina maana kuwa wakati wa kuunda sentensi, kiwakilishi nafsi katika umoja na wingi ni ki na vi mtawalia kama ifuatavyo:

**3. a) Kitu hiki kimeharibika.**

**b) Vitu hivi vimeharibika.**

Sentensi 3a) na b), zinaonyesha muwala mzuri wa maneno kutokana na hali ya kutumia viwakilishi nafsi sahihi. Hali hii ni tofauti katika insha ya mwanafunzi wa shule ya msingi ya Moi Avenue ambaye anaandika kuwa, “**chenda la ndizi na vitu zingine.**” Kiwakilishi nafsi zi-hutumiwa kurejelea nomino zilizo katika ngeli ya I-ZI Ina hili ni jambo ambalo linaifanya sentensi hii kukosa upatanisho wa kisarufi.

Katika mfano 2d), wanafunzi wa shule ya msingi ya CGHU anafanya kosa la kisarufi. Mtafitiwa anarejelea nomino mkate katika hali ya umoja ila anapoandika kiwakilishi nafsi katika kitenzi anatumia kiambishi i- ambacho hutumiwa katika hali ya wingi. Sentensi “**Mkate ilikuwa imearibika**” inakosa muoano mzuri kwa kuchanganya umoja na wingi. Katika hali ya umoja na wingi, sentensi hii ipaswa kuandikwa ifuatavyo:

**4 a) Mkate ulikuwa umeharibika.**

**b) Mikate ilikuwa imeharibika.**

Athari hii inajitokeza kwa sababu hakuna suala la ngeli katika Kiingereza. Kwa hivyo basi, wanafunzi wa ulumbilugha wanakosa kuzingatia ngeli wanapoandika insha za Kiswahili kama tulivyoonyesha hapo juu. Kutokana na data ya utafiti huu, tuligundua kuwa wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue pia hutumia vivumishi kwa namna ambayo sio sahihi katika sentensi. Kwa mujibu wa nadharia ya uchanganuzi makosa, watafitiwa wanakosa kuzingatia kaida za kuandika sentensi katika lugha ya Kiswahili. Makosa ambayo tuliyarejelea katika kisehemu hiki yanatokana na athari ya kutozingatia kaida za lugha ya Kiswahili kiasi cha kuifanya sentensi kukosa upatanisho wa kisarufi. Makosa mengine yanayotokana na kutozingatia kaida za lugha husika ni matumizi mabaya ya vivumishi. Watafitiwa hawa wanatumia vivumishi ambavyo haviambatani na nomino husika kama tulikavyoonyesha katika kisehemu kifuatacho:

#### **4.1.2 Matumizi Mabaya ya Vivumishi**

Vivumishi ni maneno ambayo huelezea zaidi kuhusu nomino katika sentensi. Vivumishi hufafanua sifa au hali ya nomino husika. Kuna aina mbalimbali ya vivumishi kukiwemo vya sifa, a- unganifu, vya pekee na vya idadi. Kwa hali hii basi, tunaweza kusema kuwa aina hizi mbalimbali za vivumishi hutumiwa kuelezea zaidi kuhusu nomino mahsus. Wakati mwingine wanafunzi hutumia vivumishi kwa namna isiyofaa katika sentensi na hili ni jambo ambalo huifanya sentensi husika kukosa upatanisho wa kisarufi. Hali hii pia husababishwa na wanafunzi kushindwa kuzingatia suala la ngeli katika sentensi. Ikumbukwe kuwa, nomino za Kiswahili zimetiwani katika matapo mbalimbali ya ngeli kutegemea sifa. Hii ndio maana nomino ambazo huwa na sifa sawa zinatiwa katika kundi moja la ngeli. Mathalan, viumbe vyenye uhai huwa katika ngeli ya A-WA, kwa mfano, chura, siafu na hata kijakazi. Hii ina maana kuwa, sio lazima kwa nomino zinazoanza kwa ki na vi katika umoja na wingi mtawalia kuwekwa kwenye ngeli ya

KI-VI. Mtafitiwa basi anapaswa kuwa makini anapotunga sentensi ili kutumia kivumishi ambacho kitaambatana na nomino husika.Haya ndio tulikayoyashughulikia katika kisehemu hiki ambapo tuliangazia vivumishi vya sifa, vionyeshi na vya idadi mionganoni mwa vivumishi vingine.

#### **4.1.2.1 Matumizi Mabaya ya Vivumishi vya –a-unganifu**

Vivumishi vya –a unganifu huundwa kwa kiambishi tamati –a, kama vile la, cha, vya na wa. Kivumishi cha a-unganifu huwa cha uhusiano na huambatanishwa kwenye viambishi vya ngeli ili kuleta maana inayokusudiwa. Mfano katika sentensi ni:

- 5. a) Tunda la mwembe huu ni tamu.** (umoja)
- Matunda ya miembe hii ni matamu.** (wingi)
- b) Chakula cha jioni kimeandaliwa.** (umoja)
- Vyakula vya jioni vimeandaliwa.** (wingi)

Katika mifano 5a) na b), mtawalia,**la** na **cha** ni vivumishi vya a-unganifu katika umoja hukuya na vya vikionyesha hali ya wingi. Vivumishi hivi vimetumiwa ipasavyo na ndio maana sentensi hii ni sahihi kisarufi na hata kimantiki. Katika mfano huu, vivumishi vya a-unganifu **nila** katika hali ya umoja na **ya** kwa wingi. Katika sentensi hizi, upatanisho wa kisarufi ulizingatiwa katika umoja na wingi. Hali hii ni tofauti katika insha za wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na ile ya Moi Avenue.Kutokana na data ya utafiti huu, tulibaini kuwa wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue hutumia vivumishi vya a-unganifu pasipostahili katika sentensi kama ifuatavyo katika insha yenye mada ‘Mnyama Nimpendaye.’

- 6. a) Mbuzi wangu ni mkubwa sana. ana rangi ya nyeupe.** (Mbuzi wangu mweupe nimkubwa sana.)
- b) Mwewe hula vifaranga vya kaka.** (Mwewe hula vifaranga wa kaka)
- c) Kuna paka ya ndume na ya kike.** (Kuna paka ndume na wa kike pia)
- d)..... ye ye yuko katika gredi la nne.** (...yuko katika gredi ya nne)
- e) Shule yetu tuna va mavazi ya rangi ya nyeupe.**  
(Shulenii mwetu tunavaa mavazi yarangi nyeupe.)

Kutokana na mifano 6), tunaweza kusema kuwa wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue hutumia vivumishi vya a-unganifu visivyo au pasipofaa. Wanafunzi wa darasa la tano walitakiwa kuandika insha kuhusu Mnyama Nimpendaye. Tulibaini kuwa, watafitiwa wetu walitia vivumishi vya a-unganifu pasipofaa au kuvitumia visivyo na hivyo basi kupotoka katika upatanisho wa kisarufi. Katika shule ya msingi ya CGHU tulikumbana na matumizi ya vivumishi vya a-unganifu katika mfano 6a), “**Mbuzi wangu ni mkubwa sana. ana rangi ya nyeupe.**” Katika sentensi hii, mtafitiwa alitumia kivumishi **ya** mahali pasipofaa. Neno **nyeupe** ni kivumishi cha sifa ambacho kinaweza kutumiwa peke yake katika sentensi. Kwa hivyo basi, sio sahihi kuongeza kivumishi cha a-unganifu kama alivyofanya mtafitiwa huyu. Hali hii pia ilibainika katika sehemu ya 6e), ambapo mwanafunzi anapachika kivumishi **ya** pasipofaa. Katika sentensi yake, mtafitiwa anaandika kuwa “**Shule yetu tuna va mavazi ya rangi ya nyeupe.**” Kivumishi **ya** baina ya neno rangi na nyeupe hakifai kuwepo katika sentensi hii. Hii ni kwa sababu neno **nyeupe** ni kivumishi cha sifa na hivyo basi haina haja ya kutumia kivumishi cha a-unganifu katika sentensi moja.

Katika sehemu ya 6b), mtafitiwa ametumia kivumishi cha a-unganifu kisichofaa katika sentensi. Mwanafunzi wa shule ya msingi ya Moi Avenue anakosea kwa kutumia kivumishi **vy**a anapoandika kuwa “**Mwewe hula vifaranga vy a kaka.**” Kivumishi **vy**a katika sentensi hii inaifanya kuwa sio sahihi kisarufi. Tunasema hivi kwa sababu nomino vifaranga imo katika ngeli ya A-WA na hivyo basi kivumishi mwafaka cha a-unganifu ni **wa**. Hali hii inaonyesha kuwa mtafitiwa ameathiriwa na Kiingereza ambacho hakina muundo wa ngeli katika nomino zake. Kutokana na athari hii basi, mtafitiwa anakosa kufuata kanuni za uandishi wa sentensi za Kiswahili na hili ni jambo ambalo huwafanya kupata alama za chini.

Athari nyingine ya Kiingereza inajitokeza katika sehemu ya 6c), ambapo mtafitiwa anatumia kivumishi **ya** katika sentensi ambayo nomino yake imo kwenye ngeli ya A-WA. Hili linadhihirika anapoandika kuwa “**Kuna paka ya ndume na ya kike.**” Kivumishi sahihi cha a-unganifu katika sentensi hii niwakwa kuwa paka ni kiumbe mwenye uhai. Ingawa hivyo, mwanafunzi huyu washule ya msingi ya CGHU anatumia kivumishi **ya** ambacho hulusishwa na vitu visivyokuwa na uhai kama vile shuka na sehemu za mwili kukiwemo macho, mabega na masikio. Makosa ya kisarufi yanayojitokeza katika data tulioishughulikia katika kisehemu hiki yanarejelewa kama ujumlishaji wa kiholela katika nadharia ya uchanganuzi makosa. Ujumlishaji

wa kiholela katika utafiti huu unajitokeza pale ambapo watafitiwa wanatumia vivumishi ambavyo havioani na maneno mengine katika sentensi na kuifanya kukosa upatanisho wa kisarufi. Makosa haya yanababishwa na athari za Kiingereza ambacho kinafuata mtindo fulani amba ni tofauti na ule wa Kiswahili katika uandishi wa sentensi.

Tulionyesha kuwa watafitiwa hutumia vivumishi vya a-unganifu hata pasipofaa na kuifanya sentensi kukosa muwala mzuri. Hii ni athari inayotokana na ulumbilugha na hasa kwa wanafunzi amba wanafunzwa masomo mengi kwa Kiingereza. Nadharia ya kumudu inaashiria kuwa watu huzungumza au kuandika kutegemea na hali na mazingira wanamokulia. Wanafunzi waliathiriwa na Kiingereza kiasi cha kufuata mtindo wake wa uandishi wanapoandika insha za Kiswahili kwa kushindwa kumudu lugha wazijuazo. Hali ya kushindwa kumudu lugha azijuazo mtu husababishwa na mazingira ambayo huathiri tabia za watu. Athari hii inawafanya wanafunzi kufuata mtindo wa uundaji wa sentensi za Kiingereza katika insha za Kiswahili. Vile vile tulitambua kuwa watafitiwa wetu hutumia vivumishi vionyeshi visivyoambatana na nomino iliyotumiwa katika sentensi kama inavyodhahirika katika kisehemu kifuatacho:

#### **4.1.2.2 Matumizi Mabaya ya Vivumishi Vionyeshi**

Vivumishi vionyeshi ni kiashiria cha kudhihirisha kitu au mtu aliyekaribu, mbali kidogo na mbali sana. Vivumishi vionyeshi vya karibu huwa kama vile: huyu, hiki, hili na hii. Vivumishi vionyeshi vya mbali kidogo huhusisha maneno kama vile, huyo, hicho, hilo na hiyo. Vivumishi vionyeshi vya mbali sana huwa ni yule, kile, lile na ile. Vivumishi hivi hutumiwa katika sentensi ifuatavyo:

7.a) Mtoto huyu ni mgonjwa.

Mtoto huyo ni mgonjwa.

Mtoto yule ni mgonjwa

b) Kiatu hiki kimeshonwa.

Kiatu hicho kimeshonwa.

Kiatu kile kimeshonwa.

Mifano 7a) na b), inaonyesha matumizi sahihi ya vivumishi vionyeshi. Hali hii ni tofauti katika insha za watafitiwa amba wanaendeleza sentensi kwa kutumia vivumishi vionyeshi vibaya.

Kutokana na data ya utafiti huu tulibaini kuwa wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue waliathiriwa na ulumbilugha kiasi cha kutumia vivumishi viashiria bila kuzingatia sarufi katika sentensi. Sentensi zifuatazo kutoka insha za watafitiwa wa shule ya msingi ya Moi Avenue na CGHU inadhihirisha matumizi mabaya ya vivumishi vionyeshi kutokana na athari za ulumbilugha:

**8 a) .....Bila kupoteza wakati gari liliuja. Ndani ya huyo gari kulikuwa na jitu linaloitwa Musa.**

**b) Paka hicho hupenda kukaa juu ya kiti.**

**c) Chakula hivyo kilikuwa vitamu.**

Sentensi 8a,b b nac, ni mifano ya athari za ulumbilugha ambapo watafitiwa wanakosa kutilia maanani suala la upatanisho wa kisarufi katika Kiswahili. Katika sentensi ya 8a) mtafitiwa anarejelea gari kama kiumbe mwenye uhai. Anasema kuwa “**Ndani ya huyo gari kulikuwa na jitu linaloitwa Musa.**” Kivumishi kiashiria katika sentensi hii ni **huyo**. Kivumishi hiki hutumiwa kurejelea binadamu kama vile *mtoto huyo ametibiwa*. Kwa hivyo basi, kutumia kivumishi **huyo** kuashiria gari sio sahihi katika sentensi. Tunaweza kusema kuwa hii ni athari inayotokana na Kiingereza ambapo kivumishi *that* hutumika kurejelea vitu na pia viumbe wenye uhai. Kwa mfano:

**9 a) She is inside that car.**

**b) That girl is pretty.**

Kutokana na mifano 9a) na b), neno **that** limetumika kuashiria gari na vile vile msichana. Hali hii ndio huwaathiri wanafunzi ambao ni wanaulumbilugha. Kutokana na athari hii, watafitiwa wanakosa kuelewa kuwa kila lugha ina upekee wake hasa katika uuundaji wa sentensi. Hii ndio maana mwanafunzi anatumia kivumishi **huyo** kurejelea gari. Athari hii ya Kiingereza ndio inamfanya mwanafunzi kutumia kivumishi **hicho** kuashiria paka katika sentensi ya 8.b), Kivumishi **hichohutumiwa** kuashiria vitu visisvyokuwa na uhai kama vile *kitabu hicho ni changu*. Ni kwa misingi hii ambapo tunasema kuwa sentensi, “**Paka hicho hupenda kukaa juu ya kiti**” sio sahihi kisarufi. Paka ni kiumbe mwenye uhai na hivyo basi huwa katika. ngeli ya A-WA. Vivumishi viashiria vya viumbe wenye uhai huwa ni **huyu, huyo** na **Yule**. Sentensi hii basi ilitakiwa kuwa *paka huyo hupenda kukaa juu ya kiti*.

Katika sentensi 8c), mtafitiwa anatumia kivumishi **hivyo** kuashiria nomino chakula. Kivumishi hiki hutumiwa kurejelea nomino chakula katika wingi. Hivyo basi sentensi “**Chakula hivyo kilikuwa vitamu**” sio sahihi kwa sababu mwanafunzi amechanganya umoja na wingi katika sentensi moja. Nomino chakula iko katika hali ya umoja na hivyo basi kivumishi kiashiria kilipaswa kuwa hicho badala ya hivyo. Kivumishi hivyo hutumiwa kuashiria vyakula. Hivyo basi, sentensi sahihi ilipaswa kuwa *chakula hicho kilikuwa kitamu*. Makosa ya kisarufi yaliyofanywa katika kisehemu hiki yalishughulikiwa na nadharia ya uchanganuzi makosa katika kitengo cha kutozingatia kaida za lugha ya Kiswahili. Kosa la kutozingatia kanuni za uundaji wa sentensi katika uandishi wa insha ni athari hasi inayotokana na ulumbilugha ambapo watafitiwa waliathiriwa na Kiingereza kiasi cha kuwafanya kufuata mtindo wake wa uandishi wa sentensi.

Katika utafiti huu, tulishughulikia matumizi mabaya ya vivumishi viashiria na kusema kuwa wanafunzi wanakosa kuzingatia suala la ngeli wanapovitumia. Tulionyesha kuwa wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue walitumia vivumishi viashiria bila kuzingatia nomino katika sentensi. Hali hii inatokana na athari ya Kiingereza kama tulivyoonyesha katika kisehemu hiki. Tulikwisha kusema kuwa Kiingereza hakina suala la ngeli na hivyo basi wanafunzi amba ni wanaulumbilugha wanashindwa kuzingatia upekee wa lugha ya Kiswahili na hivyo kushindwa kumudu lugha wanazozijua. Hili huwafanya kuishia kutunga sentensi ambazo sio sahihi kisarufi na hata kimantiki. Vile vile, tulibaini kuwa wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue hutumia vivumishi vimilikishi visivyo kama tulikavyoonyesha katika kisehemu kifuatacho:

#### **4.1.2.3 Matumizi Mabaya ya Vivumishi Vimilikishi**

Katika kisehemu hiki, tulishughulikia vivumishi vimilikishi kama vilivyojitokeza katika insha za wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue. Vivumishi vimilikishi hutoa dhana ya kuwa na. Hii ni hali ya kumiliki kitu na huwa na mzizi: **-angu, -ake, -ako, -ao, -enu** na **-etu**. Mizizi hii huambishwa katika viambishi vya ngeli kutegemea nomino husika ili kuwa sahihi kisarufi na vile vile kimantiki. Kwa mfano, *kiatu chake kimeshonwa*. Neno **chake** ni kivumishi kimilikishi kinachovumisha nomino **kiatu**. Wingi wa sentensi hii ni, *viatu vyao vimeshonwa*. Sentensi hizi zina vivumishi vimilikishi na ambavyo vimetumika kwa namna inayofaa. Katika sentensi hizi, vivumishi vimeendelezwa ipasavyo kwa kuongezewa viambishi awali vinavyooana na nomino kiatu katika umoja na wingi.

Data ya utafiti huu ilionyesha kuwa wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue wakati mwingine hutumia vivumishi vimilikishi kwa namna isiyooana na nomino husika. Matumizi mabaya ya vivumishi hutokea wakati ambapo wanafunzi wanaongezea viambishi kwa mzizi bila kuzingatia ngeli inayoambatana na nomino inayorejelewa katika sentensi. Kwa mujibu wa nadharia ya uchanganuzi makosa, wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue wanatumia sheria ambazo hazitoshelezi mahitaji ya kimawasiliano katika lugha ya Kiswahili wanapoandika insha. Makosa yanayojitokeza katika sentensi za watafitiwa yanababishwa na athari hasi za ulumbilugha na hili ni jambo linaloshughulikiwa katika nadharia ya kumudu inayoonyesha kuwa tatizo linatokana na mazingira anamolelewa mtu. Wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue waliathiriwa na Kiingereza kiasi cha kuwafanya kuandika sentensi kwa kutumia vivumishi vimilikishi visivyofaa kama inavyodhahirika katika mifano ifuatayo:

**10. a) Ng'ombe yangu huenda kukula pekeake.**

**b) Yeye huishi katika nyumba chake.**

**c) Sungura yake ilikuwa imepotea kichakani.**

Katika sentensi hizi, watafitiwa walitumia vivumishi visivyoendana na nomino husika. Vivumishi hivi ni yangu, chake na yake. Sentensi 10a), yaani “**Ng'ombe yangu huenda kukula pekeake**,” na “**Sungura yake ilikuwa imepotea kichakani**” watafitiwa walitumia vivumishi vimilikishi **yanguna yake** kurejelea nomino **ng'ombena sungura** mtawalia. Hili ni kosa kwa kuwa ng'ombe na sungura ni viumbe hai na hivyo huwa katika ngeli ya A-WA. Kwa hivyo basi, sentensi sahihi ilipaswa kuwa *Ng'ombe wangu huenda kula peke yake* na *Sungura wake alikuwa amepotea kichakani*. Hali hii inasababishwa na athari za ulumbilugha na hasa wanafunzi wanaofunzwa masomo mengi kwa Kiingereza ikilinganishwa na Kiswahili. Kutokana na mifano hii, wanafunzi walifuata kanuni za uundaji wa sentensi za lugha ya Kiingereza.

Matumizi mabaya ya vivumishi vimilikishi pia yanajitokeza katika sentensi ya 10b), mtafitiwa ameandika kuwa “**Yeye huishi katika nyumba chake**.” Nomino nyumba huwa katika ngeli ya I-ZI. Kwa hivyo basi, kivumishi kimilikishi mwafaka niyake na wala sio *chake*. Hii ndio sababu tunasema kuwa sentensi hii sio kamilifu kisarufi. Mtafitiwa anakosa kuzingatia mwingiliano wa maneno katika sentensi kwa kuangazia nomino nyumba na kivumishi kimilikishi mwafaka

kutokana na athari hasi za ulumbilugha. Sentensi sahihi inapaswa kuwa *Yeye huishi kwa nyumba yake*. Sentensi hii imezingatia upatanisho wa kisarufi kwa kutumia kivumishi kimilikishi mwafaka. Matumizi mabaya ya vivumishi vimilikishi yanababishwa na ukweli kuwa Kiingereza hakina suala la ngeli na hivyo basi, wanafunzi hujipata wakifanya makosa katika Kiswahili kwa kukosa kuzingatia upekee wake. Wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue wanakosa kufuata matumizi yafaayo ya vivumishi vimilikishi kutokana na athari ya ulumbilugha na hivyo kushindwa kumudu lugha ya Kiswahili. Athari hii hasi ya kushindwa kumudu lugha ya Kiswahili inabainika pia katika matumizi ya vivumishi virejeshi kama tulivyoonyesha katika kisehemu kifuatacho:

#### **4.1.2.4 Matumizi Mabaya ya Vivumishi Virejeshi**

Virejeshi hutumiwa kurejelea nomino husika na ambayo tayari imetajwa na hivyo inafahamika. Umuhimu wa kirejeshi ni kurudisha fikra za msomaji kwenye mtu au kitu kilichotajwa awali. Ni kwa misingi hii ambapo tunasema kuwa matumizi ya vivumishi virejeshi katika sentensi hupaswa kuendana na nomino husika. Mtafitiwa anapaswa kutumia kirejeshi ambacho kinaingiliana na nomino inayorejelewa na hili ni jambo ambalo litapelekea kuwepo kwa upatanisho wa kisarufi katika sentensi. Kwa mfano:

- a) Kiatu ambacho kimeraruka kimeshonwa.**
- b) Viatu ambavyo vimeraruka vimeshonwa.**
- c) Mwanafunzi apewaye zawadi hufurahia.**
- d) Wanafunzi wapewao zawadi hufurahia.**

Mifano 11a), b), c) na d), ni sentensi ambazo zina virejeshi mwafaka na ambavyo vinaingiliana na nomino inayorejelewa. Sentensi hizi ziko katika hali ya umoja na wingi na kinachobainika ni kuwa virejeshi hubadilika kutegemea hali ya sentensi na vile vile kutegemea nomino husika. Katika mifano hii, upatanisho wa kisarufi ulizingatiwa kwa kutumia vivumishi virejeshi vinavyooana na nomino husika. Hata hivyo, kutokana na data ya utafiti huu, tulibaini kuwa wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue hukosa kuzingatia upatanisho wa kisarufi kwa kutumia vivumishi virejeshi visivyoingiliana na nomino mahsusni katika sentensi. Athari hii hasi inasababishwa na ulumbilugha na kuwafanya wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue kufanya makosa katika sentensi. Makosa yanayojitokeza katika sentensi

yanaashiria kuwa watafitiwa wanajumlisha maneno kiholela kama inavyoshughulikiwa katika nadharia ya uchanganuzi makosa. Athari hizi hasi huwafanya kufuata mtindo wa uundaji wa sentensi wa lugha nyingine bila kuzingatia kuwa kila lugha ina upekee wake. Hili linabainika katika sentensi zifuatazo za watafitiwa wetu:

- 12. a) Bosko anameno ambazo ye ye huzitumia kuuma nyama au mutu.**
- b) **Mimi huletea ng'ombe wangu maji akisha malinza kukula vyakula abanzo nilimletea...**
- c) **Siku ya Jumamosi ambapo nilizaliwa huwa mzuri sana.**
- d) **Watu wa kijiji cha matopeni walikula chakula ambayo ni ya jioni pekeake.**
- e) **Watoto waingiaye mtoni hupotea kabisa.**
- f) **Mamangu ananiambianga kuwa kiatu kipakwayo rangi huonekana kipyä.**

Makosa yanayojitokeza katika sentensi hizi yanahusu uchopekaji na pia udondoshaji wa sauti pasipofaa ila tulijikita kwa sintaksia. Ni kwa misingi hii ambapo tunashughulikia maneno ambayo yameendelezwa vibaya au kutumiwa pasipofaa na kuifanya sentensi kukosa upatanisho wa kisarufi. Mifano hii kutoka kwa insha za watafitiwa wetu amba ni wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue. Watafitiwa walitumia vivumishi virejeshi bila kuzingatia nomino inayorejelewa katika sentensi husikana kuifanya sentensi husika kukosa umantiki. Hii ndio inapelekea sentensi hizi kukosa usarufi na umantiki kwa kuwa maneno katika sentensi yanakosa kurandana na hivyo basi kuishia kuwa na makosa ambayo huwafanya wanafunzi wa shule za msingi kuadhibiwa kwa kutolewa alama.

Katika sentensi ya 12a), na b), watafitiwa walitumia kivumishi kirejeshi ambazo pasipofaa kama ifuatavyo: **Bosko anameno ambazo ye ye huzitumia kuuma nyama au mutu** na **Mimi huletea ng'ombe wangu maji akisha malinza kukula vyakula abanzo nilimletea....** Katika sentensi ya 12a), mtafitiwa anarejelea nomino **meno** iliyo kwenye ngeli ya LI-YA. Kwa hivyo basi, kivumishi kirejeshi mwafaka ni **ambalo** katika umoja na **ambayo** katika hali ya wingi. Mtafitiwa anatumia nomino meno iliyo katika hali ya wingi na hivyo sentensi sahihi inapaswa kuwa *Bosko ana meno ambayo huyatumia kuuma nyama au mtu*. Sentensi 12b), mtafitiwa anarejelea nomino **vyakula** ambayo iko katika hali ya wingi. Mtafitiwa anakosa kuoanisha nomino na vivumishi

pamoja na maneno mengine katika sentensi na kuifanya kukosa upatanisho wa kisarufi. Kwa hivyo basi, mtafitiwa alipaswa kuandika kuwa ..... **vyakula ambavyo nilimletea**. Sentensi hii ni sahihi kwa kuwa imezingatia hali ya wingi ya nomino.

Kosa hilo hilo linajitokeza katika sentensi ya 12d), ambapo mtafitiwa anarejelea nomino **chakula** katika hali ya umoja ila anatumia kivumishi kirejeshi kisichoingiliana na nomino. Mtafitiwa anaandika kuwa, **Watu wa kijiji cha matopeni walikula chakula ambayo ni ya jioni pekeake**. Matumizi ya kivumishi kirejeshi *ambayo* kurejelea nomino **chakulani** kosa kwa kuwa hamna urari unaofaa katika sentensi hii. Mwanafunzi huyu anadhihirisha kuwa ameathiriwa na ulumbiluga na hasa kwa kuwa anafunzwa masomo mengi kwa Kiingereza ikilinganishwa na Kiswahili. Tulionyesha awali kuwa lugha ya Kiingereza haina suala la ngeli na hivyo nomino hurejelewa na *kiashiriathat* hutumiwa kurejelea nomino zote. Hali hii ni tofauti katika lugha ya Kiswahili ambapo ngeli ya nomino huzingatiwa katika uundaji wa sentensi. Athari hii ndio inayoshuhudiwa pia katika sentensi ya 12c), mtafitiwa anapotumia kivumishi kirejeshi amba- visivyo anapoandika kuwa **Siku ya Jumamosi ambapo nilizaliwa huwa mzuri sana**. Nonimo Jumamosi haioani na kirejeshi **ambapo** na hivyo basi sentensi hii sio sahihi kisarufi. Sentensi yenyewe inakosa umantiki kwa kuwa mtafitiwa anakosa kuzingatia ngeli ya nomino Jumamosi. Sentensi sahihi inapaswa kuwa *Nilizaliwa siku ya Jumamosi ambayo huwa nzuri sana*.

Kutokana na mifano iliyopo hapo juu tulibaini pia kuwa wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue hutumia kirejeshi –O- visivyo. Hili linadhihirika katika sentensi za 13a) na b), kama ifuatavyo:

**13. a) Watoto waingiye mtoni hypotea kabisa.** (Watoto waingao mtoni hypotea kabisa)

**b) Mamangu ananiambianga kuwa kiatu kipakwayo rangi huonekana kipyga.**(Mamangu huniambia kuwa kiatu kipakwacho rangi huonekana kipyga)

Katika sentensi **13a**), nomino watoto iko kwa wingi ila kirejeshi kilichotumiwa hurejelea neno mtoto iliyo katika umoja. Hii ndio maana tunasema kuwa mtafitiwa anachanganya halikwa nomino na kivumishi kirejeshi na hili ni jambo ambalo linaifanya sentensi hii kuwa na kosa kisarufi. Kasoro ya upatanisho wa kisarufi unasababishwa na kuchanganya hali ya wingi na

umoja kwa nomino na kivumishi chake katika sentensi moja. Athari hii inatokana na Kiingereza ambapo hamna tofauti inayojitokeza kwa kitenzi wakati wa kuandika sentensi hii hii katika umoja na wingi kama ifuatavyo:

**14.a) The child that enters in the river gets lost.** (Mtoto aingiaye mtoni  
hypotea)

**b) The children that enters in the river gets lost.** (Watoto waingiao  
mtoni hypotea)

Katika sentensi 14a) na b), kitenzi *nienters* katika hali ya umoja na vile vile wingi. Hali hii ni tofauti katika lugha ya Kiswahili kama tulivoonyesha kwenye mabano ambapo vitenzi, aingiaye na waingiao vinajitokeza katika hali ya umoja na wingi mtawalia. Muundo wa kirejeshi – Ounabadilika katika hali ya umoja na wingi katika lugha ya Kiswahili. Uundaji wa sentensi katika lugha ya Kiingereza ni tofauti na kanuni za uundaji wa sentensi katika lugha ya Kiswahili kama ambavyo tulionyesha na ndio sababu tunasema kuwa wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue waliathiriwa na ulumbilugha kama inavyobainika kutokana na uandishi wao wa insha.

Athari hii hasi ya Kiingereza kwa Kiswahili inadhihirika piakatika sentensi ya 13b) mtafitiwa anapokosa kuoanisha nomino **kiatu** na kirejeshi chake. Kirejeshi –O kimeendelezwa vibaya mtafitiwa anapoandika kuwa “...**kiatu kipakwayo rangi....**” Nomino kiatu iko katika ngeli ya KI-VI na hivyo basi sentensi sahihi inapaswa kuwa *mama huniambia kuwa kiatu kipakwacho rangi huonekana kipyä*. Kiambishi –**cho** ndicho mwafaka kwa nomino kiatu na wala sio –**yo**. Ni kwa misingi hii ambapo tunasema kuwa wanafunzi wa shule za msingi na ambao ni wanaulumbilugha hubainisha athari zake hasi wanapoandika insha.

Katika kisehemu hiki, tulishughulikia matumizi mabaya ya vivumishi virejeshi kama inavyobainika katika uandishi wa insha za wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue. Nadharia ya uchanganuzi makosa inabainisha kuwa makosa ya kijumla huwa katika vitengo kama vile ujumlishaji wa kiholela, kutumia sheria ambazo hazitoshelezi mahitaji wa kimawasiliano ya lugha husika, kutozingatia kaida za lugha husika na kubuni mambo yasiyo ya kweli. Vitengo hivi vyote vya dosari za kijumla vinajitokeza katika insha za Kiswahili za watafitiwa wetu na ndio maana wanatumia vivumishi kwa namna isiyofaa katika sentensi zao. Tulionyesha kuwa watafitiwa wetu walishindwa kuoanisha nomino na kivumishi kirejeshi katika

sentensi na kuifanya kukosa upatanisho wa kisarufi. Vile vile, kutokana na data ya utafiti huu, tulibaini kuwa watafifiwa wetu wanatumia vivumishi vya idadi visivyo katika sentensi kutokana na kuathiriwa na lugha ya Kiingereza kama tulivyoonyesha katika kisehemu kifuatacho:

#### **4.1.2.5 Matumizi Mabaya ya Vivumishi vya Idadi**

Kutokana na data ya utafiti wetu, tulibaini kuwa makosa katika upatanisho wa kisarufi hujitokeza kwa kila kiwango na hasa katika vivumishi vinavyovumisha nomino husika. Kwa hivyo basi, sio vyema kuyapuuza kwa kuwa huathiri uandishi wa insha kiasi cha kuwfanya wanafunzi wa shule za msingi kupata alama za chini ikilinganishwa na wenzao ambaو wanazingatia mitindo ya uandishi ifaayo katika lugha ya Kiswahili. Vivumishi vya idadi huashiria kiasi cha nomino. Kuna aina mbili za vivumishi vya idadi: idadi maalum/inayodhihirika na idadi isiyodhihirika. Idadi maalum huonyesha idadi kamili ya vitu au watu kama vile watatu, wanne, vitano na sita. Idadi isiyodhihirika huwakilishwa namaneno kama vile wachache au wengi. Katika lugha ya Kiswahili, vivumishi vya idadi pia huendelezwa kutegemea nomino husika katika sentensi. Hali hii ni tofauti katika lugha ya Kiingereza na ndiposa wanafunzi ambaو ni wanaulumbilugha wanakosa kuendeleza vivumishi vya idadi ipasavyo kutegemea nomino katika sentensi. Data ya utafiti huu imeonyesha kuwa wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue hukosa kuoanisha vivumishi vya idadi na nomino wanapoandika insha kama inavyobainika katika sentensi zifuatazo kutoka kwa insha zao.

**15. a) nikona paka mbili.** (Nina paka wawili)

**b) Kwetu tuko vijana wawili na tuko na sungura wasita.** (... tuna sungura sita).

**c) Nilitumia misitari muchache sana kuchora mbuzi wetu wa white.**  
(Nilitumia misitari michache sana kuchora mbuzi wetu mweupe.)

**d) Watoto wakumi ndio walismamia hiyo harus.** (Watoto kumi ndio walismamia hiyo harus.)

**e) Kila mtu aliwekewa chakula mdogo mdogo tu katika arusi iyo.**(Kila mtu aliwekewa chakula kidogo kidogo katika arusi hiyo.)

Kutokana na sentensi hizi, watafitiwa waliendeleza vivumishi vya idadi maalum visivyo katika 15a), b), na d). Nomino paka, sungura na vijana huwa katika ngeli ya A-WA na hivyo basi, wanafunzi wanapaswa kuzingatia hili wanapoandika sentensi katika insha zao. Katika sentensi ya 15a) mtafitiwa anakosa kuzingatia upatanisho wa kisarufi anapoandika kuwa "**nikona paka mbili.**" Kivumishi cha idadi *mbili* hakifai kutumiwa pamoja na nomino paka. Hii ni kwa sababu kivumishi hiki cha idadi (*mbili*) aghalabu hutumiwa pamoja na nomino zilizo katika ngeli ya I-ZI kama vile karatasi *mbili* zimetolewa. Kwa hali hii basi, mtafitiwa alifanya kosa anapotumia kivumsihi hiki pamoja na nomino zilizo katika ngeli ya A-WA .Sentensi yastahili kuwa: Nina paka wawili. Katika sentensi 15b), na d), watafitiwa wanakosea anapoongeza kiambishi **wa-** katika kivumishi cha idadi maalum wanapoandika kuwa "**....tuko na sungura wasita.**" na "**Watoto wakumi ndio.....**" Watafitiwa wanabainisha kuwa waliathiriwa na ulumbilugha na ndio maana wanaongezea viambishi awali katika vivumishi tasa visivyofaa kuongezewa viambishi vyovyyote.

Sentensi 15c), na e), pia zinathihirisha athari hasi za ulumbilugha katika mifano iliyopo hapo juu. Wanafunzi wa shule za msingi Moi Avenue na CGHU walitumia vivumishi vya idadi isiyodhihirika kwa namna isiyofaa katika sentensi zao. Watafitiwa waliviendeleza vivumishi kwa namna isiyoingiliana na nomino husika na hivyo basi kuzifanya sentensi kukosa upatanisho wa kisarufi. Katika sentensi 15c), mtafitiwa anatumia irabu -u- badala ya -i- anapoandika kuwa "**Nilitumia misitari muchache sana....**" Ikumbukwe kuwa, nomino misitari imo katika hali ya wingi na hivyo basi, herufi -i- ndio mwafaka. Vile vile, mtafitiwa katika sentensi ya15e), anatumia kivumishi *mdogo* kurejelea nomino *chakula* anapoandika kuwa "**....aliwekewa chakula mdogo mdogo tu....**" Nomino *chakula* inapatikana katika ngeli ya KI-VI na hivyo basi kivumishi kinapaswa kuanza na kiambishi awali ki- na vi- katika hali ya umoja na wingi mtawalia. Matumizi ya kiambishi awali m- katika mzizi -dogo yanaifanya sentensi kukosa uwiano baina ya nomino na kivumishi chake. Hii ni athari inayotokana na Kiingereza ambacho hakina suala la ngeli ila kilicho muhimu ni maneno kuwa na muoano mzuri katika sentensi. Hii

ndio sababu unapata nomino tofauti tofauti hutumia kivumishi kile kile katika Kiingereza kama vile:

- 16.** a) The baby is small. (Mtoto ni mdogo)
- b) Add me a small amount of food. (Niongeze chakula kidogo.)

Kivumishi *small* kimetumiwa kuvumisha nomino mtoto na vile vile chakula katika Kiingereza. Ingawa hivyo, hali hii ni tofauti katika Kiswahili kama ambavyo tulionyesha katika tafsiri ya Kiswahili kwenye mabano. Tulionyesha kuwa kivumishi mwafaka cha idadi ya nomino *mtoto* ni *mdogo* huku neno *kidogo* kikivumisha nomino chakula. Ni kwa misingi hii ambapo tunasema kuwa tofauti hii baina ya Kiswahili na Kiingereza husababisha athari hasi kwa kuwafanya wanafunzi kushindwa kuzingatia mtindo wa uandishi wa insha za Kiswahili.

Tulishughulikia athari hasi za Kiingereza katika sintaksia ya Kiswahili kama ilivyobainika katika insha za wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue. Tulionyesha kuwa watafitiwa wanashindwa kumudu matumizi ya aina mbalimbali ya vivumishi katika sentensi zao kwa sababu ya kuathiriwa na Kiingereza. Watafitiwa walishindwa kumudu lugha ya Kiswahili kwa kuathiriwa na Kiingereza kiasi cha kuwafanya kuunda sentensi zisizo sahihi kwa kutumia vivumishi kwa namna isiyofaa. Athari hii hasi inasababishwa na umudu lugha wa kijamii ambao huathiri pia umudu lugha wa kibinagsi. Wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue wanashindwa kumudu lugha ya Kiswahili kutokana na athari hasi ya Kiingereza hasa wanapoandika insha. Nadharia ya uchanganuzi makosa inaangazia aina mbalimbali za makosa yanayojitokeza katika mawasiliano na kuelezea visababishi vyake. Makosa yaliyojitokeza katika insha za watafitiwa ni ya kijumla na ambayo yalibainisha kuwa wanashindwa kumudu lugha ya Kiswahili kutokana na kujuu lugha zaidi ya moja. Data tuliyoitumia katika sehemu hii inabainisha kuwa hali ya kufunzwa na kutahiniwa kwa mitihani mingi kwa lugha ya Kiingereza ikilinganishwa na Kiswahili inawafanya wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue kukosa kuzingatia upatanisho wa kisarufi wanapoandika insha. Kutokana na data ya utafiti huu, pia, tulibaini kuwa wanafunzi wa shule za msingi waliathiriwa na Sheng' katika insha zao kama ambavyo tulionyesha katika sehemu ifuatayo:

## **4.2 Athari za Sheng' Kisintaksia Katika Uandishi wa Insha za Kiswahili**

Sheng'ni lugha vipindi ambayo hutumiwa katika miji mingi humu nchini Kenya (Njoroge, 2014). Watumizi wa Sheng' huunda misamiati kwa njia sahili na hubadilika kila uchao. Kilicho muhimu kwa Sheng' ni kuwasilisha ujumbe kwa wanakundi kwa nia ya kuficha siri zao na wala sio usahihi wa sentensi. Hali hii inaathiri wanafunzi ambao walikulia katika mazingira ambamo Sheng' inatumiwa katika mawasiliano. Data ya utafiti huu ilionyesha kuwa wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue waliathiriwa na Sheng' kisintaksia. Katika Sheng', misamiati huundwa kiholela na kwa njia sahili, kilicho muhimu ni kuwasilisha ujumbe kwa wanakundi. Watafitiwa walidhihirisha hali ya kutozingatia kanuni za uundaji wa Kiswahili wanapoandika insha zao na badala yake kufuata zile za Sheng'. Kwa hali hii basi, sentensi inakosa upatanisho wa kisarufi kama tulivyoonyesha katika kisehemu kifuatacho:

Awali tulionyesha kuwa watumizi wa Sheng' huunda misamiati ya lugha hii kwa njia sahili. Mbinu mbalimbali hutumiwa kuunda misamiati ya Sheng' na wala hawana kanuni maalum za uundaji wa sentensi. Sentensi za wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue hukosa upatanisho wa kisarufi. Upatanisho wa kisarufi ni ule uandishi unaotumia maneno ambayo yanaingiliana vizuri katika sentensi kwa kuzingatia ngeli. Nadharia ya kumudu inaashiria kuwa mazingira anamolelewa mtu huathiri tabia zake za kimawasiliano. Watafitiwa wetu kama tulivyosema awali ni kuwa wanatoka mitaa ambamo Sheng' hutumiwa na hivyo basi wao wanaathiriwa na ndio sababu wanatumia mitindo ya mawasiliano ya Sheng' katika insha zao. Nadharia ya uchanganuzi makosa pia inashughulikia suala la kutozingatia sheria za lugha husika katika mawasiliano. Ukosefu wa kuzingatia sheria za lugha husika zinawafanya wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue kuandika sentensi za Kiswahili kwa kutumia mtindo wa Sheng'. Athari ya Sheng' kwa watafitiwa inabainikakwa aidha kutumia mbinu ya uhuishaji pasipofaa, kuchopeka silabi au virejeshi pasipofaa na vile vile kutumia maneno ya Sheng' katika sentensi za Kiswahili. Haya ndio tuliyoyashughulikia katika vijisehemu vifuatavyo kuonyesha athari za Sheng' kisintaksia katika insha za Kiswahili.

### **4.2.1 Matumizi ya Mbinu ya Uhuishaji Pasipofaa**

Athari za ulumbilugha katika uandishi wa insha zinawafanya wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue kufanya makosa ya kisarufi. Kutokana na data ya utafiti huu tulibaini kuwa wanafunzi hutumia mbinu ya uhuishaji katika insha zao kwa namna isiyofaa na kuwafanya

kupotoka kisarufi. Hili linatokana na mazoea ya watumizi wa Sheng' ambao wakati mwingine huvipa vitu sifa za kibinadamu. Uhuishaji ni mbinu ya kifasihi ya kuvipa vitu uwezo wa kibinadamu kama vile gari lilisalimu amri. Mwanadamu ndiye anaweza kusalimu amri ilhali katika sentensi hii, gari limepewa uwezo huu wa kuwaza au kutenda kama mwanadamu. Tulibaini kuwa wanafunzi hifuata mtindo huu katika uandishi wao wa insha kwa namna isiyofaa. Tunasema hivi kwa sababu matumizi ya mbinu ya uhuishaji katika insha yanapaswa kufanywa kwa ubunifu mkubwa ili kudumisha maana na vile vile kuzingatia upatanisho wa kisarufi. Matumizi ya mbinu ya uhuishaji kwa namna isiyofaa huchukuliwa kuwa kosa la kisarufi. Hii ina maana kuwa wanafunzi atapata alama za chini ikilinganishwa na wenzao ambao hawana makosa ya kisarufi. Matumizi ya uhuishaji usiofaa katika insha za wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue yanadhihirika katika sentensi zifuatazo:

- 17. a)Mimi hupanda mimea ambayo hunichekelea kila ninapoitengeneza.**  
**b) Shule yetu hupenda wageni sana.**

Watafitiwa walitumia mbinu ya uhuishaji katika sentensi 17a) na b). Hata hivyo, mbinu hii haijaendelezwa kwa ubunifu unaofaa na ndio sababu sentensi hizi zinakosa umantiki na pia sio sahihi kisarufi. Kinachojitokeza katika sentensi hizi ni kuwa wanafunzi hawa wa Moi Avenue na CGHU wanakosa kuzingatia upatanisho wa kisarufi katika sentensi kwa kutumia mbinu ya uhuishaji visivyo.

Uhuishaji unajitokeza katika sentensi ya 17a) na b), ambapo watafitiwa waliipa mimea na shule uwezo wa kibinadamu. Katika sentensi ya 17a), mtafitiwa anaandika kuwa “.....**mimea ambayo hunichekelea.....**” Mimea imepewa uwezo wa kibinadamu kwa kuwa haiwezi kumchekelea mtu. Sentensi hii inaelekea kutolewaka kwa sababu ya matumizi ya mbinu ya uhuishaji. Hali hii pia inajitokeza katika sentensi ya 17b), mtafitiwa anapoandika kuwa “**Shule yetu hupenda wageni sana**”. Mtafitiwa huyu anaihuisha nomino shule kwa kusema kuwa inapenda wageni. Uhuishaji huu unamwacha msomaji na kutaka kubaini mwanafunzi alikuwa anakusudia kuandika nini. Mtafitiwa huyu ameathiriwa na Sheng' ambayo hutaka tu kuwasilisha ujumbe bila kuzingatia kanuni za uundaji wa sentensi. Athari hasi ya Sheng' kwa watafiwa wanapoandika insha za Kiswahili inaashiria kuwa waliathiriwa na mazingira. Haya ni kwa mujibu wa nadharia ya kumudu ambapo waasisi wake wanasema kuwa mazingira huathiri tabia za watu hivi kwamba wao huzungumza au kuandika kutegemea hali na mazingira wanamokulia. Athari hizi hasi za

Sheng' pia zinawafanya watafitiwa wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue kuchopeka viambishi pasipofaa wanapoandika insha za Kiswahili kama inavyobainika katika kisehemu kifuatacho:

#### **4.2.2 Kuchopeka Silabi au Virejeshi Pasipofaa**

Viambishi ni viungo vya maneno vilivyo na maana kisarufi na ambavyo hufungamanishwa kwa mzizi wa neno. Viambishi ni muhimu katika maneno kwa kuwa huyapa maneno maana mbalimbali. Viambishi ambavyo huambishwa katika neno sharti viingiliane na mzizi wa neno. Ingawa hivyo, tuligundua kuwa watafitiwa huchopeka viambishi katika neno bila kuzingatia mwingiliano wake na mzizi wa neno husika kama inavyobainika katika sentensi zifuatazo:

**18. a) Paka akona miguu nne akona rangi nyeusi na anakula nyamas.**

**b) Tunafanyanga kazi ya kuchunga mbuzi zetu.**

**c) Mimi na rafiki yangu Wango tunapandanga matatu moja**

**kwenda nymbani.**

**d) Tulikula chakula cha majioni na tukalala.**

Katika sentensi 18a), mtafitiwa anaiendeleza visivyo kwa kutozingatia upatanisho wa kisarufi. Mwanafunzi wa shule ya msingi ya CGHU anaongezea viambishi kwa namna isiyofaa katika sentensi. Hali hii inaashiria uundaji wa msamati sahili ambao hujitokeza zaidi katika Sheng'. Kutokana na sentensi, "**Paka akona miguu nne akona rangi nyeusi na anakula nyamas,**" neno *akona* limeendelezwa visivyo kwa kuongezewa kiambishi -ko- na vile vile limerudiwa. Uradidi wa maneno katika sentensi ni mbinu mwafaka ya kuonyesha msisitizo. Hata hivyo, sio urudiaji wote unakuwa mwafaka kama katika mfano huu wa sentensi ya mwanafunzi wa shule ya msingi. Mwanafunzi amelirudia neno ambalo ameliendeleza visivyo kutokana na athari ya lugha ya Sheng' ambayo haizingatii kanuni yoyote katika uundaji wa sentensi. Mtafitiwa alipaswa kuandika, *ana* badala ya kuongezea kiambishi -ko- ambacho kinaifanya sentensi kutokuwa na upatanisho wa kisarufi.

Katika Kiswahili, kiambishi cha kuonyesha hali ya mazoea katika sentensi huwa ni *hu-*. Kwa mfano, *Wanafunzi hunywa uji shulen*. Hata hivyo, kutokana na athari ya Sheng' watafitiwa wa

shule za msingi za CGHU na Moi Avenue hutumia kiambishi tamati –nga kuonyesha hali ya mazoea. Hili linajitokeza katika sentensi ya18,b) na c), ambapo watafitiwa waliandika kuwa “**Tunafanya kazi ya kuchunga mbuzi zetu**” na “.....**tunapandanga matatu moja.....**” Kulingana na wanafunzi hawa, sentensi hizi zimo katika hali ya mazoea. Hii inaonyesha kuwa wanafunzi amba ni wanaulumbilugha wanatumia kiambishi –nga kuashiria hali ya mazoea ilhali katika Kiswahili hali ya mazoea huwakilishwa na hu-. Matumizi ya –nga kuashiria hali ya mazoea ni athari inayotokana na Sheng’ ambayo ni lugha vipindi. Lugha vipindi huunda misamiati mipyka kila uchao tofauti na lugha ya Kiswahili iliyo na mtindo thabiti wa uundaji wa msamiati.

Mifano iliyopo hapo juu inaonyesha pia kuwa watafitiwa wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue huongezea viambishi kwa vielezi. Hii ni licha ya kuwa viambishi huongezwa zaidi kwa vitenzi ili kuleta maana mbalimbali. Vile vile, baadhi ya nomino na vivumishi huongezewa viambishi awali. Hata hivyo, ni nadra sana kwa vielezi na hasa vya wakati kuongezewa viambishi awali kama alivyofanya mtafitiwa anapoandika sentensi 18c), “**Tulikula chakula cha majioni na tukalala.**” Neno *majioni* limeendelezwa vibaya na kuifanya sentensi nzima kutokuwa sahihi. Tatizo lililopo hapa ni kuongezea kiambishi awali ma- katika kielezi jioni. Hii ni athari nyingine pia ya Sheng’ kwa wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue. Watafitiwa walishindwa kumudu kuandika sentensi sahihi za Kiswahili kwa kuathiriwa na Sheng’ ambayo huzungumzwa wanamokulia. Vile vile tulibaini kuwa wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue wanatumia maneno ya Kiswahili visivyo kamatulivyoonyesha katika data iliyo katika kisehemu kinachofuata:

#### **4.2.3 Matumizi ya Maneno ya Kiswahili Visivyo**

Athari ya ulumbilugha na hasa Sheng’ inadhihirika pia katika insha za wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue kiasi cha kuwafanya kukosa kuzingatia ngeli za nomino husika katika sentensi. Kama tulivyosema awali, nomino za Kiswahili huwekwa katika makundi ya ngeli ambayo huzingatiwa wakati wa kuandika sentensi. Zipo ngeli za Kiswahili kimofolojia na vile vile kisintaksia. Katika mofolojia, neno ndilo msingi wa uanishaji kinyume na sintaksia ambapo sentensi huzingatiwa. Katika shule za msingi, wanafunzi hufunzwa ngeli za kimofolojia. Wanafunzi wanatakiwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi katika sentensi kwa kuhakikisha kuwa maneno yanaingiliana vyema. Hata hivyo, data ya utafiti huu ilionyesha kuwa wanafunzi wa

shule za msingi za CGHU na Moi Avenue wanakosa kuzingatia upatanisho huu wa kisarufi na badala yake kutumia lugha kiholela kama wafanyakyo watumizi Sheng'. Athari hii ya Sheng' ya kutumia lugha kiholela inajitokeza katika mifano ifuatayo ya insha za wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue:

- 19. a) Paka inamea kuanzia ndogo habi kubwa.**
- b) Mimi nina penda paka yeye ana itwa abubu.**
- c) Nilipand mimea zinaitwa carroti.**
- d) Tulipo ingia ndani tulipata chenda la ndizi na vitu zingine.**

Sentensi hizi zinaashiria athari hasi ya Sheng' kwa wanafunzi wa shule za msingi CGHU na Moi Avenue. Hili linadhihirika katika sentensi ya 19a), ambapo mtafitiwa anaunda sentensi ambayo sio sahihi kisarufi na isiyo na mantiki anapoandika kuwa "**Paka inamea kuanzia ndogo habi kubwa na Paka inaitwa tama.**" Umantiki unakosekana katika sentensi hii kwa kuwa mtafitiwa hakuzinagtia ngeli ya nomino ambayo ni msingi wa sentensi husika. Nomino paka, inapatikana katika ngeli ya A-WA na hivyo basi, mwanafunzi wa shule ya msingi ya Moi Avenue alitakiwa kuzingatia hili alipokuwa akiandika vitenzi katika sentensi hizi mbili. Vile vile, paka ni mnyama na hivyo hamei bali hukua. Mimea ndio humea na hii ndio maana tunasema kuwa sentensi hii inakosa umantiki. Mtafitiwa alipaswa kuandika kuwa *paka anakua kuanzia mdogo hadi kuwa mkubwa*. Sentensi hii ingekuwa na mantiki na sahihi kisarufi na hivyo basi kueleweka na wasomaji. Namna mwanafunzi huyu anaandika inaonyesha kuwa ameathiriwa na Sheng' kwa kuwa maneno, *mea na kua hurejelewa* kwa neno moja tu growkatika Kiingereza. Tunasema hivi kwa sababu tulibaini kuwa watumizi wa Sheng' huyatumia maneno haya kwa maana moja hata wanaporejelea kukua kwa watoto. Athari hii ni hasi kwa kuwa mtafitiwa anakosa kuzingatia kuwa Kiswahili na Sheng' ni lugha mbili tofauti na ambazo zina upekee wake hasa katika uundaji wa misamiati yake na vile vile sentensi. Tunasema hivi kwa kuwa nomino katika Kiswahili hugawanywa katika ngeli mbalimbali, jambo ambalo halizingatiwi katika Sheng'.

Katika sentensi ya 19b), mwanafunzi wa shule ya msingi ya CGHU anapachika maneno ambayo sio muhimu katika sentensi na kuifanya kukosa upatanisho wa kisarufi. Kwa maoni yetu, mtafitiwa anajirudia kwa kutumia maneno yanayofanya kazi ile ile katika sentensi. Hili

linabainika anapoandika kuwa “**Mimi nina penda paka yeye ana itwa abubu.**” Mwanafunzi wa shule ya msingi ya CGHU anatenganisha maneno ambayo kwa uhalisia ni neno moja, kwa mfano, *nina penda na ana itwa*. Maneno haya yanapaswa kuandikwa kama ninapenda na anaitwa mtawalia. Ingawa hivyo, kutokana na athari za ulumbilugha na hasa Sheng’ ambayo haizingatii kanuni katika uundaji wa maneno, mwanafunzi ambaye ni mwanawingilugha alitenganisha maneno kinyume na kanuni za lugha ya Kiswahili. Vile vile, mtafitiwa alitumia nomino na kiwakilishi katika sentensi sahili. Ikumbukwe kuwa kiwakilishi husimama badala ya nomino katika sentensi. Kwa hivyo basi, nomino na kiwakilishi havipaswi kutumika katika sentensi moja na hasa sentensi sahili. Kwa hali hii basi, mwanafunzi hakutakiwa kuongezea kiwakilishi yeye baada ya kuandika paka na hivyo sentensi sahihi ilitakiwa kuwa “**Ninampenda paka anayeitwa Abubu.**” Hii inaonyesha kuwa katika Kiswahili, kirejeshi O hutumiwa katika sentensi ili kuondoa urudiaji wa maneno kwa namna isiyofaa katika sentensi.

Nomino mimea imo katika ngeli ya U-I na hili linapaswa kujitokeza katika sentensi. Ingawa hivyo watafitiwa wa utafiti huu waliashiria kuwa hawafuati ngeli za nomino wanapounda sentensi za Kiswahili. Ukosefu wa kuzingatia ngeli za nomino husika katika sentensi kwa sababu ya kuathiriwa na matumizi ya Sheng’ ambapo lugha hutumiwa kiholela bila kuzingatia kanuni zozote. Hili linabainika katika sentensi ya 19c), mwanafunzi anapoandika kuwa “**Nilipand mimea zinaitwa caroti.**” Mtafitiwa huyu ametunga sentensi inayoonyesha kuwa nomino mimea imo katika ngeli ya I-ZI. Hili ni kosa kwa kuwa nomino ambazo hupatikana katika ngeli hii ni zile ambazo hazibadiliki katika umoja na wingi kimuundo, kukiwemo sindano, ndoo, ndizi na balskeli. Nomino mmea hubadilika katika wingi na kuwa mimea. Hii basi inaonyesha kuwa haiwezi kuwa katika ngeli ya I-ZI ila mwanafunzi anakosa kufuata hili kutokana na athari ya Sheng’. Nomino zilizo katika ngeli ya U-I kama mmea huchukua kiambishi awali U katika umoja na I katika wingi ili kuleta upatanisho wa kisarufi. Kwa hivyo basi, sentensi sahihi inapaswa kuwa *nilipanda mimea inayoitwa karoti*. Sentensi hii ni sahihi kisarufi kwa kuwa imezingatia ngeli ya nomino mimea.

Nomino ndizi imo katika ngeli ya I-ZI kwa kuwa kumuundo, haibadiliki katika umoja na wingi. Mtafitiwa katika sentensi ya19d), aliiendeleza vibaya anapoandika “**Tulipo ingia ndani tulipata chenda la ndizi na vitu zingine.**” Neno ambalo limeifanya sentensi hii kutokuwa sahihi kisarufi ni *zingine*. Mtafitiwa alikusudia kuandika nomino vitu ambayo imo katika ngeli ya KI-

VI. Kwa hivyo sentensi sahihi inatakiwa kuwa *tulipoingia ndani ya gari tulipata chenda la ndizi na vitu vingine*. Sentensi hiiina nomino mbili na hivyo uandishi wake unategemea ile inayorejelewa. Katika sehemu ya pili ya sentensi hii, nomino inayorejelewa ni vitu na hivyo neno linalofuata linapaswa kuanza kwa kiambishi vi-. Hata hivyo, mwanafunzi anafanya kosa kwa kuanza na kiambishi zi- ilhali anarejelea nomino vitu. Sentensi inakosa upatanisho wa kisarufi na hili linabainisha athari hasi ya Sheng' kwa Kiswahili kisintaksia. Makosa ambayo yalibainika katika mifano ambayo tulirejelea hapa juu yamesababishwa na hali ya watumizi wa Sheng' kutumia lugha kiholela. Wanafunzi vile vile wanakosa kuzingatia kanuni za uandishi wa sentensi za Kiswahili kwa kuwa kama tulivyosema awali, kulingana na nadharia ya kumudu, mazingira huathiri namna watu huwasiliana aidha kwa maandishi au mazungumzo. Katika utafiti huu, tulijikita katika insha za Kiswahili za wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue na kubaini kuwa waliathiriwa na Sheng' kupitia kwa namna wanavoendeaza sentensi zao.

Katika kisehemu hiki, tulishughulikia athari hasi ya Sheng' kwa wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue kupitia kwa uundaji wa sentensi ambazo sio sahihi kisarufi. Tulionyesha kuwa watumizi wa Sheng' hutumia lugha kiholela na hasa wanapounda sentensi kinyume na ilivyo katika Kiswahili ambacho ni lugha iliyo thabiti na kanuni zake za uundaji wa sentensi kama inavyoelezewa katika nadharia ya kumudu na ile ya uchanganuzi makosa. Nadharia hizi zilionyesha kuwa watu hutumia lugha kutegemea na mazingira wanapolelewa na hii ndio maana wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue walifuata kanuni za Sheng' walipoandika insha za Kiswahili. Watafitiwa wetu walidhihirisha kuwa waliathiriwa na Sheng' kutokana na data tuli yoishughulikia hapo juu. Vile vile, tuligundua kuwa wanafunzi wa shule za msingi hutumia maneno ya Sheng' katika insha zao na hili ni jambo ambalo haliruhusiwi kamwe. Haya ndio tuliyajadili katika kisehemu kifuatcho:

#### **4.2.4 Matumizi ya Maneno ya Sheng' Katika Insha za Kiswahili**

Sheng' huunda misamiati yake kutoka kwa lugha zingine kukiwemo Kiswahili, Kiingereza na za Asili kama vile Kikuyu na Kidholuo. Maneno mengine hufanana sana na yale ya Kiswahili kiasi cha kuwakanganya wanafunzi ambao hudhania kuwa ni sahihi ama hata kuyatumia wanapoandika insha. Maoni yetu ni kuwa watafitiwa wetu hutumia maneno ya Sheng' wanapoandika insha za Kiswahili bila kukusudia na wala hawajui kama ni makosa. Matumizi ya maneno ya Sheng' katika uandishi wa insha za Kiswahili ni makosa kwa kuwa huathiri usarufi

wa sentensi husikakama inavyobainika katika mifano ifuatayo ya wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue:

- 20. a) Baba yangu unitengea nyumbani.....**
- b) Siku moja nilikuwa nimeenda kubai nyama na spinach.**
- c) Babangu alitubaiya nguo mzuri na kiatu.....**

Athari hasi za Sheng' zinajitokeza katika mifano ambapo wanafunzi wanaashiria kuwa waliathiriwa na ulumbilugha. Mtafitiwa anatumia neno la Sheng' katika insha katika sentensi, 20a), anapoandika kuwa "**Baba yangu unitengea nyumbani.....**" Neno *unitegea* ni la Sheng' kwa maana ya kusubiri katika lugha ya Kiswahili. Wanafunzi aliongezea herufi **n** kwa neno la Sheng' *tegea* kutokana tu na athari za lugha ya kwanza ila matumizi yake katika sentensi yanadhihirisha maana aliyokusudia kuwasilisha. Hii inabainisha kuwa mtafitiwa aliathiriwa na Sheng' kiasi cha kutumia misamiati yake anapoandika insha ilhali amepewa maagizo kuwa atumie Kiswahili peke yake. Hata hivyo, wanafunzi alitakiwa kuandika sentensi sahihi ambayo ni: *Baba yangu hunisubiri nyumbani*.

Katika sentensi ya 20b), nac), watafitiwa wanaswahilisha neno la Kiingereza *buy* kutokana na athari hasi ya Sheng' ya uundaji wa misamiati kutoka kwa lugha zingine. Hili linabainika watafitiwa wetu wanapoandika kuwa "**Siku moja nilikuwa nimeenda kubai nyama na spinach**" na "**Babangu alitubaiya nguo mzuri na kiatu.**" Maneno, **kubai** na **alitubaiya** yameswahilishwa kutoka kwa lugha ya Kiingereza. Hii ni licha ya kuwa kuna neno lake mwafaka katika Kiswahili na ambalo ni *nunua*. Neno hili la Kiswahili limezoleka kwa kuwa limetumiwa kwa muda mwangi katika Kiswahili na hivyo basi hatuwezi kusema kuwa wanafunzi wa shule za msingi wanakosa kulijua. Ni kwa misingi hii ambapo tunadai kuwa wanafunzi wa shule za msingi wanaswahilisha maneno ya Kiingereza kwa sababu ya kuathiriwa na Sheng'. kwa hivyo basi, sentensi sahihi zinapaswa kuwa, *siku moja nilikuwa nimeenda kununua nyama na spinachi na babangu alitununulia nguo nzuri na viatu*.

Tulionyesha athari hasi za ulumbilugha kwa wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue kwa kujikita kwa Kiingereza na Sheng'. Tulionyesha kuwa watafitiwa hawa hukosa kuzingatia upatanisho wa kisarufi katika sentensi za Kiswahili. Hili lilibainika kupitia kwa matumizi mabaya ya vivumishi na vile vile kutozingatia ngeli za nomino husika katika sentensi.

Pia, tulibainisha kuwa watafitiwa huswahilisha maneno au kutumia maneno ya Sheng' katika insha zao ilhali misamiati ipo kurejelea dhana ambazo walizitumia kwenye sentensi zao. Wanafunzi wanakosa kuzingatia kanuni za uandishi za lugha ya Kiswahili na hivyo basi kutumia sheria ambazo hazitoshelezi mahitaji yake ya kimawasiliano kama ambavyo waasisi wa nadharia ya uchanganuzi makosa wanavyoelezea. Vile vile, nadharia ya kumudu inaonyesha kuwa watu huweza kushindwa kumudu matumizi ya lugha ya Kiswahili kutokana na kuathiriwa na ulumbilugha. Hii ni athari hasi ya ulumbilugha kama iliyojitekeza katika insha za watafitiwa. Ingawa hivyo zipo athari chanya za ulumbilugha kwa wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue kama ambavyo tulijadili katika kisehemu kinachofuata:

#### **4.3 Athari Chanya za Ulumbilugha Katika Sintaksia**

Waasisi wa nadharia ya kumudu wanaeleza kuwa wanaulumbilugha hutumia lugha fulani kutegemea umuhimu wake na uwezekano wa kutumia lugha hiyo katika muktadha husika. Wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue walidhihirisha athari chanya za ulumbilugha na hili linabainisha kuwa wanamudu lugha wanazozijua katika miktadha fulani fulani. Wanafunzi amba ni wanaulumbilugha huweza kutunga sentensi kamilifu, kimaana na kimantiki baada ya kugundua kuwa kila lugha ina upekee wake. Wanaulumbilugha huweza kuswahilisha neno iwapo watakosa msamiati mwafaka katika Kiswahili. Hii ni kutokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia. Mabadiliko haya yanapotokea, misamiati inapaswa kubuniwa katika lugha zingine. Hata hivyo, wakati mwingine misamiati hii huchukua muda kubuniwa na hivyo basi mbinu ya utohozi hutumiwa. Utohozi unawezakana iwapo tu watu ni wanaulumbilugha amba wataelewa dhana zinazotumiwa kurejelea kitu fulani.

Data ya utafiti huu ilikusanywa wakati wa janga la korona. Huu ni ugonjwa amba unaasambaa mionganini mwa watu na kuwaathiri wengi. Kutokana na tandavu ya korona, watu walishauriwa kujikinga kwa kufanya mambo ambayo ni mageni kwao. Mojawapo wa njia za kujikinga dhidi ya virusi vya korona ni kuva barakoa, kunawa mikono kwa maji yanayotiririka au kutumia vieuzi. Virusi hivi ni vipya, njia za kujikinga pia zilikuwa mpya na hivyo basi, maneno yaliyotumiwa kurejelea ugonjwa wa korona yalikuwa ya Kiingereza. Njia za kuunda misamiati katika Kiswahili ni nyingi kukiwemo, tafsiri sisisi, utohozi na kuunganisha maneno mawili na kulifanya neno moja. Kutokana na tandavu ya korona, utohozi ulikuwa mbinu mwafaka ya kuunda misamiati yake mwafaka. Kwa hivyo, wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi

Avenue ambao ni wanaulumbilugha walitumia utohozi kurejelea mambo mbalimbali yaliyohusiana na virusi vya korona kama inavyobainika katika sentensi zifuatazo:

**21. a) Tulivaa maski tulipoenda kanisani.**

**b) Ugonjwa wa korona ulienea sana.**

**c) KOVID-19 ni mbaya sana kwa watu.**

Kutokana na sentensi 21a), b), na c), mbinu ya utohozi ambayo inahusu kuswahilisha neno kwa kuliendeleza kwa kufuata muundo wa Kiswahili. Maneno, **maski**, **korona** na **KOVID-19** yametoholewa kutoka kwa Kiingereza. Maneno haya yameendelezwa kwa njia sahihi kwa kufuata muundo wa uundaji wa silabi za Kiswahili ipasavyo. Utahozi wa aina hii huweza kufanywa na wanaulumbilugha ambao wanajua muundo wa silabi za Kiswahili. Hali ya kujua muundo wa silabi wa lugha nyingine kama vile Kiswahili huwa na miundo ifuatayo:

**22. a) Konsonanti vokali kama vile ba-ba (baba).**

**b) Vokali kama vile a-u (au).**

**c) Konsonanti konsonanti vokali kama vile mbe-le (mbele)**

**d) Konsonanti konsonanti konsonanti vokali kwa mfano mbwa**

**e) Konsonanti kama vile maalu-m (maalum)**

Kutokana na miundo hii ya silabi za Kiswahili, tunaweza kusema kuwa wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue walitoho maneno ya Kiingereza na kuyaswahilisha ipasavyo. Tunasema hivi kwa sababu, katika Kiingereza neno **mask** limekamilika kwa konsonanti hali ambayo ni nadra kwa maneno ya Kiswahili yenye asili ya kibantu. Hivyo basi, hali ya kuongezea irabu i katika neno **mask** na kulifanya kusomeka kama **maski** nikuonyesha kuwa mwanafunzi anajua mbinu mbalimbali za uundaji wa msamiati wa Kiswahili na ambazo anazitumia ipasavyo. Mbinu mojawapo ya uundaji wa msamiati wa Kiswahili ni utohozi kama ilivyobainika katika insha za wanafunzi. Hii ni athari chanya ya ulumbilugha kwa wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue.

Kutokana na mifano ya sentensi 21b), na c), maneno **korona** na **KOVID-19**, yametoholewa. Watafitiwa wetu walitumia herufi **k** ya Kiswahili mahali ambapo palikuwa na **c** ya kiingereza. Hii inabainisha kuwa watafitiwa walielewa herufi ambazo hupatikana katika lugha fulani na pia wanajua kuwa mtu anapotohoa neno anapaswa kutumia herufi mwafaka zinazopatikana katika

lugha husika. Vile vile hii ni athari chanya ya ulumbilugha kwa wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue.

Athari chanya za ulumbilugha ambazo tulizishughulikia zinaonyesha kuwa wanaulumbilugha wanaweza kubainisha herufi za lugha fulani na vile vile kuunda neno kwa kufuata utaratibu wa lugha ya Kiswahili. Kwa hali hii basi, tunaweza kusema kuwawanaulumbilugha wana uwezo wa kutunga sentensi ambayo imekamilika kimaana na sahihi kimantiki katika Kiswahili hata baada ya kutohoa neno kutoka kwa Kiingereza. Utahozi wa maneno ambayo wanafunzi wa shule za msingi hawayajui katika Kiswahili huwawezesha kujieleza vizuri bila kukosa msamiati wa kutumia katika sentensi husika. Matumizi ya utahozi kwa maneno ambayo msamiati wake haujazoeleka katika Kiswahili ni athari chanya ya ulumbilugha kwa kuwa watafitiwa wanafidia msamiati kwa namna inayofaa. Wanafunzi wa shule za CGHU na Moi Avenue ambao walitumia utahozi katika insha zao walidhahirisha kuwa waliweza kumudu lugha ya Kiswahili hata ingawa wao ni wanaulumbilugha. Wanafunzi hawa walidhahirisha kuwa maoni ya waasisi wa nadharia ya kumudu yalikuwa sawa wanaposema kuwa wanaulumbilugha hutumia lugha fulani kutegemea umuhimu wake na uwezekano wa kutumia lugha hiyo katika muktadha husika na hili liliwawezesha kutohoa maneno kutoka kwa lugha ya Kiingereza kwa mtindo mwafaka wa lugha ya Kiswahili.

#### **4.4 Hitimisho**

Katika sura hii, tulishughulikia athari hasi na chanya za Kiingereza na Sheng' kisintaksia. Tulionyesha kuwa wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na wenzao wa Moi Avenue ni wanaulumbilugha ambao waliathiriwa na Kiingereza na Sheng' katika insha zao za Kiswahili. Tulionyesha kuwa athari hasi za ulumbilugha zinazojitokeza kisintaksia kwa wanafunzi hawa ni kutumia vivumishi kwa namna isiyoambatana na nomino husika katika sentensi, kukosa kuzingatia upatanisho wa kisarufi katika sentensi za Kiswahili na hili ni jambo ambalo husababishwa na kutozingatia ngeli za nomino za Kiswahili. Athari hizi zinaifanya sentensi kutokuwa sahihi kisarufi na vile vile kimantiki. Pia tulishughulikia athari chanya na kusema kuwa ulumbilugha huwawezesha wanafunzi wa shule za msingi kwa kutohoa misamiati hasa inayohusiana na janga la korona ambalo lilijitokeza mwaka wa 2020, Disemba. Kutokana na data ya utafiti huu, tunaweza kusema kuwa athari hasi za ulumbilugha ni nyingi ikilinganishwa na

chanya. Athari hizi hasi huwafanya watafitiwa kupata alama za chini ikilinganishwa na wenzao ambao wanazingatia kanuni za uandishi wa insha za Kiswahili.

## SURA YA TANO

### MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

#### 5.0 Utangulizi

Sura hii, inashughulikia muhtasari, mahitimisho na mapendekezo yanayohusiana na matokeo ya utafiti huu. Tuliangazia maswali ya utafiti wetu ili kubaini kama yanaoana au kukinzana na matokeo ya utafiti huu kwa mujibu wa data ya utafiti huu. Hatimaye tulitoa mapendekezo kwa tafiti za baadaye kuhusiana na athari hasi na chanya za ulumbilugha kwa watafitiwa na vile vile tuliorodhesha changamoto tulizokumbana nazo wakati wa kukusanya data kwa ajili ya utafiti huu.

#### 5.1 Muhtasari

Katika sura ya kwanza, tulishughulikia mambo ya kimsingi kuhusiana na tasnifu hii ambapo tulionyesha suala kuu la utafiti huu. Katika utafiti huu, tuliongozwa na malengo matatu katika kushughulikia tatizo la utafiti wetu. Malengo hayo ni: kwanza, kuchanganua athari hasi za Sheng' na Kiingereza kwa Kiswahili katika uandishi wa insha za wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue. Pili, kuchunguza athari chanya za Sheng' na Kiingereza kwa Kiswahili katika uandishi wa insha za wanafunzi wa shule za msingi za CGHU na Moi Avenue. Tatu, kuchanganua sababu ambazo huwafanya wanafunzi wa shule za msingi kupendelea Sheng' au Kiingereza zaidi kuliko Kiswahili na jinsi mitazamo yao ya Sheng' na Kiingereza huathiri maandishi yao ya insha za Kiswahili.

